BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Saba - Tarehe 13 Novemba, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydrofluocarbons* (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances);* na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development 3 Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development).*

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydrofluocarbons (HFCS) chini* ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances);* na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ratiba ya kikao cha leo Serikali inawajibika kuweka pia mezani Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ambayo inawasilishwa na Wizara ya Viwanda.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda na Biashara, Injinia Stella Manyanya.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization).*

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia yaani *Protocol Amending the Marakesh Agreement Establishing The World Trade Organization*.

MHE. JOYCE J. MUKYA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza Uzalishaji na 4 Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCS) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances);* na

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development).*

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA):

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Marakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(Protocol Amending The Marakesh Agreement Establishing The World Trade Organization)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu!

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 85

Kuongeza Madaktari Hospitali ya Gonja – Same

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Serikali inashirikiana na Hospitali ya Gonja chini ya KKKT na Hospitali hiyo inatoa huduma za upasuaji wagonjwa wengi kuliko Hospitali ya Wilaya ya Same. Aidha, Jimbo la Same Mashariki lenye Kata 14 lina Kituo kimoja tu cha Afya kilichoboreshwa hivyo kusababisha msongamano katika Hospitali ya Gonja:-

Je, ni lini Serikali itaongeza madaktari katika Hospitali ya Gonja ili iweze kuhudumia Kata tisa ambazo wagonjwa wake wanapata shida sana kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu Hospitali ya Wilaya ya Same?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Gonja ina jumla ya watumishi 50, kati ya hao watumishi 10 ni waajiriwa wa Serikali. Ili kupunguza changamoto ya uhaba wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya Same Serikali imepeleka watumishi wa kada mbalimbali za afya 68 katika Halmashauri ya Wilaya ya Same kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Oktoba, 2019. Serikali itaendelea kuajiri na kuwapanga watumishi wa kada mbalimbali za afya nchini kwa kutoa kipaumbele kwenye maeneo na vituo vyenye upungufu mkubwa ikiwemo Hospitali ya Gonja.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA Mheshimiwa Mwenyekiti, *yeah,* nashukuru kwa majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumueleza Waziri kwamba hospitali hii inafanya *operations* nyingi kuliko hata Hospitali ya Wilaya ya Same, na wagonjwa wengi wanapenda kuitumia. Niombe tu kwamba ufanye tathmini kuona kwamba kwa *volume* ya wagonjwa wanaokwenda hospitali ile, je, madaktari hao wanatosheleza?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu kwanza nimpongeze kwa dhati kabisa jinsi ambavyo Mhehsimiwa Mbunge amekuwa akipigania suala zima la afya kwa Wananchi wa jimbo lake na tulipata fursa ya kuteta na akasema aneo ambalo fedha zikipatikana tuongeze kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba Hospitali ya Wilaya ya Same ina idadi kubwa ya Wananchi ambao wanafanyiwa upasuaji ukilinganisha na hiyo ya Gonja; lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba tunashukuru kazi kubwa inayofanywa na hospitali hii na kwa kadri nguvu itakavyoongezeka na kupata wataalam wa kutosha hatutasahau kupeleka Hospitali ya Gonja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Aysharose N. Matembe Mbunge wa Viti Maalum, bado linaelekezwa Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Na. 86

Zahanati ya Mtisi Kuwa Kituo cha Afya

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE aliuliza:-

Kata ya Mtama katika Manispaa ya Singida haina Kituo cha Afya kwa ajili ya kuwahudumia wakazi wake na Sera ya Serikali inaelekeza kila kata kuwa na kituo cha afya.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuifanya Zahanati ya Mtisi kuwa kituo cha afya, ambayo ujenzi wake umekuwa wa kusuasua kutokana na Serikali kutopeleka fedha za kutosha

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imeidhinisha kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Mtisi kilichopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu safi kabisa, mafupi, *to the point.* Mheshimiwa Ndogholi.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii, na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI. Ninalo swali dogo moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa kuna umbali mrefu kutoka Kata ya Mtamaa hadi kufika Mjini kwenye hospitali ya mkoa; je, Serikali ina mpoango gani wa hara

kuhakikisha kwamba sasa Zahanati hii ya Mtisi inakuwa kituo cha afya? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Matembe kwa kazi kubwa ambayo anafanya katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma iliyobora ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimemhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetenga shilingi milioni 200. Shilingi milioni 200 zikipatikana tafsiri yake ni kwamba tunakwenda kuboresha hiyo zahanati, na mwendo ni kuhakikisha kwamba igeuke kutoka zahanati na kuwa kituo cha afya hivyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, tukiahdi tunatekeleza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati ya Sanzantsi imejengwa toka Mwaka 2014 na imekuwa na vikwazo vingi ikiwemo kujenga nyumba ya mganga lakini wananchi wale wamejenga kila kitu kinachohitajika pale, nyumba ya mganga ikatolewa na mfadhili kwa kukaa miaka mitano. Hata hivyo mpaka sasa hospitali ile ya Sanzati haijafunguliwa, Naibu Waziri ameshakwenda pale…

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: …je sasa ni lini hospitali hiyo itafunguliwa baada ya kuwa nguvu za Wananchi zimetumika pale kwa muda mrefu na sasa ina miaka mitano zaidi?

MWENYEKITI: Ahsante. Ni lini hospitali hiyo itafunguliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba pale ambapo nguvu ya Wananchi imetumika haiachwi ikapotea. Naomba uniruhusu nikutane na Mhehsimiwa Getere tujue hasa tatizo ni nini ili tuweze kutatua na hospitali hiyo ifunguliwe ili Wananchi waweze kuendelea kupata huduma.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, bado linaelekezwa kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Na. 87

Hitaji la Wafanyakazi – Kituo cha Afya Kidodi

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya Kidodi katika Wilaya ya Kilosa kitapatiwa wafanyakazi wa kutosha?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Kidodi kina watumishi 36, sawa na asilimia 92 ya mahitaji ya watumishi 39 kwa kuzingatia Mwongozo wa Ikama ya Watumishi wa

Kada ya Afya wa Mwaka 2014. Watumishi muhimu wanaokosekana kituoni hapo ni mteknolojia wa mionzi na mtoa usingizi. Serikali imepeleka masomoni wataalam 200 katika vyuo vya KCMC na Muhimbili kwa ajili ya mafunzo ya huduma ya usingizi. Watumishi hao watapangwa katika vituo vilivyojengwa na kukarabatiwa kikiwemo Kituo cha Afya cha Kidodi ili kuviwezesha kutoa huduma za upasuaji. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI imewasilisha maombi ya kuajiri watumishi wapya wa sekta ya afya, hivyo pindi Serikali itakapoajiri watumishi hao itawasambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya Nchini kikiwemo Kituo cha Afya Kidodi Wilayani Kilosa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyeiti, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; Kituo cha Afya Kidodi kinahudumia wagonjwa wanaotoka zaidi ya vijiji nane. Tatizo lililopo kubwa ni usafiri. Ni lini Serikali itaweza kutupatia Kituo cha Afya Kidodi gari la wagonjwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kituo cha Afya Kidodi kimejengwa katikati ya Mji wa Kidodi kiasi kwamba kuna muingliano mkubwa wa watu ambao hawaleti usalama sasa wanahatarisha usalama wa wagonjwa pamoja na wafanyakazi. Je, ni lini Kituo hiki cha Afya cha Kidodi kitajengewa uzio? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, anaongelea juu ya suala zima la kupatikana kwa gari kwa ajili ya kusaidia wagonjwa. Naomba niendele kumhakikishia Mbunge kwamba Serikali inafanya jitihada kwa ajili ya kusambaza gari za *ambulance* kwasababu uhitaji bado ni mkubwa. Naomba nimhakikishie Mbunge, kwa kadri gari za *ambulance* zitakavyopatikana na wao tutatazama uhitaji tukilinganisha na maeneo mengine ili waweze kupatiwa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lake la pili anaongelea suala zima la uzio ili kusiwe na maingiliano kati ya kituo cha afya na watu ambao wanapita pale; naomba nichukue fursa hii kumugiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa kupitia bajeti yao wahakikishe wanaanza kutenge fedha ili uzio uanze kujengwa ili kutenganisha kati ya kituo cha afya na watu wanaopita kwa miguu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nachuma.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulize swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Mtwara Mikindani ina watu wengi sana, na ni manispaa ambayo haina kituo cha afya, kituo kilichopo ni cha zamanai sana ambacho kinahudumia watu wengi sana; na kulikuwa na mpango wa serikali wa kujenga kituo cha afya pale Kata ya Ufukoni, Mtwara Mjini. Je, Serikali ni lini italeta fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya kwenye Kata ya Ufukoni, Manispaa ya Mtwara Mikindani ili kuweza kuwasaidia Wananchi wa Mtwara kupata huduma za afya? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAMISEMI - MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba

nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge Nachuma la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye mwenyewe amekiri kwamba eneo hilo ambalo ni kata ambayo ameitaja kuna wananchi wengi, na ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapunguza adha kusiwe na mrundikano kwa Wananchi wanapofuata huduma ya afya.

Naomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri yake, na bahati nzuri sasa hivi zao la korosho limeshaanza, ni vizuri katika hizi fedha ambazo tunakwenda kuzipata tuanze kutenga na Serikali kuu tutahakikisha wkamba tunapeleka jitihada zile ambazo wananchi wameanzisha na halmashauri yao na sisi tutapeleka nguvu ili wananchi waweze kujengewa kituo cha afya.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Frank Gorge Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, linaelekezwa kwa Waziri wa Maji.

Na. 88

Kufufua Mradi wa Kutega Maji Katika Kijiji cha Ukwile

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafufua mradi mkubwa wa maji wa kutega maji safi na salama katika Kijiji cha Ukwile mradi ambao ulijengwa na Shirika la Reli *(TAZARA)* uliokuwa ukihudumia wananchi wa Kata ya Mpemba na Katete?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Mpemba ambao chanzo chake kipo katika Kijiji cha Ukwile ulijengwa mwaka 1973 na Shirika la Reli *(TAZARA)* kwa lengo la kuhudumia wananchi wapatao 2,000 katika Kijiji cha Mpemba. Kulingana na ongezeko la watu na chanzo kuharibiwa kutokana na shughuli mbalimbali za kibinadamu na miundombinu kuwa chakavu kumesababisha upatikanaji usiotosheleza mahitaji ya wananchi kwa kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto hiyo, mwaka 2017 Serikali ilichimba visima vitatu na mwaka 2019 kisima kimoja kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya Vijiji vya Mpemba, Chapwa na Katete. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali kupitia Programu ya Usambazaji Maji Endelevu Vijijini na Usafi wa Mazingira imetenga jumla ya shilingi milioni 561 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji kutoka katika visima hivyo kwa ajili ya vijiji vyote vitatu. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 200,000 litakalojengwa eneo la Chapo. Ulazaji wa mabomba yenye ukubwa mbalimbali wa urefu wa kilometa 25 na ujenzi wa vituo 40 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali vile vile imekamilisha uchimbaji wa visima vitano katika maeneo ya Mpemba - Nandanga, Chapwa – Isanzo, Chapwa - Msapania, Ipito na Majengo Mapya na inaendelea na uchimbaji wa visima vingine vine katika maeneo ya Nyerere na Msongwa. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo hayo utatekelezwa katika mwaka fedha ujao wa 2020/2021.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba marekebisho kidogo. Sio Vijiji

vya Mpemba, Chapwa na Katete ni Kata ya Chapwa, Kata ya Mpemba na Kata ya Katete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Ni dhahiri Serikali inajua kabisa kwamba visima vingi vinavyochimbwa na Serikali vimekuwa vikikauka lakini kwenye Mkoa wetu wa Songwe tuna vyanzo vikubwa sana vya maji ambavyo ni Mto Momba pamoja na Mto Bupigu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inatumia mito hiyo kupeleka maji kwenye Mji wetu wa Tunduma ili kuhakikisha kwamba tunapunguza uhaba wa maji kwenye eneo letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ushahidi uliopo ni kwamba Mji wa Tunduma unakua kwa kasi sana, lakini miradi inayotekelezwa sasahivi kwenye Mji wa Tunduma ni miradi midogo ambayo haiwezi kukidhi haja ya wananchi walioko pale na wageni wanaotumia mpaka wa Tunduma. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuleta mradi mkubwa wa maji ambao unaweza ukapunguza kabisa tatizo la maji kwenye Mji wa Tunduma?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge. Tunatambua pamoja na changamoto kubwa sana pale Tunduma lakini tuna mradi wa uboreshaji ambao unakamilika zaidi ya bilioni moja na milioni 300. Katika kuhakikisha tunatatua kabisa tatizo la maji, tumeagiza visima zaidi ya 10 na vitano vimekwishachimbwa. Kwa kuwa tunajua Tunduma ni *centre* ambayo ina uhitaji mkubwa na watu wengi sana, tumeamua sasa kuagiza *RUWASA* wanaendelea na usanifu ambapo tutatoa maji Bupigu kwa ajili ya kuhakikisha tunatatua tatizo la maji kabisa Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee tumepeleka fedha za *P4R* zaidi ya bilioni 1.3 kwa ajili ya

kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji katika Mji wa Tunduma na fedha zimekwishafika. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba niulize swali; Mji wa Igunga kwa sasa kwa muda kama wa wiki tano hivi kumekuwa na matatizo makubwa sana ya maji. Wananchi wanasumbuka kweli, wanapanga foleni kwa sababu bwawa la Bulenya limejaa tope, limekauka kwa hiyo maji hayatoshi. Je, Serikali itatusaidiaje juu ya jambo hili ambalo ni la dharura wakati tunasubiri maji ya Ziwa Victoria kuingia katika Mji wa Igunga? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu ya swali hilo kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua eneo la Tabora, Igunga na Nzega ni maeneo yenye changamoto kubwa sana ya maji. Kwa namna ya kipekee Rais Dkt. John Pombe Magufuli ametupa zaidi ya bilioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa mradi mkubwa sana wa maji na umefikia hatua za mwisho. Nataka kuwahakikishia wananchi wa Nzega tunaenda kutatua tatizo la maji kabisa pale Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee maji hayana mbadala. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge tukutane leo mapema ili tuangalie namna ya kuweza kuwa-*support* wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Vijiji vya Bumila, Iyoma na Mima kuna miradi ya maji ambayo inaendelea na vijiji vina matatizo makubwa sana ya maji na kwa kuwa wakandarasi wanaotekeleza miradi hawajalipwa mpaka sasa na Serikali

inasema imewalipa. Mheshimiwa Waziri, ana maelezo gani ya kuwalipa wale wakandarasi mpaka sasa?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso. Lini mnawalipa wakandarasi?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha na ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Mheshimiwa Mbunge tumeshakutana naye, nataka nimhakikishie kwamba mwezi huu mfuko tumeshapokea, tutaweza kuwalipa wakandarasi ili wananchi wake waweze kupata huduma hii ya maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu walifika Babati kushughulikia matatizo mawili ya maji. Tatizo la Kata ya Sigino kutokuwa na maji kabisa na tatizo la *bill* ya maji kupanda Babati. Naomba nifahamu ni lini wananchi wa Babati watapata majibu ya yale matatizo ambayo waliwakabidhi?

MWENYEKITI: Ahsante. Jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, ni lini utatekeleza ahadi yako.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kama nilivyosema maji hayana mbadala kwa Kata ile ya Sigino kwamba tumeshaunda timu kwa maana ya vikosi kazi vya *RUWASA* katika kila mkoa kwa ajili ya kufanya kazi kwa kupitia *force account,* tunataka tuwahakikishie ile kazi tutaifanya kwa Kata yake ya Sigino. Kuhusu suala zima la kupanda kwa bei, kuna timu maalum ambayo inafanya makubaliano ya bei ili mwisho wa siku tunatambua kabisa ili miradi iweze kwenda lazima wananchi waweze kulipia *bill* za maji, lakini sio za kubambikiziwa. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mbunge wa Mcheweni.

Na. 89

Mkopo wa *USD* 500 Milioni kwa ajili ya Mradi wa Maji

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Serikali ya Tanzania ilipata mkopo wa *USD* milioni 500 wenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maji katika Miji ikiwemo Zanzibar:-

Je, Serikali imeandaa mkakati gani wa kuanza kwa miradi hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Aweso.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Jimbo la Mchewani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji kupitia mkopo wa…

MWENYEKITI: Mheshimiwa, Micheweni.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifanye marekebisho Micheweni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maji kupitia mkopo wa dola za Marekani milioni 500 kutoka Serikali ya India umegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa upande wa Tanzania Bara, Serikali kupitia Wizara ya Maji ilisaini mkataba na Mtaalam

Mshauri *WAPCOS* mwezi Mei 2019. Mkataba huo umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni usanifu wa Miradi wa Maji ya Miji 28 Tanzania Bara ambapo taarifa ya usanifu imekamilika mwezi Agosti, 2019. Sehemu ya pili inahusu kupata mkandarasi wa ujenzi wa miradi katika miji iliyopangwa ambapo unatarajiwa kupatikana mwezi Desemba, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar taratibu zote za usanifu na utekelezaji wa mradi huo zinasimamiwa na Wizara inayohusika na Sekta ya Maji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khatib.

MHE. HAJI KHATIB KAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na maelezo mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa akiyatoa hata wakati tunapokutana kwenye Kamati, lakini hata hivyo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni kawaida kila inapofika mwezi Machi, Kamati za Kisekta zimekuwa zikitembelea miradi ya maendeleo ambayo imekuwa ikipitishwa na Bunge, hata hivyo Miradi ya Maji ya Miji 28 ikiwemo Mji mmoja wa Zanzibar, nataka kujua Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba miradi hii itakuwa ina uwezo, Kamati ya Kilimo na Mifugo na Maji kuitembelea.

Je, kwa Kamati ya Kilimo itakuwa na uwezo wa kutembelea mradi huu wa maji ambao umetajwa katika miradi ya miji 28 katika Mji wa Zanzibar?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa miradi hii imezungumzwa kwa muda mrefu, ni lini hasa miradi hii itatekelezwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo, kwa kifupi tu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali ni moja na maji ni uhai sidhani kama kuna sababu ya Kamati kushindwa kutembelea mradi wa maji, ni busara tu. Kikubwa ambacho nataka kusema huu ni mradi wa muda mrefu sana, lakini tumefanya jitihada kubwa sana sisi kama Wizara na Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza kutekelezwa. Ndiyo maana mpaka sasa usanifu tumekwishamaliza na ripoti tumekwishaituma Serikali ya India tunasubiri kibali kwa ajili ya kumpata mkandarasi na utekelezaji wake uanze mara moja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kakoso.

MHE. SELEMANI M. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mji wa Mpanda Manispaa una tatizo kubwa sana la maji na kuna mradi mkubwa wa maji wa kuyatoa maji Ziwa Tanganyika kuleta Manispaa. Serikali imeahidi kwa muda mrefu, tunataka tujue mradi huu utakamilika lini sambamba na kukamilisha vijiji vile ambavyo vitakuwa kwenye mzunguko ambavyo viko kwenye jimbo langu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, lini mtakamilisha?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimeeleza awali, tupo kwenye taratibu ya kupata mkandarasi katika kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa haraka.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti na linaelekezwa kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 90

Kulitwaa Eneo Lililohodhiwa na Kampuni ya Tanzania Oxygen

MHE. MARWA R. CHACHA aliuliza:-

Kampuni ya Tanzania *Oxygen* kwa muda wa takribani miaka 30 imehodhi eneo lenye maji ya moto lililopo Kata ya Majimoto, Kijiji cha Majimoto katika Wilaya ya Serengeti:-

Je, Serikali ipo tayari kulitwaa eneo hilo na kuwarejeshea wananchi kwa kuwa Kampuni hiyo ilishashindwa kuliendeleza?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Angelina Mabula.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kugawa Viwanja na Mashamba ya Mkoa wa Mara tarehe 23 Agosti, 1996 iliidhinisha, pamoja na maombi mengine, ombi la Shirika la Tanzania *Oxygen Limited (TOL)* kumilikishwa ardhi yenye ukubwa wa ekari 450 kwa ajili ya utafiti wa gesi. Aidha, Shirika hili lililipa fidia kwa wananchi waliokuwepo katika eneo hilo na kugharamia upimaji. Eneo hilo liliandaliwa hatimiliki iliyosajiliwa kwa Na.22705LRM ya muda wa miaka 66 kuanzia tarehe 1 Aprili, 1997. Baada ya kupewa milki hiyo na baada ya kupata vibali vyote vya utafiti wa gesi ya *helium*, Shirika hili halikuweza kufanya shughuli iliyotarajiwa kutokana na wananchi kuvamia eneo hilo na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uvamizi huo, Wizara ilipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba eneo limetekelezwa. Tarehe 31 Mei, 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ilituma ilani ya siku 90 kwa Shirika la *TOL* ikilitaka shirika liwasilishe sababu kwa nini milki yao isibatilishwe. Shirika la *TOL* lilijibu ilani hiyo tarehe 25 Julai, 2016 likielekeza kuwa wapo tayari kurejesha milki hiyo kwa kuwa wameshindwa kutekeleza shughuli iliyokusudiwa na Serikali kutokana na wananchi kuvamia eneo hilo. Halmashauri ya Serengeti iliandaa nyaraka za kurejesha umiliki na kuziwasilisha Shirika la *TOL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilishwa kwa nyaraka hizo, ilibainika urejeshaji hauwezi kukamilika kwa sababu taasisi hiyo ilikuwa inadaiwa kodi ya Sh.1,718,791,959.00 katika milki hizo. Wizara yangu inafanya mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango ili kupata kupata msamaha wa deni kwani taasisi husika imeshindwa kulipa deni hilo. Aidha, baada ya taratibu hizo kukamilika ardhi hiyo itarudishwa kwa wananchi na kupangiwa matumizi mengine.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kuchukua eneo la wananchi miaka karibu 30, umekaa nalo ni jambo ambalo halikubaliki. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika makubaliano yaliyokuwepo kwa wananchi wa Kata ya Majimoto na Kijiji cha Majimoto kwenye hili eneo lenye maji ya moto ilikuwa ni kwamba wahamishwe na waoneshwe eneo la kwenda kuishi, lakini wajengewe shule na zahanati. Mambo haya hayakufanyika.

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, anawaambiaje wananchi wa

Kijiji cha Majimoto ambao walidhulumiwa na hii kampuni bila kujengewa shule wala zahanati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Waziri amesema Wizara yake itawasiliana na Wizara ya Fedha; kwa kuwa Wizara ya Fedha iko hapa, kwa nini isitoe majibu leo ili wananchi wa Kijiji cha Majimoto waweze kuisikia Serikali yao inasema nini kuhusu eneo lao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Angelina Mabula, Naibu Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Ryoba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimthibitishie kwamba wananchi wale hawakudhulumiwa kwa sababu *TOL* walipewa ardhi ile kisheria na hata wale wananchi walipokuja kuvamia, bado walifuata taratibu za kuona ni jinsi gani ataweza kuendeleza, lakini kwa sababu wananchi tayari walikuwa wameshajaa pale akawa yuko tayari ku-*surrender* ile milki yake ili wananchi wapewe. Sasa habari ya kusema kwamba hawakufanyiwa *resettlement* haikuwa katika makubaliano ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba, kwa sababu tayari hawa wameshindwa na kama nilivyosema kwamba bado tunaendelea ndani ya Serikali kuona ni jinsi gani tunaweza tukawaachia wananchi ile eneo, lakini pesa ya Serikali nayo lazima taratibu za kifedha ziweze kufuatwa, kwa sababu bila kufanya hivyo maana yake watu wengi watakuwa wanafanya hivyo halafu anaachia anaacha deni. Kwa hiyo hili lingine tunashughulika nalo kama Serikali na utaratibu ukikamilika wananchi wale watamilikishwa kama ambavyo Serikali imeridhia.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Shally

Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 91

Kufufua Skimu za Umwagiliaji-Kilimanjaro

MHE. SHALLY J. RAYMOND aliuliza:-

Kuna Skimu ndogo na kubwa za umwagiliaji ambazo hazitumiki kama ilivyosanifiwa na kujengwa na nyingine zimekufa katika Wilaya za Moshi, Hai na Same Mkoani Kilimanjaro:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kufufua na kurejesha skimu hizo zifanye kazi kama ilivyokusudiwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, namwona Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekuwa ikishirikiana na wataalam kutoka Halmashauri za Wilaya pamoja na wakulima katika hatua zote za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa lengo la kujenga uelewa wa pamoja kuhusu umuhimu wa miundombinu ya umwagiliaji miongoni mwa wadau. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekuwa ikitoa mafunzo ya nadharia na vitendo katika mashamba darasa kwa wakulima na wataalam kuhusu uendeshaji na matunzo ya skimu za umwagiliaji kwa lengo la kuhakikisha miundombinu iliyojengwa inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekuwa ikitembelea skimu za umwagiliaji na kufanya ukaguzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam ili kuhakikisha skimu husika zinakuwa endelevu.

Aidha, kutokana na ufuatiliaji huo, wataalam wameweza kubaini skimu ambazo hazifanyi kazi na zimewekwa katika mpango wa kutafutiwa fedha ili ziweze kujengwa/kukarabatiwa na hivyo kufanya kazi kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha Tume inafanya kazi na kusimamia skimu kwa ufanisi, kuanzia mwezi Julai, 2019, Muundo wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji umerekebishwa kwa kuwapeleka Wataalam wa Umwagiliaji katika ngazi ya mikoa na halmashauri za wilaya ambazo zina miradi ya umwagiliaji kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wakulima pamoja na kufufua na kurejesha skimu zilizokufa ili kuhakikisha uendeshaji wa skimu na kilimo cha umwagiliaji kwa ujumla kinakuwa endelevu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu nilizokuwa nimeulizia ni kubwa na ndogo ikiwemo ile skimu ya *Lower Moshi Irrigation Scheme* na ile skimu ya Ndungu kule Same lakini zikiweko pia skimu nyingine kama zile za Mwanga, Kiria, Kambi ya Swala, Kituri kule Kilewo na hela zimekuwa zikipelekwa na Serikali huku Mwanga sasa imefikia bilioni 1.8 kwa kipindi kifupi cha miaka mine, lakini skimu zile bado zinasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii iliamua ikachimba visima…

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa nauliza swali kwa sababu hata majibu yapo kwenye *bracket*, hawajui ni *scheme* zipi, naomba kuuliza sasa. Ni lini Serikali itapeleka wataalam kupanua *scheme* hizi ili wananchi wa Moshi waweze kufaidika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili wengi wanaolima katika *scheme* hizo ni wanawake wa Moshi, wanawake wa Mwanga, wanawake wa Same na kwingineko ikiwepo Hai kule Rundugai. Ni lini wananake hawa watapatiwa mafunzo maalum waweze kutumia hayo maji kikamilifu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante majabu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Omary Mgumba.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua ni lini tutapeleka wataalam katika Mkoa wa Kilimanjaro katika kusimamia *scheme* hizi. Kama nilivyojibu kwwenye swali langu la msingi sasa hivi Serikali tumeshapeleke watalam wote katika zile *scheme* katika Wilaya ambazo zina *scheme* za umwagiliaji ambao muundo sasa hivi unaanzia ngazi ya Taifa, ngazi ya anda, ngazi ya Mkoa na ngazi, kila halmashauri kutakuwa mtaalam mmoja wa kusimamia *scheme* za umwagiliaji mwaka mzima ndiyo kituo chake cha kazi kitakuwa huko. Na nichukue nafasi hii kuwaelekeza tena wote Wahandisi wa Umwagiaji nchini waaache kukaa Ofisi waende huku mashambani kwenye *scheme* hizi zinakofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua ni lini wananwake hawa watapelekewa kufanyiwa mafunzo maalum. Mara hawa wataalam watakapofika wkenye vituo vyao vya kazi jukumu lao la kwanza ni kuanza kutoa elimu kwa wote wale ambao wanufaika wa *scheme* hizo pamoja na wakinamama wa Kilimanjaro.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kalanga.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru kwa kunipa nafasi, Naibu Waziri mwaka jana 2018 aliagiza timu ya wataalam kwenda kutembelea na kufanya utafiti *scheme* za umwagiliaji katika Kata ya Engaruka, Selela na Mto wa Mbu na timu ya wataalam mmeshawakabidhi ripoti. Naomba nijue Mheshimiwa Waziri, ni lini atatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha *scheme* za umwagiliaji katika maeneo hayo?

MWENYEKITI: Lini mtatoa fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T.MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kujua kwamba ni lini kwamba tutapeleka fedha. Kama anavyofahamu Serikali inafanya kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu lakini hasa baada ya kupitishwa na Bunge. Kweli ripoti hiyo imeshatufikia tunaendelea kuichakata ili kuja kuleta hapa kwa sababu bajeti ilishapita tutaingiza kwenye mpango wa bajeti wa msimu ujao ili kuijenga walau *scheme* hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kikwembe

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Bunge la bajeti lililopita nilitoa maombi yangu maalum kuhusiana na miradi ya umwagiliaji katika Kata ya Mamba mradi wa Wawakilida pamoja na mradi wa Mwambapuli, na nimekwisha peleka maombi yangu katika Wizara kuhusiana na mradi wa Mwamapuli ili uweze kuingizwa kwenye mradi uweze kuendana na miundombinu iliyo pale ambayo imekuwa ikiharibika na kuweza kuzuia mafuriko ambao mvua sasa hivi zimeanza..

MWENYEKITI: Swali!

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Je ni lini sasa mpango wa mradi wa Mwamapuli wa umwagiliaji utaingizwa kwenye mpango ili tuweze kuzuia mafuriko kwa mvua hizi ambazo zinaendelea?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mgumba ni lini.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T.MGUMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alishasema kwenye Bunge lililopita kuhusu *scheme* hizi na sisi kama Serikali tumeshawaelekeza hawa wataalam wetu wa umwagiaji Tume kwenda kuangalia hali halisi ikoje na kuja na taarifa ya kina ili kutuelekeza nini cha kufanya kwa sababu hatuwezi kuanza kupanga mipango kabla hatujajua hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi tena kuwaelekeza wataalum Wahandisi wa Tume ya umwagiliaji Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenda haraka iwezekanavyo katika Mkoa huu na kwenye *scheme* hizi kufanya tathmini ya kina na kuja na taarifa ili tuingize kwenye mpango wa kuijenga scheme hizo.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Waheshimiwa Wabunge swali linalofuatwa linaulizwa na Mheshimiwa Sauli Amon Mbunge wa Rungwe bado linaelekezwa kwa Waziri wa Kilimo.

Na. 92

Kilimo cha Maparachichi – Rungwe

MHE. FREDY A. MWAKIBETE (K.n.y. MHE. SAUL H. AMON) aliuliza:-

Jimbo la Rungwe ni kati ya maeneo yenye ardhi yenye rutuba na inafaa sana kwa kilimo cha maparachichi:-

(a) Je Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vitalu vya maparachichi ili wananchi wapate miche kwa bei nafuu kwani bei ya sasa ya shilingi elfu tatu kwa mche kwa mkulima wa kawaida ni ghali sana?

(b) Kilimo cha maparachichi kinahitaji utaalamu ili kukidhi kiwango cha kimataifa. Je, Serikali ina mpango gani

wa kusambaza wataalamu wa kilimo katika jimbo la Rungwe?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saul Henry Amon lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo cha parachichi ni muhimu katika kuongeza kipato na lishe kwa wakulima na jamii pamoja na kuliingizia Taifa fedha za kigeni kutokana na mauzo nje ya nchi. Kutokana na umuhimu huo Serikali imekuwa ikihamasisha wakulima na wadau wengine kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi hususan aina ya HASS ambayo imekuwa na soko la uhakika. Serikali pia inatekeleza mkakati wa kuainisha maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha parachichi nchini (*mapping of all potential areas),* kuongeza uzalishaji wa miche ya maparachichi aina ya HASS na kuilinda ili isiharibiwe na aina nyingine za miparachichi kupitia *"cross breeding".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhamasishaji wa Serikali wadau mbalimbali wakiwemo wakulima na makampuni binafsi wameanza kuzalisha miche bora ya parachichi ambapo jumla ya vitalu 233 vikiwemo vitalu 230 vya wakulima wadogo na vitalu vitatu (3) vya Makampuni binafsi vimeanzishwa Wilayani Rungwe. Aidha, vitalu hivyo vinazalisha miche 345000 ambapo miche 265,473 imezalishwa na wakulima wadogo na miche 80,000 imezalishwa na Makampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha upatikanaji wa miche bora ya miparachichi, mkakati wa Serikali ni kukiboresha Kituo cha utafiti cha Uyole pamoja na Kituo cha Utafiti cha Horti-Tengeru ili kuwa vituo mahiri *(Centre*

of Excellence) katika uzalishaji wa miche bora ya miparachichi aina ya *HASS* nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuhamasisha, kuratibu na kusimamia uzalishaji wa miche ya miparachichi kupitia vituo vya utafiti ili kuhakikisha kuwa miche yote inayozalishwa inakuwa na ubora na inauzwa kwa bei nafuu kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imeajiri jumla ya wataalam 70 waliopo katika Kata 29 na Vijiji 116 vya Wilaya ya Rungwe wanaotoa elimu ya kilimo bora cha mazao mbalimbali ikiwemo zao la parachichi. Aidha, Sekta binafsi pia imeajiri wataalam wapatao 23 ambapo wataalam 19 wameajiriwa na kampuni ya Kuza Africa na wataalam wanne (4) wameajiriwa na kampuni ya Rungwe *Avocado Company*. Aidha, Serikali pia inashirikiana na Sekta Binafisi katika kutoa mafunzo ya uzalishaji wa zao la parachichi kwa wakulima.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Atupele Mwakibete.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, Wilaya ya Rungwe pamoja na Busokelo tunalima zao hili la Parachichi na tuna jumla ya Kata 42, lakini kwa maelezo ya Mheshimwia Naibu Waziri anasema wataalam wapo kwenye Kata 29 pekee.

Je, ni lini Serikali itaajiri wataalam wengine kwa Kata zilizobaki 13 ili zao hili la parachichi liweze kuendelezwa vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kwa kuwa wananchi wa Rungwe kwa ujumla wake kwa maana ya Rungwe pamoja na Busokelo sisi sote tunalima zao hili la parachichi, lakini bei yake kwa mche mmoja ni shilingi 3,000 na ninaamini kupitia Serikali ina uwezo wa kutoa *incentives* ama ruzuku badala ya kununu mche mmoja kwa shilingi 3,000 ikanunua hata kwa shilingi pengine 500.

Je, ni lini Serikali sasa itaanza kutoa ruzuku kwa zao hili la parachichi ili wanunue miche angalau kwa shilingi 500, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, majibu kwa maswali hayo mawili kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Bashe.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuajiri wataalam kama sote tunavyofahamu suala la kuongeza wafanyakazi Serikalini linategemea uwezo wa Serikali. Pale ambapo mapato ya Serikali yatakuwa yanaongezeka ndivo hivo hvo katika sekta mbalimbali tutakuwa tunaongeza wataalam. Tunafahamu umuhimu wa kuwaajiri maafisa kilimo ambao wanaweza kwenda kusaidia wakulima wetu. Vilevile kama Wizara ya Kilmo katika mpango wetu mpya ambao tunaupitia sasa hivi wa *horticulture* tunahusisha Sekta Binafsi sasa hivi kwa ajili ya kutoa *extension services*. Kwa hiyo, tu maeneo ya Nyanda za juu Kusini ni maeneo ambayo tunayapa *priority*. Kwa hiyo, hii *consign* ya Mheshimiwa Mbunge tutaiweka katika sehemu ya *priority* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la gharama sasa hivi suala la uzalishaji linafanywa na watu binafsi na Serikali na tumeamua kama Serikali kuipa kituo cha *Horti*-Tengeru na Uyole kama ni *Centre of Excellence.* Kwa hiyo, tutakachokifanya kama Serikali ni kuongeza matiplication katika vituo hivi miche ikiongezeka zaidi maana yake bei ya miche itaendelea kupungua. Kwa hiyo, tutafanya jitihada kwa ajili ya kuangalia *cost structure*, na sasa hivi tumeanza kupitia gharama za *input* katika uzalishaji wa mazao mbalimbali tutaangalia hii *consign* ya wakulima ili tuone tunaweza kufanyaje, hatuwezi kuahidi kutoa *subseed* sisi hatuwezi kutoa hiyo *commitment* kama Serikali kwa sababu mazao mengine vilevile yanachangamoto ya gharama ya *input*, lakini tutaendelea kupunguza gharama za uzalishaji.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mwambalaswa.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali ina nia njema sana ya kuendeleza kilimo ili wananchi waweze kukuza kipato chai na mara nyingi Serikali huwa inatoa pesa ili kuwasaidia wakulima kuendeleza mazao yao. Lakini pamoja na nia nzuri ya Serikali baadhi ya watendaji waSerikali wanakwamisha zoezi hili jema la Serikali mfano uko kwenye zao la korosho...

MWENYEKITI: Swali sasa!

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2018 Serikali imetoa shilingi bilioni kumi ili kununua pembejeo na viuatifu vya zao la korosho la kusikitisha! Hivi ninavyoongea ni mwaka umepita pembejeo hizo na viuatilifu viko bandarini. Serikali inasema nini kuhusu ucheleweshaji wa namna hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukweli usioficha ni kwamba Serikali kweli ilitoa shilingi bilioni kumi kwa ajili ya agiza viuatilifu vya korosho vya salfa. Na ni kweli kwamba viuatilifu hivyo maka sasa hivi viko bandarini, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Serikali imemsimamisha Mtendaji Mkuu wa kampuni ya *TFC* kama hatua ya awali kwa uzembe huu.

(ii) Vilevile Serikali kupitia Wizara ya Kilimo tumemuagiza mfanyabiashara aliyepewa fedha za Umma shuilingi bilioni 4.5 kinyume na maelekezo ya Serikali arudishe fedha hizo Serikalini. Na nitumie nafasi hii kumwambia ndani ya Bunge hili Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Bajuta arudishe bilioni 4.5 kama *limit* tuliyotoa ili fedha hizo ziweze kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tumeshaanza kuchukua hatua kama wizara kwa ajili ya kuzitoa pembejeo

hizo tumeongea na *TPA* wamekubali kutupunguzia kuondoa gharama zote, tumeongea na Kampuni ya Azam kutuondolea gharama za *storage* na sasa hivi tuku katika hatua za mwisho kufanya mchakato wa kuvitoa viuatifu hivi kabla havijaharibika ili tuweze kuwagawia wakulima wa korosho kwenye msimu ujao. Naomba nitumie nafasi hii kuwaambia watendaji wa Wizara ya Kilimo yoyote atakaye *misuse* fedha za Umma katika nafasi yoyote hatutomvumilia.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kabisa kwamba zao la parachichi sasa hivi na hasa aina ya HASS linachangia sana kuingiza fedha za kigeni, na kwa kuwa zao hili sasa hivi linalimwa sana katika Mikoa ya Mbeya, Njombe na maeneo ya Iringa sehemu za Kilolo. Na kwa kuwa kuna baadhi ya wanunuzi siku hizi wameanza kununua kiholela ambao wana *compromise quality* ya *export* yetu.

Je, Serikali inaweka utaratibu gani ku-*control* hao makanjanja wa kununua zao hili na kuuza kwa jina la Tanzania nje ambayo inaharibu soko la parachichi zetu?

MWENYEKITI: Ahsante jibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba sasa hivi zao letu la parachichi limekuwa likisafirishwa kwenda nje aidha kwa kutumia wafanyabiashara wwetu wa ndani ama vilevile madalali wanaonunua kwa niaba ya wafanyabiashara wa nchi zingine kwa ajili ku-*export* kupitia nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatua tulizochukua sababu zinazopelekea wafanyabiashara wengi kutokusafirisha parachichi yetu kupitia aidha bandari ya Dar es Salaam ama *airport* zetu za ndani, tumeshakutana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Miundombinu kwa maana ya

TPA na sasa hivi tuko katika hatua za mwisho kuanzisha kitu kinaitwa *green belt* kupitia Dar es Salaam *port* ili mazao ya kilimo yaweze kupita pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi katika mabadiliko ya Sheria yanayokuja kama Wizara tutakuja na mamlaka ya *horticulture*, *Horticulture Development Authority* ambayo itasimamia mazao yote ya mboga mboga na matunda ili yasiweze kuathirika na wakulima wetu waweze kupata bei nzuri na kutengeneza *export procedure* nzuri ili tuweze kuingia kwenye masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua maabara ambayo itatupa uhalali wa kuingia katika soko la kimataifa kwa sababu mpaka sasa hivi kama nchi tulikuwa hatuna *certified lab* ambayo inaweza kutusaidia kuuza mazao yetu moja kwa moja. Kwa hiyo, baada ya muda Mfupi Waheshimiwa Wabunge tuwaombe kufika Januari, Frebruari tutakuwa tumeshaweka *infracture* hii ili tuweze kuondoa matatizo yanayokabili *sub sector* hii.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Selasini Mbunge wa Rombo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu haya ya mwisho ya Waziri yamenipa faraja sana, huenda hiyo *horticulture Authority* ikatusaidia. Jimboni Rombo kule tunalima sana maparachichi na maparachichi haya yana nunuliwa na wafanyabiashara waranguzi kutoka Kenya na kilimo hiki cha *horticulture* Kaskazini huko wakulima wanapata hasara kubwa sana. Sasa kwa nini pamoja na mkakati wa *horticultute authority* mkakatuti wa kutafuta masoko, tusiangalie uwezekano sasa kama nchi kununua ndege ya mzigo maana yake mazao haya ya *horticulture* yanakwenda Nairobi Jomo Kenyatta *International Airport* yanasafirishwa kwa ndege za Kenya. Kwanini tusiangalie sasa uwezekano wa kununua ndege ya mizigo ambayo itatusaidia kufungua biashara hii ya *horticulture* kwa urahisi zaidi na kusaidia wafanyabiashara wetu nje ya nchi?

MWENYEKITI: Huo ni ushauri Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na zao la *horticulture* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna miaezi mitatu tulishaanza kujadiliana kuhusiana na jinsi ya kupata ndege ya kubeba *horticulture* kutoka kiwanja cha ndege cha Songwe, lakini pamoja na minofu ya samaki kutoka Mwanza.

Kwa hiyo, suala tayari tunalifanyia kazi tutaanza na kukodi *KIA* kwa bahati nzuri pale Kia kuna ndege *KLM* inabeba kila siku, lakini shida ilikuwa ni upande wa Mwanza pamoja na Mbeya. Kwa hiyo, tutaanza kwanza na kukodi ndege kwa sababu tunachangamoto ya mzigo wa kutoka Europe kuleta huku, lakini kutoka hapa kwenda kule mzigo upo. Kwa hiyo, bado tutaanza na kukodi baadaye tunaweza tukanunua. *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yanayotoa matumaini, tunaendelea swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi Mbunge wa Mafinga Mjini linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Na.93

Mikataba ya Kimataifa Ambayo Haijaridhiwa

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

(a) Je, ni mikataba mingapi ya kimataifa ambayo nchi imesaini lakini haijaridhiwa?

(b) Je, kuna athari zozote kwa nchi kutoridhia mikataba ambayo tayari nchi imesaini?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Mammbo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dkt. Ndumbaro.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kuratibu na kusimamia mikataba na makubaliano ya kimataifa. Mikataba na makubaliano hayo yanahusisha ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine yaani *(Bilateral Agreements),* Taasisi za Kikanda na za kimataifa yaani *(Regional and International Treaties and Conventions*) kwa ujumla mikataba hii inatofautiana kwa maudhui na umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mikataba hii inatofautiana kwa maudhui na umuhimu. Lengo na maudhui ya mikataba hii ni kuwezesha au *to compliment* nchi yetu kudumisha na kuimarisha ushirikiano uliopo na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na Kimataifa kwa maslahi ya Taifa letu. Aidha, kupitia mikataba hiyo, Tanzania imeweza kusimamia majukumu mbalimbali ya Kimataifa kwa kushirikiana na nchi nyingine na taasisi mbalimbali na kunufaika na fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inatumia utaratibu wa kisheria wa kutobanwa moja kwa moja na mikataba ya Kimataifa mara tu inaposainiwa *(dualism).* Utaratibu huu unatoa nafasi kwa nchi yetu kuanza mchakato wa ndani ambao ni shirikishi kwa sekta husika kuandaa waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mkataba huo kwa ajili ya kuridhiwa ndani ya Serikali kabla ya kuidhinishwa na Bunge. Hivyo, hakuna athari zozote kwa nchi yetu kutoridhia mikataba

ambayo tayari tumesaini kwa kuwa nchi yetu inafungwa na mikataba ya Kimataifa baada ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesaini na kuridhia mikataba ya Kimataifa 39. Aidha, Serikali ina jumla ya mikataba ya Kimataifa 42 ambayo imesaini lakini haijaridhiwa na Bunge kwa sababu inaendelea kufanyiwa tathmini ya kina ili kubaini athari zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kabla ya maswali yangu mawili ya nyongeza, naomba kwa ridhaa yako nitumie nafasi hii, maana najua sitapata nafasi, kuitakia Timu ya Taifa ya Tanzania maandalizi mema na ushindi katika mchezo wake wa kesho wa Kimataifa dhidi ya *Equatorial Guinea. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa mujibu wa majibu ya Serikali ni kwamba tuna mikataba takribani 42 ambayo kama Taifa tumeisaini lakini bado haijaridhiwa na hapa tulipo Bunge la Kumi na Moja tunaelekea mwishoni mwakani mwezi Juni. Je, Serikali iko tayari kuleta walau mikataba kumi katika Bunge la Januari ili tuweze kuridhia mikataba hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mimi natoka Mafinga na watu wengi wa mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma na Mbeya tunalima sana na kupanda miti; na tuliambiwa kwamba ikiwa Serikali itaridhia baadhi ya mikataba ya kimazingira, tutapata ile wanaita *carbon credit* kutokana na mchango wetu katika dunia wa *carbon emission*. Je, Serikali iko tayari kuchambua mikataba ya aina hiyo ambayo sisi watu tunaotoka kunakopandwa miti, tunaweza kunufaika kwa kulipwa kutokana na *carbon credit?*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali haya mawili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa ufupi tu, yako *very straight.*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Chumi kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Nikianza na lile swali la kwanza ni kwamba katika Bunge hili linaloendelea, tuna mikataba takribani mitatu ambayo imeletwa kwa ajili ya kuridhia. Hiyo ni nia nzuri ya Serikali kuendelea kuridhia mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze kwamba, siyo yote inaweza kuridhiwa, kwa sababu mikataba mingine inakinzana na mila na desturi zetu, inakinzana na imani za dini, inakinzana na sheria ambazo tumezitunga, Katiba pamoja na mambo mengine ambayo hayawezi kuelezewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na *carbon credit,* moja kati ya mkataba ambao utaridhiwa katika Bunge hili ni unaohusiana na suala zima la mazingira. Kwa hiyo, suala hilo la *carbon credit* linafanyiwa kazi na Bunge hili kabla halijaisha ndani ya wiki hii mkataba huo utakuwa umeridhiwa. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkuya.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza. Hakuna utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba mikataba hii ya Kimataifa ambayo tunairidhia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapelekwa Zanzibar kwa ajili tu ya kupata uelewa juu ya hii mikataba:-

Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa mikataba inayoridhiwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa vilevile inapelekwa Zanzibar kwa ajili ya

kupata uelewa na kujua kwamba nchi yao imeridhia mikataba hii?

MWENYEKITI: Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya mikataba hii haijafika katika Baraza la Mawaziri ni lazima ipelekwe katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili iweze kupata ridhaa na ridhaa hiyo huwa inakuja kimaandishi. Sasa inawezekana utaratibu wa kushirikishana kule Zanzibar ukawa tofauti, lakini ni lazima inakwenda na yote imekwenda na ndipo tumeweza kufika hapa.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na swali linalofata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini na linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasialiano.

Na. 94

Barabara ya Kiboriloni, Kikarara, Kidia Mpaka Tsuduni

MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. ANTONY C. KOMU) aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Kiboriloni, Kikarara, Kidia mpaka Tsuduni yenye urefu wa kilometa 10.8 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kiboriloni – Kikarara – Kidia mpaka Tsuduni yenye urefu wa kilometa 10.8 ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini *(TARURA)* Mkoa wa Kilimanjaro. Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilipewa jukumu la kusimamia usanifu na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kabla ya *TARURA* kuanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilianza ujenzi wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya shilingi bilioni moja zilitengwa na kutumika kujenga kilometa 1.0 kuanzia eneo la Kiboriloni, kwenye makutano ya barabara kuu ya Segera – Himo – Moshi kuelekea Tsuduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi milioni 770 zimetengwa ili kuendeleza utekelezaji wa ujenzi wa kilometa 0.77 kwa kiwango cha lami katika barabara hii na kwa sasa mradi huu upo katika hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa mwenyekiti, nashukuru kwa majibu. Ukiangalia au ukiyasoma majibu haya, inaonesha wazi kwamba kwa fedha wanazozitenga, barabara hii ya kilometa 10 itachukua takribani miaka 10 ili kukamilika, hasa ikizingatiwa kwa mwaka huu peke yake ni shilingi milioni 770 tu. Je, Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba inaharakisha ujenzi huo hasa ikizingatiwa kwamba Makao Makuu sasa ya Halmashauri ya Moshi Vijijini imehamia pale Kolila na ambapo barabara hii inapita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa muktadha huo pale Dar es Salaam ninakotoka mimi kuna barabara ya kutoka Chuo Kikuu kuelekea Changanyikeni katika Jimbo la Kawe, barabara hiyo ni mbovu kweli kweli. Najua iko chini ya

TARURA lakini Serikali ni moja na nimeshaenda *TARURA* na mpaka leo tunapta shida sana na Mheshimiwa Ndalichako anajua tatizo hili kwa sababu tunatoka katika eneo moja:-

Je, ni lini Serikali itafanya utaratibu wa kujenga barabara hizo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake la msingi amesema kwamba tulianza kuhudumia Wizara ya Ujenzi, *TANROAD* ilianza kuhudumia hizi barabara kabla ya *TARURA* kuwepo. Sasa *TARURA* ipo, jibu ni moja tu, barabara zote mbili alizozizungumza, naomba awasiliane na watu wa *TARURA.* Huo ndiyo utaratibu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bilakwate Innocent.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mgakorongo kwenda mpaka Mlongo na barabara ya Mrushaka kwenda mpaka Mrongo, hizi barabara ni ahadi ya muda mrefu ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Awamu ya Tano:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi ni lini zitajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, lini?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumekamilisha usanifu wa awali na usanifu wa kina. Namwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba na wananchi wa eneo hilo ambalo linamgusa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, ni kwamba

Serikali inamalizia mazungumzo ya kupata fedha kutoka *East Africa* kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, wananchi watulie, baada ya kukamilisha malengo yapo, lazima tujenge barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara ya Kimanga sasa inajengwa ni miaka minne, lakini hata hivyo pia kuna barabara ambayo ni ya Segerea ambayo imekwanguliwa juzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu. Ni lini barabara hizo muhimu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Bonnah kwa sababu barabara hizi tumezizungumza sana amekuja ofisini mara nyingi. Niseme tu kwamba pale Segerea pamekwanguliwa, walichelewa kupaziba kwa sababu ya mvua hizi zilikuwa zinanyesha kwenye siku hizi mbili, tatu. Tulitegemea kama jana na leo hapatokuwa na mvua, kesho lami itawekwa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara ya Kimanga, utaratibu wa ujenzi unaendelea. Kwa hiyo, nikutoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge, utaratibu uko vizuri, ujenzi unaendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amar Hussein.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa tumekuwa na maombi ya mara kwa mara kuhusu kujengewa kilomita mbili za lami Makao Makuu pale Karumwa, napenda kuuliza ni lini lami hiyo ya kilomita

mbili itajenga pale Makao Makuu ya Karumwa ili kupunguza vumbi ambalo linaweza kuwasababishia maradhi wananchi wangu?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu nami nimetembelea Geita. Ujenzi wa kilomita mbili za lami kwenye Mji wa Karumwa upo kwenye Mpango na anafahamu. Kwa hiyo, nakupongeza tu kwa juhudi zako, lakini tutajenga barabara hizi pamoja na mitaro kwenye eneo hili ili kutoa usumbufu ambao upo katika mji huu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Rais alipofanya ziara mkoani Mbeya aliahidi kujenga barabara ya lami ya Mbalizi, Shigamba mpaka Isongole. Sasa ni lini barabara hiyo ya kilomita 52 mpaka Shigamba itajengwa kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais aliagiza, lakini ujenzi tumeshaanza. Sasa hivi tayari tunajenga kutoka Pemba kwenda Isongole. Tukishamaliza, basi tutaendelea na eneo lingine ili kuikamilisha hiyo barabara.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa majibu yanayotoa matumaini. Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla. Barabara ya

Nachingwea Liwale Mkandarasi yupo barabarani anafanya usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Mtwara bado haujaunganishwa japo hata kwa barabara ya changarawe. Wananchi wa Mkoa wa Lindi na Morogoro...

MWENYEKITI: Uliza swali.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: ...wanatamani kusikia Serikali yao inasema mikoa hii miwili itaunganishwa lini kwa barabara angalau ya changalawe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mkoa wa Lindi na Mtwara kuhusu kuunganishwa kwa barabara.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kuchauka kwa sababu amekuwa akifuatilia kwa umakini sana barabara zake na matokeo yake ndiyo kama hayo, tunaendelea na usanifu wa kilomita 129 kutoka Nachingwea kwenda Liwale. Pia Bunge lako limetenga fedha kwa ajili ya usanifu kilometa 230 kutoka Nangurukuru Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu pia ana hamu ya kuunganishwa na Morogoro. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira, tunakwenda hatua kwa hatua, wakati utafika, tutaitazama kwa macho mawili barabara hii kutuunganisha kwenye Mkoa wa Morogoro.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo. Kwa vile Serikali imeshafanya uwekezaji mkubwa kujenga daraja la Sibiti na kwa vile barabara hiyo inahudumiwa na *TANROADS* na Nduguti sasa ni Makao Makuu ya Wilaya.

Ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo kidogo japo kilometa 40 kutoka Iguguno mpaka Nduguti Makao Makuu ya Wilaya? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri unafahamu sana kwa nini nataka uweke msisitizo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Kiula anafahamu maeneo haya yalikuwa korofi muda mrefu na kufanikiwa kujenga daraja la Sibiti ni mwendelezo mzuri sasa wa kuja kuunganisha Iguguno, Sibiti kwenda kwenye mikoa ya Simiyu, Mwanza. Kwa hiyo, avute subira, lakini maeneo yote korofi tumeendelea kuyafanyia matengenezo makubwa. Tumeendelea kujenga madaraja, Mheshimiwa Kiula anafahamu hata kule Msingi kuna daraja kubwa linatengenezwa na maeneo yote korofi tumeyaimarisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wananchi wavute subira tu, tutakuja kuitizama barabara hii tuinunganishe na Sibiti ili sasa maeneo yote yaweze kupata huduma nzuri ya barabara.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na swali linalofuatwa, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo. Bado linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. *(Makofi)*

Na. 95

Ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA aliuliza:-

Ujenzi wa Barabara ya Makofia – Mlandizi kwa kiwango cha lami uko katika Ilani za uchaguzi za CCM za miaka 2005, 2010 na 2015.

Je, ni lini Barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Makofia - Mlandizi ni barabara ya mkoa yenye urefu wa kilometa 35.4 ambayo inaunganisha Wilaya ya Bagamoyo na Kibaha. Barabara hii ni sehemu ya barabara ya Makofia – Mlandizi – Maneromango ambayo ina jumla ya urefu wa kilometa 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua mbalimbali za maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimefanyika ikiwemo kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina pamoja na uhakiki wa mali zilizoko kwenye eneo la barabara zitakazoathiriwa na mradi huu. Barabara hii itakuwa ya njia nne *(dual carriage way)* kutoka Makofia hadi Mlandizi. Ujenzi wa barabara hii utaanza mara tu fedha kwa ajili ya fidia na ujenzi kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Pwani inafanya matengenezo mbalimbali kila mwaka ili kuifanya barabara hii ipitike majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi 433,332,980/= zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hii. Mkataba wa matengenezo hayo tayari umesainiwa na Mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi ya matengenezo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kawambwa.

MHE. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuulizwa maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii sasa hivi haipitiki kabisa, ni adhabu kubwa sana kupita katika barabara hiyo katika Vitongoji vya Sanzale, Kijiji cha Machimbwa, Kijiji cha Yombo na Kijiji cha Simba. Upitaji wa barabara kipindi hiki ni ngumu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali inatenga fedha kwa ajili ya matengenezo kabla ya ujenzi kwa kiwango cha lami, kwa nini fedha hizi zinachelewa sana kutolewa na matengenezo hayafanywi kwa kipindi kirefu kiasi kwamba inawapa wananchi adhabu kubwa ya kuipita hii barabara na masika yatakapokuja itakuwa ndiyo haipitiki kabisa barabara hii:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jibu, kwa nini matengenezo hayafanywi kwa wakati ili wananchi waweze kuitumia barabara hii vizur? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa sababu sasa hivi ni takribani karibu miaka 14 tangu 2005 barabara hii ilipoingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ujenzi kwa kiwango cha lami na wananchi ambao maeneo yao yataathirika yamezuiwa kufanyiwa maendelezo yoyote. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anipe jibu kwa kuzingatia muda huo mrefu, ni lini sasa fidia ya wananchi katika barabara hii itatolewa? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa maswali hayo mawili.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Dkt. Kawambwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa barabara ile na mimi naipita kila miezi mitatu. Uharibifu uliojitokeza sasa hivi ni kutokana na mvua kubwa zinazonyesha katika Jiji la Dar-es-Salaam. Hata hivyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumepokea hoja yake na tutaifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tunarudisha ile hali nzuri ya barabara ile ambayo kwa kweli huwa unatengenezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu hoja ya wananchi ambao wamepisha ujenzi, tumeendelea kulipa fidia kidogokidogo na wakati tukijiandaa kwa sababu usanifu wa awali na wa kina ulishakamilika, malengo ni kuijenga barabara hiyo ili kuwa njia nne. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge fedha zikipatikana, barabara hiyo lazima itajengwa kwa sababu hiyo ndiyo nia na ni ahadi ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mulugo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mbalizi - Mkwajuni yenye kilometa 91 lakini jambo hilo halikufanyika. Awamu hii Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli alipokuwa kwenye kampeni pale Mkwajuni alituahidi lami kilometa 91 kutoka Mbalizi - Mkwajuni. Mimi mwenyewe nimekuwa nikifanya juhudi binafsi kumuona Waziri kila mara tukikutana lakini bado sijapata majibu kamili. Naomba leo Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini ujenzi wa barabara hii utafanyika kutoka Mbalizi - Mkwajuni? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni lini kazi ya ujenzi itaanza ya barabara ya Mbalizi – Mkwajuni?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mbalizi - Mkwajuni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa awali na usanifu wa kina umekamilika. Ile ni barabara ya mkoa, kwa hiyo, niwafahamishe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa maeneo ya Mkwajuni mpaka kule Ibungu kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami. Tunaendelea na kutafuta fedha, zikishapatikana ujenzi utafanyika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Karatu – Mbulu – Sibiti katika bajeti iliyopita tumepata kilometa 50. Je, ni lini sasa barabara ile inaanza kujengwa?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer* Isack Kamwelwe.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeweka kilometa 50 katika bajeti hii tunayoendelea nayo ili tuweze kujenga hiyo barabara katika kipande alichokitaja. Maandalizi yanaendelea vizuri, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge mwaka haujaisha lazima chochote kitokee katika barabara hiyo. Naomba niwahakikishie wananchi kwamba tumelenga kujenga barabara hii ili kuweza kuunganisha Haydom pamoja na maeneo mengine kwa sababu pale Haydom kuna hospitali kubwa ambayo inafanana na hospitali ya mkoa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Serikali imekuwa ikitoa majibu mazuri sana kuhusu barabara ya Sepuka – Ndago - Kizaga lakini utekelezaji wake hauko kama majibu yanavyotoka. Naomba leo Serikali iwahakikishie wananchi wa maeneo hayo barabara hiyo itajengwa lini kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Ahsante. Nani anaweza kutoa *assurance* hiyo? Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge muda mrefu sana amekuwa akifuatilia barabara hii. Barabara hii ilitengewa fedha za usanifu na kazi hiyo inaendelea kukamilishwa. Baada ya usanifu kukamilishwa, niwahakikishie wananchi wa maeneo haya kuanzia eneo la Magereza – Ndago - Kizaga nina uhakika kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, bado tupo Wizara hiyohiyo, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga.

Na. 96

Barabara Inayotoka Samuye – Puge

MHE. SEIF K.S. GULAMALI aliuliza:-

Ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Samuye –Choma – Zia – Nkinga –Simbo hadi Puge inayokadiriwa kuwa na urefu wa km. 100:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Samuye – Choma – Ziba – Nkinga – Nsimbo - Puge inahusisha barabara mbili za Puge – Ziba yenye urefu wa kilometa 83.06 na Ziba – Choma yenye urefu wa kilometa 26.6. Barabara hizi ni za mkoa na zinasimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu Swali Na.234 katika Bunge lako Tukufu la tarehe 15 Mei, 2019, barabara hizi zitakuwa miongoni mwa barabara zitakazopewa kipaumbele katika kutengewa fedha kwa ajili ya kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kazi hiyo ikisubiriwa, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*, itaendelea kuzifanyia matengenezo mbalimbali barabara hizi ili ziendelee kupitika vizuri majira yote ya mwaka. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, barabara hizi zimetengewa jumla ya shilingi milioni 934.885 kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo muhimu maeneo ya barabara nilizozitaja

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gulamali.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupatia fedha za ukarabati wa barabara hii kila mwaka. Pia napenda kutumia nafasi hii kueleza kuwa fedha tunazopewa karibu shilingi milioni 934 ambazo zinatumika kwa ajili ya kukarabati barabara hii hutumika na kazi huwa inafanyika lakini mara tu baada ya kazi hizo kumalizika...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. SEIF K.S. GULAMALI: Barabara hiyo huanza kuharibika na changamoto ya uharibifu wa barabara inaanza kurudia palepale. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa barabara hiyo ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Gulamali, Mbunge wa Manonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nipokee pongezi alizozitoa nami pia nampongeza kwa sababu amekuwa machachari sana kufuatilia barabara zake. Ni kweli kufanya matengenezo barabara katika maeneo korofi na maalum, kutengeneza madaraja na ukarabati mbalimbali ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Gulamali kwamba barabara ikitengenezwa lazima tuendelee kuifanyia marekebisho mbalimbali na tutaendelea kufanya hivyo ili kuhakikisha kwamba barabara zinapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi nikuhakikishie kwamba tutakapofanya usanifu wa barabara hizi muhimu tutakwenda kwenye ujenzi. Nafahamu kwamba yako maeneo kwa mfano kwenye Hospitali ya Nkinga kuna wagonjwa wengi sana ndiyo maana utaona mara kwa mara tunafanya

marekebisho makubwa ili wagonjwa wanaokwenda kupata huduma hiyo wasipate shida. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge tumejipanga vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Makilagi.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga barabara kilometa tano ya Musoma – Usekela yenye urefu wa kilometa 80, napenda kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipokuja ziara Mkoa wa Mara mwaka jana alimuagiza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kamwelwe atangaze barabara kilometa 40. Napenda kujua sasa Mheshimiwa Kamwelwe lini anatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, *Engineer* Isack Kamwelwe.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la mama yangu Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa Rais aliagiza kwamba tutangaze kilometa 40. Wakati ameagiza tulikuwa tumeshafanya usanifu wa kina kilometa 5 zile nyingine zilikuwa bado. Kwa hiyo, tunaendelea kukamilisha maandalizi lakini tukasema tuanze kujenga kwanza hizi 5. Kwa hiyo, maagizo ya Mheshimiwa Rais mama yangu yameshaanza kutekelezwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Chiza.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kutenga fedha za kujenga barabara ya kutoka Kabingo – Kibondo – Kasulu - Manyovu na kuunganisha Mkoa wa Kigoma na Burundi. Barabara ambayo inakwenda kuufungua Mkoa wa Kigoma Kitaifa na Kimataifa. Lakini barabara hii ili ikamilike…

MWENYEKITI: Uliza swali sasa.

MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nimuulize Mheshimiwa Waziri, kipande cha kutoka Nyakanazi - Kabingo kilometa 50, tangu 2014 kipande hiki bado kinajengwa na sasa kimefikia takribani asilimia 60. Namwomba Mheshimiwa Waziri aseme neno tu watu wa Mkoa wa Kigoma wapone kuhusu hiki kipande cha Nyakanazi - Kabingo.

MWENYEKITI: Ahsante. Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa, kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimia Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu na Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba kwa hatua ambazo Serikali tumezichukua kuangalia menejimenti ya ujenzi wa barabara ilivyo kwa hali ya sasa kuna mabadiliko makubwa. Changamoto ambazo zilikuwepo kwa mkandarasi tulizishughulikia na naamini atakubaliana na mimi kwamba sasa kasi iko kubwa kwa sababu nilipotembelea kwenye mradi huu kilometa 29 zilikuwa zimeshakamilika kati ya kilometa 50 na hizi 21 zilizobakia zilikuwa ziko kwenye hatua ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kakonko kwamba muda siyo mrefu tutakwenda kukamilisha barabara hii kwa maana sehemu zile korofi pamoja na kwenye daraja lile kubwa na nilitembelea nikaona kwamba sasa hatua ilikuwa inakwenda vizuri. Kwa hiyo, nimtoe hofu muda siyo mrefu tutapita kilometa 50 hizi kwenda Kakonko vizuri kabisa.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje, linaelekezwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Na. 97

Athari Zitokanazo na Michezo ya Kubahatisha

MHE. JANET Z. MBENE aliuliza:-

Michezo ya kubahatisha inaingiza pato kwa Taifa lakini ina athari kubwa za kimaadili na kisaikolojia kama ilivyo kwenye dawa za kulevya ikiwa haitaangaliwa kwa umakini:-

(a) Je, Serikali imechukua tahadhari zipi kuhakikisha kuwa michezo hii inashirikisha watu wenye ufahamu wa athari za kutegemea michezo hii hali inayoweza kuwaletea athari kubwa za kiuchumi, kijamii, hadi ndani ya familia na Taifa kwa ujumla?

(b) Je, Serikali inaweza kuwatambua na kuwafuatilia wachezeshaji wote wa michezo hii ya kubahatisha?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Majibu kwa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa michezo ya kubahatisha bila uratibu na usimamizi thabiti unaweza kuwa na athari hasi kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Ili kukabiliana na athari hasi zinazoambatana na michezo ya kubahatisha, Serikali imechukua hatua zifuatazo; kujenga Mfumo wa TEHAMA utakaotumika katika kusimamia mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha pamoja na kuratibu mienendo ya wachezaji kwa nia ya kukabiliana na uraibu wa michezo hiyo: Kutoa elimu kwa umma kuhusu athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha; kudhibiti uagizaji na uendeshaji holela wa michezo ya kubahatisha hususan michezo ya *slot machine* na michezo ya mitandaoni na kuboresha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kwa lengo la kukabiliana na athari za michezo hiyo. Hatua zinazochukuliwa na Serikali zinalenga kupunguza ushawishi wa kushiriki michezo ya kubahatisha kupita kiasi na hivyo kupunguza athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha kwa jamii.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna changamoto ya kusimamia wachezaji wa michezo ya kubahatisha, hususan wachezaji wa michezo isiyohusisha mfumo wa TEHAMA. Hata hivyo, Serikali ipo mbioni kuunganisha michezo yote kwenye mfumo wa TEHAMA unaoendelea kujengwa. Mfumo utaiwezesha Serikali kuratibu mienendo ya kila mchezaji na kuchukua hatua dhidi ya wale wanaokiuka sheria na kanuni za michezo ya kubahatisha. Mfumo huo utatumika pia kudhibiti uchezaji uliokithiri kwa kuweka viwango vya fedha za kucheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa michezo inayoendeshwa kwa mfumo wa kompyuta, usimamizi wa wachezaji unafanyika kwa kuwa taarifa za mchezaji huchukuliwa kikamilifu na hivyo Serikali inaweza kuwatambua na kuwasimamia kupitia taarifa zao. Pale inapobainika kuwa mchezaji ameathirika kutokana na kujihusisha kwenye michezo ya kubahatisha (kucheza kupita kiasi), hufungiwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha kwa kushirikiana na

waendeshaji. Pia, Serikali inaandaa utaratibu wa kuanza kutoa tiba kwa wachezaji ambao wamepata uraibu kutokana na kujihusisha kupita kiasi kwenye michezo ya kubahatisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu yanayotia moyo lakini kwa kweli, ni dhahiri kuwa kudhibiti michezo hii sio rahisi kiasi hicho. Napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kuhusiana na masuala ya mafunzo. Je, Serikali inaweza kutueleza hayo mafunzo mpaka sasa hivi yameshafanyika wapi, kwa utaratibu upi na kwa watu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuhusiana na wale ambao wanachezesha michezo hii nje ya mfumo wa kielektroniki au nje ya mitandao. Je, ni lini sasa hiyo mikakati mbadala au ya *interim* itakayotumika kuhakikisha kuwa kwa kipindi hiki ambacho tunangojea na wao waingizwe katika mifumo tunadhibiti zile athari ambazo nimezitaja katika swali langu la msingi?

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu kwa maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ufupi tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa lleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika ni wa semina mbalimbali kwenye maeneo yenye makundi mengi ya vijana ambapo *Gaming Board of Tanzania* huwa wanakwenda na kukaa na vijana hawa na kuwapa mafunzo haya. Pia katika kila eneo inakoendeshwa michezo hii ya kubahatisha Serikali tumekuwa tukisambaza vifurushi na

majarida mbalimbali kama haya niliyoshika mkononi yanayowajulisha vijana athari ya kucheza michezo hii kupita kiasi. Majarida haya yameandikwa mambo mengi ya kuwapa elimu vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi Bodi yetu ya Michezo ya Kubahatisha ipo kwenye kampeni ambayo tumeipa jina la Makinika Kijana ambapo tunamtaka kijana wa Kitanzania aelewe michezo ya kubahatisha siyo mbadala wa ajira wala chanzo cha mapato bali ni sehemu tu ya burudani. Kama tunavyofahamu, burudani huwa inachukua sehemu ndogo sana ya muda wa mwanadamu zaidi waweke nguvu zao nyingi katika kazi muhimu za kujenga uchumi wa mtu mmojammoja na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kwanza nilishukuru sana Bunge lako Tukufu ni mwaka huu tumeweza kufanya mabadiliko ya Sheria hii ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003 ambapo sasa ni lazima kwa kila anayeendesha mchezo huu wa kubahatisha aweze kuingizwa katika mfumo wa TEHAMA. Tunakamilisha mfumo huu wa TEHAMA, wote tutawaunganisha na tutaweza kuwa-*monitor* wachezaji wanaocheza michezo hii ya kubahatisha na kujua ni yupi anapita kiasi ili aweze kufungiwa kushiriki kwenye mchezo huo.

MWENYEKITI: Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 98

Wingi wa Tozo na Kodi kwa Wafanyabiashara Nchini

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko toka kwa wafanyabiashara kwamba tozo na kodi zimezidi na kusababisha kukosa faida au kusababisha mfumuko wa bei pamoja na upungufu wa wateja:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kero hizo ili kukuza biashara?

MWEYEKITI: Ahsante. Bado tuko Wizara ya Fedha na Mipango, majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Fddha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali kupitia Bunge lako tukufu imekuwa na utaratibu wa kufanya mapitio ya sheria za kodi pamoja na sheria nyinginezo zinazosimamia tozo na ada mbalimbali kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako tukufu lilipitisha kwa kauli moja maboresho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 mwezi Juni 2019 ili kutoa msamaha wa kutengeneza hesabu ambazo zinatakiwa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa ajili ya ukokotoaji wa kodi ya mapato, kutoka kiwango cha awali cha shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 100. Lengo la maboresho haya ni kupunguza gharama kwa mlipa kodi ya kutafuta mtaalamu mwenye *Certified Public Accountant,* kwa ajili ya kutengeneza hesabu zake.

Aidha, hatua hii pia ililenga kuchochea ulipaji kodi wa hiari na kuongeza mapato ya Serikali. Pia Bunge lako Tukufu liliridhia mapendekezo ya kupunguza kiwango cha chini cha kodi, kutoka shilingi 150,000 kwa mwaka hadi shilingi 100,000. Vilevile Bunge lako tukufu liliridhia msamaha wa kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne kwa wajasiriamali wadogo. Maboresho haya yalilenga kupunguza mzigo wa kodi kwa walipa kodi wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge lako la Bajeti la mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara *(Blue Print*), imefuta na kurekebisha jumla ya ada na tozo 54 zilizokuwa zinatozwa na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali zinazojitegemea. Lengo la kufuta ada na tozo hizo ni, kuondoa kero na urasimu, kuwapunguzia mzigo wa kodi wafanyabiashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Aidha, Serikali itaendelea kufuta na kupunguza baadhi ya kodi, ada na tozo mbalimbali ambazo ni kikwazo katika shughuli za kiuchumi na kijamii, kama ilivyoainishwa kwenye mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Najma Giga.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa naishukuru na kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambayo inachukua, kwa kushirikiana na Bunge letu, kurekebisha sheria mbalimbali za kodi ili kuweka uwezeshaji rahisi katika biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mazuri sana yanayofanywa na Serikali, na ambayo yanaendelea kufanywa, bado kuna changamoto kubwa katika bidhaa za chakula, ambazo najua hazina kodi. Vilevile bado kuna changamoto ya mfumuko wa bei katika bidhaa muhimu za chakula, kama vile unga wa mahindi na maharage kwa wananchi wetu wa Tanzania, ambao wanatumia na ambao ni wengi sana, hasa wenye kipato cha chini. Je, Serikali ina mpango gani kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, kuhakikisha kwamba bidhaa muhimu za chakula ambazo zinatumika na Watanzania walio wengi, hasa wa kipato cha chini, zinapungua bei ili kuwarahisishia maisha yao?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango; kwa ufupi tu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la pacha wangu Mheshimiwa Najma Murtaza Giga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa, mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba 2019, umeongezeka hadi 3.6% kutoka 3.4% kwa mwaka ulioishia mwezi Septemba 2019, na katika bidhaa zilizochangia ongezeko hili la 0.2% ni bidhaa za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama taifa tunafahamu kuwa taifa letu halina upungufu wa chakula, tuna chakula cha kutosha. Hata hivyo yapo maeneo ndani ya taifa letu ambayo hayakupata chakula cha kutosha; hivyo yamesababisha, kulingana na *competition* iliyopo, kuongeza bei ya bidhaa hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Kama taifa tunalitambua hili na tayari *NFRA* wameshatoa angalizo; kuweza kutoa chakula hiki kwa wafanyabiashara, wanunue kwa bei nafuu, ili kwenda kupeleka maeneo ambayo yana upungufu wa chakula; na hatimaye kupunguza bei ya vyakula; na taifa letu kuendelea kuweka historia ya kuwa na mfumuko wa bei ambao ni mdogo; hivyo Watanzania wetu kuendelea kupata chakula na bidhaa nyingine katika bei ambazo ni rahisi na wanazozimudu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando Mbunge wa Kibiti.

Na. 99

TANESCO Kushindwa Kupeleka Nguzo za Umeme na Mita Kibiti

MHE. ALLY S. UNGANDO aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Kibiti maeneo yaliyofikiwa na umeme baadhi yao wamekuwa na adha kubwa na *TANESCO* kwa kuwa wamelipa nguzo na mita kwa pesa zao lakini *TANESCO* wameshindwa kutimiza wajibu wao.

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha *TANESCO* kushindwa kutimiza wajibu wao?;

(b) Je, ni lini Wananchi hao watapelekewa huduma ikiwa tayari wameshalipia?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea kuhakikisha kuwa nguzo na vifaa kwa ajili ya kuwaunganishia umeme wananchi vinapatikana kwa wakati. Vifaa muhimu vikiwamo nguzo, mita, nyaya na vifaa vingine kwa ajili ya kuunganishia huduma ya umeme wateja kwa sasa vinanunuliwa kupitia wazalishaji wa ndani ya nchi. Hatua hiyo imeifanya *TANESCO* kuongeza kasi ya kuwaunganishia umeme wateja. Awali *TANESCO* ilikuwa inategemea kupata nguzo kutoka kwa mzabuni mmoja tu, ambaye hakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya nguzo kwa wakati. Hivi sasa kuna viwanda tisa (9) vya nguzo hapa nchini. Kwa upande wa mita jumla ya viwanda vitatu (3) vipya vimeanzishwam vyenye uwezo wa kuzalisha mita 2,000,000 ilhali mahitaji ya mita kwa miradi ya *TANESCO* na *REA* ni mita 1,090,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kuongeza uwezo wa upatikanaji wa vifaa vya kuunganishia huduma ya umeme nchini, Serikali imeiagiza *TANESCO* kuhakikisha kuwa wateja wote wanaolipia huduma ya umeme wanaunganishwa katika kipindi cha mwezi mmoja. Aidha, kupitia mgao wa nguzo wa mwezi Oktoba, 2019, nguzo zimeanza kusambazwa kwa kila mkoa, na kupelekwa katika maeneo ya wilaya mbalimbali nchini. Hivyo, Wilaya ya Kibiti ni miongoni mwa wilaya zilizopelekewa nguzo, kwa ajili ya kuwaunganishia wateja wote waliolipia hadi kufikia tarehe 30/10/2019. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ungando; muda wangu si rafiki, muda wangu siyo rafiki.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kibiti ina jumla ya vijiji 58, lakini vijiji ambavyo vimepata umeme ni 37; na umeme huu umepita kwenye maeneo ya barabarani tu. Je, sasa Serikali ina mpango gani kupeleka umeme katika mitaa?

(b) Kibiti ina jumla ya Kata tano, vijiji 17 na vitongoji 42 ambavyo viko *Delta.* Mpaka hivi ninavyoongea wananchi wa kule hawana kabisa umeme. Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kupeleka umeme? Ukizingatia kwamba mpango wa Wizara hii ni kuzima vibatali nchi nzima?

MWENYEKITI: Ahsante majibu kwa maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Nishati.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ally Seif Ungando Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ungando kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo la Kibiti na hususan katika kufuatilia miradi ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema, katika Jimbo hilo letu la Kibiti lina vijiji 58, vijiji 21 ndivyo ambavyo havina umeme. Hata hivyo, kwa sasa kuna mradi unaendelea wa ujazilizi awamu ya pili ambao unatarajia kuanza mwezi Novemba 2019. Mradi huo unaihusisha mikoa tisa, ukiwemo mkoa wa Pwani. vilevile utahusisha vitongoji 1,103. Bunge lako Tukufu liliidhinisha takriban bilioni 197; na hivyo kazi hiyo inataka kuanza. Kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, yale maeneo yot,e hasa zile *centers,* maeneo ya Bungu, maeneo ya Mtawanya maeneo ya Mjawa, na mji mzima wa Kibiti, yatapatiwa umeme kupitiwa umeme mradi

huo. Pia maeneo ya vijiji ambavyo amevitaja, kata tano ambazo hazina umeme kabisa zilizopo katika maeneo ya *Delta,* na vijiji vyake vya Mbuchi, Kiongoroni, Saninga, Salale, Mfisini, Jaja na Keichu na maeneo mbalimbali; kupitia *REA* tutapeleka umeme kwenye maeneo haya ambayo yako nje ya gridi ya taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sasa hivi kinachoendelea ni kufanya *due diligence* kwa mkandarasi ambaye amepatikana; na takriban bilioni 38 zitatumika katika maeneo mbalimbali ya visiwa nchini Tanzania ambayo hayana umeme. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tumekula sana muda wetu; tunaendelea kuwasihi sana maswali na majibu yawe mafupi. Bado; kuna Wizara sitaki kuitaja, ziko mbili namuachia *Chief Whip* kwasababu majibu mnayo, hayo majibu yanaweza kufupishwa sana bila kuathiri maana ya swali lililotaka kupata majibu.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni 10 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa (Mb), Waziri wa Viwanda na Biashara ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo, Prof. Joseph Bunchweishaija, Katibu Mkuu, Ndugu Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Ally Gugu, Mkurugenzi Mtangamano wa Biashara, Ndugu Alfred Mapunda, Mkurugenzi Msaidizi Sera na Mipango, Ndugu Obadiah Nyagiro, Mkurugenzi Sera na Mipango, Ndugu Renatus Theobald, Mkuu wa Kitengo cha Sheria. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 55 wa Mheshimiwa Kapt. Mstaafu George Mkuchika (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni Maafisa wa Takukuru kutoka Makao Makuu na Mikoa ya Tanzania Bara waliopo Dodoma kwa ajili ya Mafunzo ya Mfumo wa Takukuru App. na Kampeni ya Utatu Kuzuia Rushwa Barabarani na Vunja Ukimya, Kataa Rushwa ya Ngono wakiongozwa na Mkurugenzi wa Elimu kwa Umma Ndugu Joseph Mwaiswelo.

Wako wapi wataalam wetu hawa, karibuni sana tunawapongeza sana kwa kazi nzuri mnayoifanya, mnayoendelea kuifanya nchi nzima, naamini na uwakilishi wa Mkoa wa Simiyu upo; nawaona. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb), Waziri wa Kilimo, ambao ni ndugu zake kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Ndugu Iman Bernard. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu (Mb), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Lolensia Bukwimba (Mb), ambao ni kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Askofu wa Kanisa la *Christian Gospel Revavil Assembly* Gideon Parapanda. Mko wapi wageni wetu; karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Josephat Kandege (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambao ni Walimu kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma wakiongozwa na Ndugu Jobu Mwakalambo. Walimu wetu karibuni kokote mlipo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua (Mb), ambaye ni mdogo wake kutoka Masasi Mkoa wa Mtwara Ndugu Deogratius Mkapa. Karibu sana ndugu yetu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Allan Kiula (Mb), ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na wananchi wa Jimbo la Mkalama Ndugu Joram Nyonyi, Ndugu Maria Gole na Ndugu Mussa Gunda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mwantum Dau (Mb), ambaye ni mtoto wake kutoka Zanzibar Ndugu Maryam Ismail. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete (Mb), ambao ni kutoka UMATI; Mwenyekiti wa UMATI Ndugu

Jasmeen Masengi na Dkt. Elisha Makarabo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa John Kadutu (Mb), ambaye ni baba yake mdogo kutoka Mkoa wa Shinyanga, Ndugu Benjamin Masongo. Karibu sana ndugu yetu mzee Masongo. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Jasmine Bunga (Mb), ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoa wa Morogoro Ndugu Fadhilla Tiisekwa. Karibu sana Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mgeni Kadika (Mb), ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam Dkt. Isihak Rashid. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Daniel Mtuka (Mb), ambao ni maafisa waandamizi wa World vision kutoka Wilaya ya Manyoni Mkoa wa Singida Ndugu Joseph Shayo na Ndugu Devota Jonathan. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Zainab Bakar (Mb), ambao ni familia yake kutoka Pemba, Zanzibar wakiongozwa na Baba yake Mzazi Ndugu Mussa Bakar**.** Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rehema Migilla (Mb), ambao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam ambao ni Ndugu Martin Bigawa na Ndugu Zacharia Ntakisigaye. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Tunza Malapo (Mb), ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Maua Mabunda na Ndugu Adrian Mponda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Oran Njeza (Mb), ambao ni wajasiriamali kutoka Mkoa wa Mbeya Ndugu Tanganyika Mwasile, Ndugu Matatizo Kameka na Ndugu Imma Mwanjuguja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Willy Qambalo (Mb), Madiwani kutoka Halmashauri ya Karatu Mkoani Arusha wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Lazaro Gege. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Amina Makilagi ambae ni Mtoto wake anayesoma Chuo Kikuu cha St. Augustine Mtwara Ndugu Elia Dominick. Ndugu Dominick karibu sana. *(Makofi)*

Wageni Waliopo Bungeni kwa ajili ya Mafunzo; hili ni kundi la tatu. Tuna wanafunzi 100 na walimu watano kutoka shule ya Sekondari ya Kikuyu ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Eneda Kahemela. Karibuni sana, mmekuja kwenye mafunzo. *(Makofi)*

Wageni wengine Wanafunzi 100 na Walimu watatu kutoka Dodoma Sekondari ya hapa Jijini Dodoma. Wako wapi? Kundi lingine kubwa hilo la wanafunzi wetu na walimu wao wamekuja kwa mafunzo. *(Makofi)*

Wageni watatu ambao ni Watumishi wa Manispaa ya Ilala wakiongozwa na Ndugu Salehe Kizigha. Manispaa ya Ilala, karibuni sana. *(Makofi)*

Hayo ndiyo matangazo kwa wageni waliopo leo. Lakini nina tangazo; Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas More hapa Bungeni, Mheshimiwa Shally Raymond Mbunge, anaomba niwatangazie Wabunge leo kwamba leo Jumatano tarehe 13 kutakuwa na ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoliki saa 7.00 mchana mara tu baada ya kuahirishwa kwa shughuli za Bunge. Katika ibada hiyo kutakuwepo na nia maalum ya kuombea marehemu Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki pamoja na ndugu zetu jamaa na marafiki. *(Makofi)*

Aidha, Waheshimiwa wote na wageni wote waliopo hapa Bungeni mnaalikwa mjumuike pamoja katika ibada hiyo ambayo inafanyika katika jengo la Pius Msekwa ghorofa

ya pili. Karibuni sana Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo niliyokuwa nayo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Nani anataka Mwongozo?

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mlinga.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Musukuma.

MWENYEKITI: Na iwe ni kwa jambo lililotokea mapema humu Bungeni.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Ndio.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Ndio

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Mlinga.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) ambayo imetokana na swali namba 99 linalohusiana na uunganishwaji na usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imetangaza kuwa wananchi hawapaswi kulipia nguzo, mita na waya na wananchi wakapokea kauli hiyo kwa vifijo na nderemo, matokeo yake wakaruhusu maeneo yao nguzo zipite bila kulipwa fidia. Rais wetu mpendwa ametangaza kuunganishwa umeme ni shilingi 27,000, Mheshimiwa Waziri

Mkuu ametangaza pia na Mheshimiwa Waziri wa Nishati ametangaza umeme ni shilingi 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanapoenda kukutana na watendaji wa *TANESCO* wanapotaka kuunganishiwa umeme wanatozwa kuanzia shilingi 100,000 mpaka shilingi 1,000,000. Watendaji wa *TANESCO* wanasema kauli hizo ni...

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie...

MWENYEKITI: Malizia maana mnanipigia *story*.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kauli ya Serikali, mwananchi wa kawaida Mtanzania anapaswa kulipa shilingi ngapi pindi anapotaka kuunganishiwa umeme wa *TANESCO?*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba mwongozo kwa Kanuni ile ya 68 kwenye swali namba 97, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali namba 97 kuhusiana na michezo ya kubahatisha, ameeleza kwamba wapo kwenye mchakato elimu inatolewa ili kuwaweka kwenye *system* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba suala la michezo ya kubahatisha hizi kamari za Kichina zilizopo huko majimboni kwetu hasa vijijini zimetuletea taabu sana kwa watoto wadogo wanafunzi. Kamari hizi zimewekwa ovyo tu mitaani na watoto wanacheza kuanzia asubuhi mpaka jioni. Ukienda mjini *at least* kuna vyumba, wanafuata utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo, tukienda ofisi inayowasimamia Wachina, Ofisi ya Utamaduni

hawaelewi utaratibu. Nataka kupata mwongozo huu utaratibu unaoendeshwa na Wachina kucheza huko vijijini kwetu uko halali kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa busara yako kwa sababu si jambo lililotokana humu Bungeni lakini ni suala linalohusu na maslahi ya Taifa hasa kwenye huu mwelekeo tunaouenda ambao tunaandikisha vitambulisho vya Taifa vya *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo limekuwa ni kubwa hasa katika majimbo yetu ya vijijini hususan Jimbo langu la Kavuu na Wilaya ya Mlele kwa ujumla kwa maana kwamba uandikishwaji haupo na wananchi wamekuwa wakipata shida na tunajua mwisho ni tarehe 30 Disemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kauli ya Serikali nini kinafanyika mpaka sasa hivi na kifanyike nini kwa wananchi hawa waweze kujiandikisha na kuweza kupata vitambulisho vyao. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Nianze na moja la jumla ambalo ndio maamuzi ya Kiti, maamuzi ya Maspika ya nyuma maana naona sasa swali la nyongeza mtu asiporidhika nalo anataka tu kuingilia kuuliza mwongozo.

Nataka niwaambie kwamba kwa maamuzi ya Spika na kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni zinaruhusu Mbunge aliyeuliza swali na akajibiwa lakini amesimama kuuliza maswali yake ya nyongeza amejibiwa lakini hakujisikia kama amejibiwa ipasavyo ni kwamba sasa hakuridhika, sasa Kiti kitapima kama majibu yaliyotolewa na Serikali wakati swali linajibiwa kama yamejitosheleza au la, Kiti kikiamua kwamba hayajajitosheleza ataelekeza liende likajibiwe tena.

Kwa Mbunge mwingine atakayepata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza atajibiwa na Serikali, kama haridhiki, hawezi akatafuta njia nyingine ya kusema majibu niliyopewa hayakuniridhisha. Wewe una fursa ya kwenda ku-*frame* swali lako kuliwasilisha uweze kujibiwa kikamilifu. Sasa nataka niliweke sawa hilo kwa sababu naona sasa tunaanza kutumia majibu hayo hata kupata nafasi zingine.

Sasa kwa hayo ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe kwa upande wa usajili wa Watanzania kupata Vitambulisho vya Taifa, mchezo wa kamari sio kamari tu, michezo ya bahati nasibu na michezo mingine ya kubahatisha ambayo ipo kwa mujibu wa sheria za nchi na suala la umeme malipo kule wanapotozwa, ni kweli maelezo ya Serikali mwananchi analipa Sh.27,000 tu au vipi? Sasa haya Serikali muyajibu haraka ili twende mbele, maana ratiba yangu ya leo ina msongamano kidogo.

Nianze na Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mlinga kwa kuleta hoja ya kutaka kujua kauli ya Serikali kuhusiana na malipo ya Sh.27,000 au zaidi na kutozwa nguzo. Jibu ni fupi sana, kauli ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza malipo yote ya kuunganisha umeme wateja vijijini ni Sh.27,000 nchi nzima. Kwa hiyo, meneja yoyote haruhusiwi kwa namna yoyote kutoza zaidi ya Sh.27,000 na mtaalam yeyote atakayebainika amefanya kitendo hicho atachukuliwa hatua kali sana za kisheria na kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa kazi. Hiyo ni kauli ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kutozwa nguzo maelekezo ni hayohayo, kwanza wateja wote hawaruhusiwi kutozwa gharama ya nguzo iwe mijini ama vijijini. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na viongozi wote wanaosimamia mamlaka za vijijini na mitaani mpaka mijini watusaidie kutoa

taarifa kwa mteja yeyote atakayetozwa nguzo kwa namna yoyote ili Serikali ichukue hatua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kwa nchi nzima, ni marufuku mara dufu kutoza nguzo na kutoza bei zaidi ya shilingi 27,000 kwa Mtanzania vijijini kuunganishwa umeme. Hiyo ndio kauli ya Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, mchakato wenu huo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Musukuma kwa hoja hii ambayo ameileta hasa kuhusu michezo hii ya kubahatisha inayochezeshwa huko vijijini. Yeye amewataja raia wa nchi fulani, mimi naomba nisiwataje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya kubahatisha inaendeshwa kulingana na Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake na marekebisho yaliyofanyika mwaka huu 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inafuatilia michezo yote ya kubahatisha inayofanyika kwenye maeneo yote Tanzania. Jambo la msingi tunalotakiwa kufahamu sasa ni kwamba Bodi ya Michezo ya Kubahatisha inashirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Mameneja wake wa mikoa wote kuhakikisha wanajua idadi ya michezo ya kubahatisha pamoja na mashine za *slot* zilizopo kwenye mikoa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha, kwa sababu tuna utaratibu wa kuwa-*register* kila mwaka wa fedha, kila baada ya miezi 12 wanatakiwa waombe leseni mpya. Kwa sasa hivi tunazo leseni 3,310 kwa mwaka huu wa fedha ambazo tumeweza kuzi-*register* upya na ndizo zinazofahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tunatambua wapo wanaoendesha michezo hii bila kufuata

taratibu. Bodi ya Michezo ya Kubahatisha naomba niwaelekeze waendelee kufuatilia kila eneo ndani ya Taifa letu ili tujiridhishe kwanza na wapi michezo inafanyika, inafanyika kihalali na wale ambao hawatakiwi kucheza michezo hii ya kubahatisha hasa watoto walio chini ya umri wa miaka 18 hawashiriki kwenye michezo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndio kauli ya Serikali kuhusu jambo hili lililohojiwa na Mheshimiwa Mbunge Musukuma. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Kwa *NIDA* Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya Serikali kuhusiana na suala la Vitambulisho vya Taifa *almaarufu NIDA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba niwaondolee wasiwasi Watanzania wote kwamba zoezi la utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao wana sifa za kupata vitambulisho ni zoezi endelevu halina mwisho wala halina tarehe kwamba ikifika tarehe fulani kuna Mtanzania hajapata kitambulisho basi huyo Mtanzania sasa hatapata kitambulisho tena. Kwa hiyo, Watanzania wasiwe na wasiwasi zoezi hilo ni endelevu. Ndio maana kila mwaka kuna Watanzania wanaofikisha miaka 18 na kuna Watanzania wanaopoteza. Kwa hiyo wale wanaendelea kupata vitambulisho kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili zoezi la kusajili *line* za simu kwa kutumia alama za vidole na kwamba lazima uwe na Kitambulisho cha Taifa *(NIDA).* Zoezi hilo ndilo lina muda wa mwisho wa Desemba mwaka huu. Naomba tena niwatoe wasiwasi Watanzania wote kwamba maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli ni kwamba hakuna Mtanzania ambaye simu yake itazuiwa kutumika eti kwa sababu hana Kitambulisho cha Taifa na hivyo hajasajili laini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la usajili na utambuzi ilikuwa ni 24,500,000 lakini hadi sasa tumekwishasajili Watanzania 20,500,000 na hadi sasa tumekwishazalisha namba za vitambulisho kwa Watanzania 15,500,000. Utaratibu wetu ni kwamba hata Mtanzania ambaye hajapata kitambulisho *(physical ID)* atumie namba yake ya utambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe sasa agizo kwa Mkurugenzi Mkuu wa *NIDA* kwamba maafisa wetu wa *NIDA* wilaya zote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wahakikishe hizi namba ambazo tayari zimekwishazalishwa, wazipeleke kwa wenyewe kule vijijini, tusitegemee masuala ya kuzipata kwenye simu. Wakishazipeleka kila Mtanzania asaini kwamba amepata namba yake na niagize Wakuu wa Wilaya wapate taarifa kutoka kwa Maafisa wa *NIDA* kwamba tayari kila Mtanzania amekwishapata namba yake ya utambulisho ili akimbizane na zoezi la kusajili laini yake ya simu. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Katibu.

NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAAZIMIO

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)*

MWENYEKITI: Namwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), nataka muwasilishe hoja na maazimio yenu hayo moja baada ya lingine, lakini pia na Waziri wa Viwanda hivyo hivyo, halafu Waheshimiwa Wabunge nitayatoa kwenu myajadili kwa

pamoja. Una dakika zako zisizozidi 30, ukitumia muda mfupi nitashukuru sana.

WAZIRI WA MAJI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community SADC – Protocol on Environmental Management for Sustainable Development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The Treaty for the Establishment of The Southern African Development Community)* ulipitishwa tarehe 17 Agosti, 1992 na Nchi 10 ambazo ni Angola, Botswana, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Swaziland, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la mkataba huu ni kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Malengo mengine mahsusi ni pamoja na kuwa na matumizi endelevu ya maliasili na uhifadhi wa mazingira. Aidha, Ibara ya 22 ya Mkataba huu inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwepo kwa changamoto za mazingira zinazovuka mipaka katika Ukanda wa Jumuiya ya *SADC* ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, kuenea kwa hali ya jangwa na ukame, upotevu wa baianowai, kupungua kwa rasilimali za maji, uchakavu wa hewa na kadhalika; na kwa

kuzingatia kuwa masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia na kisiasa, zinahitajika jitihada za pamoja za kukabiliana na changamoto hizo baada ya nchi moja moja ili kuwezesha usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya *SADC* kwa kutambua kuwepo kwa changamoto hizo, zilipitisha Azimio la Kuanzisha Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu tarehe 18 Agosti, 2014 Mjini Gaborone, Botswana. Aidha, nchi wanachama zinatakiwa baada ya kusaini zikamilishe mchakato wa kuridhia kwa kuzingatia sheria na taratibu za ndani ya kila nchi. Aidha, hadi sasa nchi zilizosaini na kuridhia Itifaki ni pamoja na Eswatini, Namibia na Afrika ya Kusini na nchi za Mauritius na Comoros bado hazijasaini Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui ya Itifaki ya *SADC* yanashabihiana na baadhi ya maeneo ya mikataba ya Itifaki mbalimbali za kimataifa za Bara la Afrika na za Kikanda kuhusu usimamizi na uhifadhi wa mazingira ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia. Pamoja na kuwepo kwa mikataba na Itifaki za Kimataifa zinazoshabihiana na Itifaki ya *SADC*, kupitia Itifaki hii nchi wanachama kwa pamoja zitapata fursa zaidi ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali zake tofauti na kutumia mkataba au itifaki nyingine ambazo nchi wanachama zimeridhia kwani mikataba au itifaki hizo hazina uhusianao wa moja kwa moja na rasilimali za pamoja zilizomo ndani ya Ukanda wa Jumuiya ya *SADC*. Vilevile nchi wanachama wa *SADC* zitakuwa na fursa zaidi ya kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka baada ya kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu ina ibara 40, hapa kwa muda nilionao nitataja ibara chache tu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; Ibara ya pili inahusu mawanda ya itifaki kwa kuweka mipaka ya maeneo ya

ushirikiano katika masuala ya usimamizi wa mazingira na maliasili katika Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Ibara ya 4 inahusu malengo ya itifaki ambapo malengo makuu ambayo yatawezesha usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu miongoni mwa Nchi Wanachama kwa kuimarisha usimamizi wa mazingira na matumizi ya maliasili zinazovuka mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 inahusu wajibu wa Nchi Wanachama kwa kuzingatia kuhakikisha malengo ya Itifaki hii yanatekelezwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 inahusu usimamizi wa rasilimali zinazovuka mipaka kwa kuweka utaratibu wa kudhibiti uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia Mkataba wa *SADC* na Itifaki zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 15 inahusu uzingatiaji wa Sheria kwa mujibu wa nchi husika kwa kushirikiana na nchi wanachama katika kuzingatia sheria za mazingira zenye maeneo ikiwemo mifumo ya ufuatiliaji, uzingatiaji na urejeshaji wa wahalifu wanaotokana na makosa ya uharibifu wa mazingira na maliasili zinazovuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 inahusu biashara na uwekezaji endelevu kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Ibara ya 19 inahusu sayansi na teknolojia kwa kutoa fursa kwa nchi kuunganisha nguvu za kifedha na utaalam kwenye masuala ya tafiti na ukuzaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 inahusu utaratibu wa taarifa na upashanaji wa habari baina ya nchi wanachama kushirikiana katika kuandaa na kupashana habari muhimu kwa kuhakikisha malengo ya Itifaki hii yanafikiwa kwa kupeana taarifa za kuwezesha usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 28 inahusu utaratibu wa kifedha katika nchi wanachama kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza Itifaki hii. Ibara ya 32 inahusu utatuzi wa migogoro kwa kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro inayojitokeza baina ya nchi wanachama wa *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 37 inahusu kuridhia pasipo pingamizi na kuweka masharti ya kuridhia Itifaki hii kama ilivyo pasipo pingamizi katika Ibara zote. Ibara ya 38 inahusu marekebisho ya Itifaki kwa kutoa nafasi kwa nchi wanachama kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha Itifaki baada ya kukabiliana na changamoto wakati wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 39 inahusu kujitoa kwenye Itifaki kwa kuweka utaratibu wa nchi Wanachama wa kujitoa ndani ya Itifaki baada ya kupita muda wa miezi kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu kama ifuatavyo:-

Kwa Kuwa, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani *SADC - The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community* iliyopitishwa tarehe 17 Agosti, 1992 na nchi kumi ambazo ni Angola; Botswana; Lesotho; Malawi; Msumbiji; Namibia; Swaziland; Tanzania; Zambia; na Zimbabwe kwa lengo kuu la kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya *SADC.*

Na Kwa Kuwa, Ibara ya 22 ya Mkataba huu inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya *SADC* kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huo.

Na Kwa Kuwa, kwa kuzingatia kuwa, masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia, kisiasa, na kuhitaji jitihada za pamoja za kukabiliana na changamoto hizo, ili kuwezesha usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa *SADC*.

Na Kwa Kuwa, kwa kutambua masuala hayo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani (*SADC*) zilipitisha Azimio la kuanzishwa Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu tarehe 18 Agosti, 2014 huko Gaborone, Botswana na kusainiwa na Nchi 14 kati Nchi 16 ikiwemo Tanzania.

Na Kwa Kuwa, Jumuiya ya Nchi za *SADC* imetambua kuwepo kwa changamoto za mazingira zinazovuka mipaka katika ukanda wa *SADC*, ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; kuenea kwa hali ya majangwa na ukame; upotevu wa bioanuai; kupungua kwa rasilimali za maji; uchakavu wa hewa; uharibifu wa ardhi; uharibifu wa misitu; uharibifu wa vyanzo vya maji; utupaji ovyo wa taka; na kuenea kwa viumbe wageni vamizi.

Na Kwa Kuwa, utekelezaji wa Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Itifaki hii kutaleta fursa zaidi ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali zake ndani ya ukanda wa *SADC* tofauti na kutumia Mikataba au Itifaki nyingine za Kimataifa na za Kikanda ambazo Nchi wanachama zimeridhia kwani Mikataba au Itifaki hizo hazina uhusiano wa moja kwa moja na rasilimali zilizopo ndani ya ukanda wa *SADC*, kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka ndani ya ukanda wa Jumuiya ya *SADC* kuanzisha programu ya tafiti za sayansi za pamoja ambazo zitapunguza gharama za utafiti na utekelezaji wa programu kwa Nchi moja moja na kupata misaada ya kitaalam, kiteknolojia na kifedha kutoka Jumuiya za Kimataifa za Kifedha, mifuko ya kifedha iliyoanzishwa chini ya Jumuiya za kimataifa na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza programu za kikanda ambazo hupewa kipaumbele zaidi ikilinganishwa na programu za Nchi moja moja.

Na Kwa Kuwa, utekelezeji wa Itifaki ya *SADC* utazingatia sheria za ndani ya nchi ambazo ni pamoja na: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297; Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279; Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219; Sheria ya Uhifadhi ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, Sura ya 283; Sheria ya Mali Kale, Sura ya 383; Sheria ya Utalii, Sura ya 65; Sheria ya Ardhi, Sura ya 113; Sheria ya Ardhi za Vijiji, Sura ya 114; Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355; Sheria ya Madini, Sura ya 123; na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Maji, Sura ya 331.

Na Kwa Kuwa, Sheria hizo hazihitaji marekebisho yoyote kwa sasa kwa sababu zina miongozo itakayowezesha utekelezaji wa Itifaki hii.

Hivyo Basi, kwa kuzingatia manufaa yanayotokana na Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Nchi Wanachama, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Saba (17) na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaazimia Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu, yaani *The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development.*

MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA), WAKATI WA KUWASILISHAAZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA SADC YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA AJILI YA MAENDELEO ENDELEVU *(THE SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT COMMUNITY PROTOCOL ON ENVIRONMENTAL MANAGEMENT FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT)* – KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika -The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community ulipitishwa tarehe 17 Agosti, 1992

na Nchi kumi (10) ambazo ni: Angola; Botswana; Lesotho; Malawi; Msumbiji; Namibia; Swaziland (kwa sasa Eswatini); Tanzania; Zambia; na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Mkataba huu ni kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Malengo mengine mahsusi ni pamoja na kuwa na matumizi endelevu ya maliasili na uhifadhi wa mazingira. Aidha, Ibara ya 22 ya Mkataba huu inatoa nafasi kwa nchi wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwepo kwa changamoto za mazingira zinazovuka mipaka katika ukanda wa Jumuiya ya SADC, ambazo ni pamoja na: kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; upotevu wa bioanuai; kupungua kwa rasilimali za maji; uchafuzi wa hewa; uharibifu wa ardhi; uharibifu wa misitu; uharibifu wa vyanzo vya maji; utupaji ovyo taka; na kuenea kwa viumbe wageni vamizi. Na kwa kuzingatia kuwa, masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia na kisiasa, zinahitajika jitihada za pamoja za kukabiliana na changamoto hizo badala ya nchi mojamoja ili kuwezesha usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa SADC.

Mheshimiwa Spika, Nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC, kwa kutambua kuwepo kwa changamoto hizo, zilipitisha Azimio la kuanzisha Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu (The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development tarehe 18 Agosti, 2014 Mjini Gaborone, Botswana. Aidha, Nchi wanachama zinatakiwa baada ya kusaini zikamilishe mchakato wa kuridhia kwa kuzingatia Sheria na taratibu za ndani za kila Nchi. Aidha, hadi sasa Nchi zilizosaini na kuridhia Itifaki hii ni pamoja na: Eswatini, Namibia na Afrika Kusini na Nchi za Mauritius na Comoros bado haijasaini Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya Itifaki ya *SADC* yanashabihiana na baadhi ya maeneo ya Mikataba na Itifaki mbalimbali za Kimataifa, za Bara la Afrika na za Kikanda kuhusu usimamizi na uhifadhi wa mazingira ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia. Pamoja na kuwepo kwa Mikataba na Itifaki za Kimataifa zinazoshabihiana na Itifaki ya *SADC,* kupitia Itifaki hii, nchi wanachama kwa pamoja zitapata fursa zaidi ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali zake tofauti na kutumia Mikataba au Itifaki nyingine ambazo Nchi wanachama zimeridhia kwani Mikataba au Itifaki hizo hazina uhusiano wa moja kwa moja na rasilimali za pamoja zilizomo 3 ndani ya ukanda wa Jumuiya ya *SADC.* Vilevile, nchi wanachama wa *SADC* zitakuwa na fursa zaidi ya kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka baada ya kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu ina Ibara 40. Baada ya uchambuzi wa kina tumebaini Ibara zifuatazo kati hizo kuwa ni muhimu Bunge lako likazitambua, Ibara hizo ni:-

(i) Ibara ya 2: Inahusu mawanda ya Itifaki kwa kuweka mipaka ya maeneo ya ushirikiano katika masuala ya usimamizi wa mazingira na maliasili katika Jumuiya ya *SADC.*

(ii) Ibara ya 4: Inahusu malengo ya Itifaki ambapo malengo makuu ambayo yatawezesha usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu miongoni mwa Nchi wanachama kwa kuimarisha usimamizi wa mazingira na matumizi ya maliasili zinazovuka mipaka ya nchi.

(iii) Ibara ya 13: Inahusu wajibu wa nchi wanachama kwa kuzitaka kuhakikisha malengo ya Itifaki hii yanatekekelezwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya *SADC.*

(iv) Ibara ya 14: Inahusu usimamizi wa rasilimali zinazovuka mipaka kwa kuweka utaratibu wa kudhibiti uharibifu wa mazingira na usimamizi wa rasilimali zinazovuka mipaka kwa kuzingatia Mkataba wa *SADC* na Itifaki zake.

(v) Ibara ya 15: Inahusu uzingatiaji wa Sheria kwa mujibu wa nchi husika kwa kushirikiana na nchi wanachama katika kuzingatia sheria za mazingira kwenye maeneo ikiwemo mifumo ya ufuatiliaji, uzingatiaji na urejeshaji wa wahalifu wanaotokana na makosa ya uharibifu wa mazingira na maliasili zinazovuka mipaka.

(vi) Ibara ya 18: Inahusu biashara na uwekezaji endelevu kwa kuzingatia hifadhi ya mazingira. Ibara hii inatoa fursa kwa jamii kutambua na kuwekeza kwenye sekta ya mazingira kwa kuhamasisha uwekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika nishati mbadala.

(vii) Ibara ya 19: Inahusu sayansi na teknolojia kwa kutoa fursa kwa nchi kuunganisha nguvu za kifedha na utaalam kwenye masuala ya tafiti na ukusaji wa teknolojia.

(viii) Ibara ya 21: Inahusu uratibu wa taarifa na upashanaji habari baina ya nchi wanachama kushirikiana katika kuandaa na kupashana habari muhimu kwa kuhakikisha malengo ya Itifaki hii yanafikiwa kwa kupeana taarifa za kuwezesha usimamizi wa mazingira na maendeleo endelevu.

(ix) Ibara ya 28: Inahusu utaratibu wa kifedha katika nchi wanachama kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza Itifaki hii. Uwepo wa Ibara hii utawezesha masuala ya mazingira kupewa kipaumbele katika kutengewa rasilimali fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

(x) Ibara ya 32: Inahusu utatuzi wa migogoro kwa kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro inayoweza kujitokeza baina ya Nchi wanachama wa *SADC* katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa Itifaki hii. Ibara hii itawezesha Nchi wanachama kutatua migogoro kwa njia ya amani, urafiki na hivyo kuongeza fursa za mtangamano baina ya Nchi wanachama wa *SADC*. Iwapo njia ya amani itashindikana, usuluhishi utafanyika kwa njia ya Kamati ya

Baraza la Mawaziri wa Mazingira wa *SADC* au Mahakama ya *SADC.*

(xi) Ibara ya 37: Inahusu kuridhia pasipo pingamizi na kuweka masharti ya kuridhia Itifaki hii kama ilivyo pasipo pingamizi katika Ibara zote.

(xii) Ibara ya 38: Inahusu marekebisho ya Itifaki kwa kutoa nafasi kwa nchi wanachama kuwasilisha mapendekezo ya kurekebisha Itifaki baada ya kukabiliana na changamoto wakati wa utekelezaji.

(xiii) Ibara ya 39: Inahusu kujitoa kwenye Itifaki kwa kuweka utaratibu kwa nchi mwanachama wa kujitoa ndani ya Itifaki baada ya kupita muda wa miezi kumi na mbili (12) tangu kuwasilisha ombi la kujitoa kwa njia ya maandishi kwa Katibu Mtendaji wa SADC. Utaratibu huu unatoa fursa kwa Nchi Mwanachama kutathmini utekelezaji wa Itifaki kabla ya kuamua kujitoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu kama ifuatavyo:

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika - *The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community* iliyopitishwa tarehe 17 Agosti, 1992 na Nchi kumi (10) ambazo ni Angola; Botswana; Lesotho; Malawi; Msumbiji; Namibia; Swaziland (kwa sasa Eswatini); Tanzania; Zambia; na Zimbabwe kwa lengo kuu la kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

NA KWA KUWA, Ibara ya 22 ya Mkataba huu inatoa nafasi kwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano

yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huo;

NA KWA KUWA, kwa kuzingatia kuwa, masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia, kisiasa, na kuhitajika jitihada za pamoja za kukabiliana na changamoto hizo, ili kuwezesha usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa SADC; 7

NA KWA KUWA, kwa kutambua masuala hayo, nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) zilipitisha Azimio la kuanzisha Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)* tarehe 18 Agosti, 2014 Gaborone, Botswana na kusainiwa na Nchi 14 kati 16 ikiwemo Tanzania;

NA KWA KUWA, Jumuiya ya nchi za *SADC* imetambua kuwepo kwa changamoto za mazingira zinazovuka mipaka katika ukanda wa SADC, ambazo ni pamoja na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; upotevu wa bioanuai; kupungua kwa rasilimali za maji; uchafuzi wa hewa; uharibifu wa ardhi; uharibifu wa misitu; uharibifu wa vyanzo vya maji; utupaji ovyo taka; na kuenea kwa viumbe wageni vamizi;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Itifaki hii kutaleta fursa zaidi ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali zake ndani ya ukanda wa *SADC* tofauti na kutumia Mikataba au Itifaki nyingine za Kimataifa na za Kikanda ambazo Nchi wanachama zimeridhia kwani Mikataba au Itifaki hizo hazina uhusiano wa moja kwa moja na rasilimali zilizomo ndani ya ukanda wa *SADC*, kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka ndani ya ukanda wa Jumuiya ya SADC kuanzisha programu za tafiti za sayansi za pamoja ambazo zitapunguza gharama za utafiti na utekelezaji wa program kwa nchi mojamoja na kupata misaada ya kitaalam, kiteknolojia na kifedha kutoka Jumuiya

za Kimataifa za Kifedha, mifuko ya kifedha iliyoanzishwa chini ya Jumuiya za kimataifa na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza programu za kikanda ambazo hupewa kipaumbele zaidi ikilinganishwa na program za Nchi mojamoja;

NA KWA KUWA, utekelezeji wa Itifaki ya SADC utazingatia sheria za ndani ya nchi ambazo ni pamoja na: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sura ya 297; Sheria ya Uvuvi, Sura ya 279; Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182; Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219; Sheria ya Uhifadhi ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, 283; Sheria ya Mali Kale, Sura ya 383; Sheria ya Utalii, Sura ya 65; Sheria ya Ardhi, Sura 113; Sheria ya Ardhi za Vijiji, Sura 114; Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355; Sheria ya Madini, Sura ya 123; na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sura ya 331;

NA KWA KUWA, Sheria hizo hazihitaji marekebisho yoyote kwa sasa kwa sababu zina miongozo itakayowezesha utekelezaji wa Itifaki hii.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa Nchi wanachama, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Saba (17) na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka linaazimia Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu yaani *The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya kupunguza uzalishaji wa matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydro Fluorocarbons (HFCs)* chini ya Itifaki ya *Montreal* inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la *OZONI (Kigali Amendment on Phasing Down Hydro Fluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*)

WAZIRI WA MAJI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja ya Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya kupunguza uzalishaji wa matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydro Fluorocarbons (HFCs)* chini ya Itifaki ya *Montreal* inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la *OZONI (Kigali Amendment on Phasing Down Hydro Fluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Vienna kuhusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni *(The Vienna Convention for the Protection of the Ozone Layer)* ulianza kutekelezwa na Nchi Wanachama mwaka 1988 na Tanzania iliridhia mwaka 1993. Lengo kuu la Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na kumong'onyoka kwa Takaba la Ozoni ambalo huzuia Mionzi ya Urujuani (*Ultraviolet - B Radiation*) kutoka kwenye jua lisifike duniani. Aidha, Ibara ya 8 ya Mkataba wa Vienna inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Ibara hii, Itifaki ya *Montreal* Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni ilianzishwa na kuanza kutekelezwa mwaka 1989 baada ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuridhia ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo irilidhia tarehe 16 Agosti, 1993. Katika utekelezaji wa Itifiki hiyo, yamefanyika

marekebisho mara sita. Kati ya marekebisho hayo, marekebisho matano yameridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa inatakiwa kuridhia marekebisho ya sita (6) yaliyofanyika mwezi Oktoba mwaka 2016 Mjini Kigali Rwanda. Marekebisho haya yanahusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *Hydro Fluorocarbons* (*HFCs*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi na uzalishaji wa Kemikali jamii ya *HFCs* yameonyesha kuwa na athari katika mazingira na kuchangia ongezeko la joto duniani na hatimaye mabadiliko ya tabianchi ambayo athari zake tayari yamejitokeza hapa nchini.

Aidha, hadi kufikia tarehe 4 Oktoba, 2019 nchi 85 zimeridhia Marekebisho ya Kigali zikiwemo nchi mbili za Afrika ya Mashariki ambazo ni Rwanda na Tanzania na yameanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2019 baada ya nchi ishirini kuridhia kwa mujibu wa Ibara IV ya Marekebisho ya Kigali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama nchi Mwanachama wa Itifaki ya *Montreal*, haina budi kuridhia Marekebisho ya Kigali kwa kuwa tayari athari za mabadiliko ya tabianchi yamejitokeza hapa nchini katika uchumi na maendeleo ya kijamii hasa katika sekta ya Kilimo, Maji, Mifugo, Nishati na miundombinu kutokana na upungufu wa mvua za uhakika; ukame wa muda mrefu; na mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania kuridhia marekebisho ya Kigali kutaiwezesha Nchi kuchangia juhudi za kimataifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupokea teknolojia mbadala wa Kemikali Jamii ya *HFCs* na rasilimali fedha za kutekeleza Marekebisho ya Kigali kupitia Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya *Protocol* ulioanzishwa kwa ajili ya kuzisaidia nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Kigali yana vipengele vingi, kati ya vipengele vilivyorekebishwa vipengele muhimu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 1(4) inayohusu Tafsiri, Ibara hii imeongezewa wigo wa tafsiri ya kemikali zinazodhibitiwa na Itifaki ya *Montreal*, kupitia Marekebisho ya Kigali ya Mwaka 2016, kwa kujumuisha Kemikali Jamii ya *Hydro Fluorocarbons (HFCs)* ambazo hazikuwepo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2J inayohusu *hydro fluorocarbons (HFCs),* Ibara hii inaongeza wajibu wa ziada kwa Nchi Wanachama wa kupunguza uzalishaji wa matumizi ya Kemikali Jamii ya *HFCs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 3(2) inahusu Ukokotoaji wa Viwango vya Udhibiti wa Kemikali, Ibara hii inawezesha utambuzi wa viwango vya kuchangia ongezeko la joto duniani kwa kila Kemikali Jamii ya *CFCs*, *HCFCs* na *HFCs* na hivyo kutuwezesha kupima hatua kwa hatua kiwango cha kupunguza Kemikali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(1) Septemba) inahusu Udhibiti wa Biashara Kati ya Nchi zisizo Wanachama, Ibara hii inatoa nafasi ya kuendelea kufanya biashara na nchi zisizowanachama kwa kipindi cha miaka kumi na nne kutoka sasa. Ibara ya 5 inahusu Utaratibu Maalum kwa nchi zinazoendelea: Ibara ya 5(6) kutoa nafasi kwa Nchi zinazoendelea ambazo ni Wanachama wa Marekebisho ya Kigali kupewa muda zaidi wa kuchelewa kuanza kutekeleza; na Ibara ya 5(8) *qua* kuzipa unafuu wa nchi zinazoendelea katika kupunguza uzalishaji na matumizi ya Kemikali hii ikilinganishwa na nchi zilizoendelea ambazo zinatakiwa kupunguza kwa asilimia 85 ifakapo mwaka 2036.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7(3) inahusu Uwasilishaji wa Takwimu. Ibara hii itawezesha nchi kujua kiwango cha kemikali cha *HFCs* kinachoingizwa na kinachotumika ili kuweka mikakati ya Kitaifa ya kuondosha kemikali hizo hatua kwa hatua kulingana na matakwa ya Marekebisho ya Kigali.

Na Kwa Kuwa, katika utekelezaji wa Itifaki ya *Montreal* yamefanyika marekebisho mara sita ambayo ni:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya *hydro fluorocarbons (HFCs)* Chini ya Itifaki ya *Montreal* Inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni kama ifuatavyo:

Moja, Kwa Kuwa, Mkataba wa Vienna Unahusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni ulianza kutekelezwa na Nchi Wanachama mwaka 1988 kwa lengo kuu la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na kumong'onyoka kwa Tabaka la Ozoni na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba huo mwaka 1993;

Na Kwa Kuwa, Ibara ya 8 ya Mkataba wa Vienna inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama, kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano, kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba na hatimaye kusaidia kuanzishwa kwa Itifaki ya *Montreal*, inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni na kuanza kutekelezwa mwaka 1989 baada ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuridhia, ikiwemo Tanzania ambayo iliridhia tarehe 16 Agosti mwaka 1993.

Na Kwa Kuwa, katika utekelezaji wa Itifaki ya *Montreal* yamefanyika marekebisho mara sita ambayo Marekebisho ya London mwaka 1990 yaliyohusu kusitisha uzalishaji na matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *Chlorofluorocarbons; Carbon tetrachloride*; na *Methyl chloroform*, ambayo yaliridhiwa na Tanzania tarehe 16 Agosti mwaka 1993. Marekebisho ya *Copenhagen* yaliyohusu kusitisha uzalishaji na matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *Methyl bromide*, *Hydro bromo fluorocarbons* na *Hydro chlorofluorocarbons* (HCFCs) ambayo yaridhiwa na Tanzania tarehe 6 Disemba mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya Vienna ya mwaka 1995 yaliyohusu kupunguza uzalishaji na matumizi ya Kemikali Jamii ya *Chlorofluorocarbons (CFCs)* ambayo Tanzania iliridhia tarehe 6 Disemba, 2002; Marekebisho ya

Montreal mwaka 1997 yalihusu kuweka mfumo wa usimamizi na uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa Kemikali Jamii ya *HCFCs* ambayo Tanzania iliridhia tarehe 6 Disemba, 2002; Marekebisho ya Beijing ya mwaka 1999 ya kusitisha uzalishaji wa matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *Bromochloromethane* ambayo Tanzania iliridhia tarehe 6 Disemba mwaka 2002; na Marekebisho ya Kigali ya mwaka 2016 yanayohusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *hydro fluorocarbons* yaani *(HFCs)* ambayo yanatakiwa kuridhiwa na Nchi Wanachama wa Itifaki ya *Montreal* ikiwemo Tanzania.

Na Kwa Kuwa, matumizi ya uzalishaji wa Kemikali Jamii ya *HFCs* yameonyesha kuwa na athari katika mazingira zinazosababishwa na uvujaji Kemikali kutoka katika vifaa husika vikiwemo majokofu, viyoyozi, vifaa vya kuzima moto na mitambo ya viwandani, na inakadiriwa uchafuzi utokanao na Kemikali hizo wa kg 1 ni mara 10,000 ya kg 1 ya Hewa Ukaa yaani *carbon dioxide* ambayo huchangia ongezeko la joto duniani na hatimaye mabadiliko ya tabianchi ambayo tayari athari zake zimejitokeza hapa Duniani.

Na Kwa Kuwa, Nchi Wanachama wa Itifaki ya *Montreal* zilichukua hatua ya kurekebisha Itifaki ya *Montreal*, ili kuanza kupunguza na hatimaye kuondosha kabisa matumizi ya Kemikali Jamii ya *hydro fluorocarbons* na kupitishwa katika Mkutano uliofanyika Kigali Rwanda mwezi Oktoba mwaka 2016 na hadi kufikia tarehe 30 Oktoba, 2019 nchi 85 zimeridhia zikiwemo Nchi mbili za Afrika Mashariki ambazo ni Rwanda na Uganda na yameanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2019.

Na Kwa Kuwa, utekelezaji wa Itifaki hii kwa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, na kwa Nchi Wanachama wa Itifaki hii, kutaleta manufaa ya kupunguza Kemikali Jamii ya *HFCs* kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2047 ambazo ni sawa na kupunguza ongezeko la joto Duniani kwa nyuzi 0.5.

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali utazingatia sheria za nchi ikiwa ni pamoja na Sheria ya

Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 na kufanya marekebisho katika Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Kemikali Zinazoharibu Tabaka la Ozoni) za Mwaka 2007;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii, kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Saba na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, lina azimia kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydrofluorocarbons (HFCs),* Chini ya Itifaki ya *Montreal* Inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni *(Kigali Amendment On Phasing Down Hydrofluorocarbons to the Montreal Protocol on Ozone Depleting substances.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA WAKATI WA KUWASILISHA AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAREKEBISHO YA KIGALI YA KUPUNGUZA UZALISHAJI NA MATUMIZI YA KEMIKALI JAMII YA HYDROFLUOROCARBONS (HFCs) CHINI YA ITIFAKI YA MONTREAL INAYOHUSU KEMIKALI ZINAZOMONG'ONYOA TABAKA LA OZONI (Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to the Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Vienna Kuhusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni (The Vienna Convention for the Protection of the Ozone Layer) ulianza kutekelezwa na Nchi Wanachama mwaka 1988 na Tanzania iliridhia mwaka 1993. Lengo kuu la Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na kumong'onyoka kwa Takaba la Ozoni ambalo huzuia Mionzi ya Urujuani (Ultraviolet - B Radiation) kutoka kwenye jua lisifike duniani. Aidha, Ibara ya 8 ya Mkataba wa Vienna inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Ibara hii, Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni ilianzishwa na kuanza kutekelezwa mwaka 1989 baada ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuridhia ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo irilidhia tarehe 16 April, 1993.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Itifiki hii, yamefanyika marekebisho mara sita (**6**). Kati ya marekebisho hayo, marekebisho matano (**5**) yameridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa inatakiwa kuridhia marekebisho ya sita (**6**) yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2016 Mjini Kigali, nchini Rwanda. Marekebisho haya yanahusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs).

Mheshimiwa Spika, matumizi na uzalishaji wa kemikali jamii ya HFCs yameonesha kuwa na athari katika mazingira na kuchangia ongezeko la joto duniani na hatimaye mabadiliko ya tabianchi ambayo athari zake tayari zimejitokezahapa hapa nchini. Aidha, hadi kufikia tarehe 04 Oktoba, 2019 Nchi **85** zimeridhia Marekebisho ya Kigali zikiwepo nchi mbili (**2**) za Afrika Mashariki ambazo ni Rwanda na Uganda na yameanza kutekelezwa tarehe 01 Januari, 2019 baada ya Nchi ishirini (**20**) kuridhia kwa mujibu wa Ibara IV ya Marekebisho ya Kigali.

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama nchi mwanachama wa Itifaki ya Montreal, haina budi kuridhia Marekebisho ya Kigali kwa kuwa tayari athari za mabadiliko ya tabianchi zimejitokeza hapa nchini katika uchumi na maendeleo ya kijamii hususan katika sekta za kilimo, mifugo, nishati na miundombinu kutokana na upungufu wa mvua za uhakika; ukame wa muda mrefu; na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, kwa Tanzania kuridhia marekebisho ya Kigali kutaiwezesha Nchi kuchangia juhudi za kimataifa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kupokea teknolojia mbadala wa Kemikali Jamii ya HFCs na rasilimali fedha za kutekeleza Marekebisho ya Kigali kupitia Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal (Multilateral Fund for

Implementation of the Montreal Protocol) ulioanzishwa kwa ajili ya kuzisaidia Nchi Zinazoendelea ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Kigali yana vipengele vingi, kati ya vipengele vilivyorekebishwa vipengele muhimu ni kama vifuatavyo:-

Ibara ya 1(4) inayohusu Tafsiri: Ibara hii imeongeza wigo wa tafsiri ya kemikali zinazodhibitiwa na Itifaki ya Montreal, kupitia Marekebisho ya Kigali ya Mwaka 2016, kwa kujumuisha kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) ambazo hazikuwepo awali.

Ibara ya 2J inayohusu Hydrofluorocarbons (HFCs): Ibara hii inaongeza wajibu wa ziada kwa Nchi Wanachama wa kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya HFCs.

Ibara ya 3(2) inayohusu Ukokotoaji wa Viwango vya Udhibiti wa Kemikali: Ibara hii inawezesha utambuzi wa viwango vya kuchangia ongezeko la joto duniani kwa kila kemikali jamii za CFCs, HCFCs na HFCs na hivyo kutuwezesha kupima hatua kwa hatua kiwango cha kupunguza kemikali hizo.

Ibara ya 4(1 sept) inayohusu Udhibiti wa Biashara Kati ya Nchi Zisizo Wanachama: Ibara hii inatoa nafasi ya kuendelea kufanya biashara na nchi zisizowanachama kwa kipindi cha miaka kumi na nne (**14**) kutoka sasa.

Ibara ya 5 inayohusu Utaratibu Maalum kwa Nchi Zinazoendelea: Ibara ya 5(6) kutoa nafasi kwa Nchi Zinazoendelea ambazo ni wanachama wa Marekebisho ya Kigali kupewa muda zaidi wa kuchelewa kuanza kutekeleza; na **Ibara ya 5(8qua)** kuzipa unafuu Nchi Zinazoendelea katika kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali hii ikilinganishwa na Nchi Zilizoendelea ambazo zinatakiwa kupunguza kwa asilimia **85** ifakapo mwaka 2036.

Ibara ya 7(3) inayohusu Uwasilishaji wa Takwimu. Ibara hii itawezesha nchi kujua kiwango cha kemikali za HFCs kinachoingizwa na kinachotumika ili kuweka mikakati ya

kitaifa ya kuondosha kemikali hizo hatua kwa hatua kulingana na matakwa ya Marekebisho ya Kigali.

Ibara ya 10(1) inayohusu Utaratibu wa Upatikanaji wa Rasilimali Fedha. Ibara hii inatoa fursa kwa nchi zinazoendelea (ikiwemo Tanzania) kupata misaada ya kifedha, kitaalamu na kiteknolojia kwa ajili ya kutekeleza Marekebisho ya Kigali na kutoa angalizo kuhusu gharama za ziada za utekelezaji wa Itifaki.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) Chini ya Itifaki ya Montreal Inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni kama ifuatavyo:

KWA KUWA, Mkataba wa Vienna Unaohusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni (The Vienna Convention for the Protection of the Ozone Layer) ulianza kutekelezwa na Nchi Wanachama mwaka 1988 kwa lengo kuu la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na kumong'onyoka kwa Tabaka la Ozoni na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 1993;

NA KWA KUWA, ibara ya 8 ya Mkataba wa Vienna inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama, kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano, kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba na hatimaye kusaidia kuanzishwa kwa Itifaki ya Montreal, inayohusu Kemikali Zinazomongónyoa Tabaka la Ozoni (Itifaki ya Montreal) na kuanza kutekelezwa mwaka 1989 baada ya Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuridhia, ikiwemo Tanzania ambayo iridhia tarehe 16 Aprili, 1993;

NA KWA KUWA, katika utekelezaji wa Itifaki ya Montreal yamefanyika marekebisho mara sita ambayo ni:

(a) Marekebisho ya London (1990) yaliyohusu kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Chlorofluorocarbons

(CFCs); Carbon tetrachloride; na Methylchloroform, ambayo yaliridhiwa Tanzania tarehe 16 Aprili, 1993;

(b) Marekebisho ya Copenhagen (1992) yaliyohusu kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Methylbromide, Hydrobromofluorocarbons(HBFCs) na Hydrochlorofluorocarbons (HCFCs) ambayo yaridhiwa na Tanzania tarehe 06 Desemba, 2002;

(c) Marekebisho ya Vienna (1995)yaliyohusu kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Chlorofluorocabons (CFCs) ambayo Tanzania iliridhia tarehe 06 Desemba, 2002;

(d) Marekebisho ya Montreal (1997) yaliyohusu kuweka mfumo wa usimamizi wa uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa kemikali jamii ya HCFCs ambayo Tanzania iliridhia tarehe 06 Desemba, 2002;

(e) Marekebisho ya Beijing (1999) ya kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Bromochloromethane ambayo Tanzania iliridhia tarehe 06 Disemba, 2002; na

(f) Marekebisho ya Kigali (2016) yanayohusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) ambayo yanatakiwa kuridhiwa na Nchi Wanahama wa Itifaki ya Montreal ikiwemo Tanzania.

NA KWA KUWA, matumizi na uzalishaji wa kemikali jamii ya HFCs yameonesha kuwa na athari katika mazingira zinazosababishwa na uvujaji kemikali kutoka katika vifaa husika vikiwemo majokofu, viyoyozi, vifaa vya kuzima moto na mitambo ya viwandani, na inakadiriwa uchafuzi utokanao na kemikali hizo wa kg **1** ni mara **10,000** ya kg **1** ya Hewa Ukaa (CO2) ambayo huchangia ongezeko la joto duniani na hatimaye mabadiliko ya tabianchi ambayo tayari athari zake zimejitokeza hapa nchini;

NA KWA KUWA, Nchi Wanachama wa Itifaki ya Montreal zilichukua hatua ya kurekebisha Itifaki ya Montreal, ili kuanza kupunguza na hatimaye kuondosha kabisa matumizi ya

kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) na kupitishwa katika Mkutano uliofanyika Kigali, Rwanda mwezi Oktoba, 2016 na hadi kufikia tarehe 30 Oktoba, 2019 nchi 85 zimeridhia zikiwemo Nchi mbili (2) za Afrika Mashariki ambazo ni Rwanda na Uganda na yameanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2019;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Itifaki hii kwa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, na kwa Nchi Wanachama wa Itifaki hii, kutaleta manufaa ya kupunguza kemikali jamii ya HFCs kwa asilimia 85 ifikapo mwaka 2047 ambapo ni sawa na kupunguza ongezeko la joto duniani kwa kiasi cha 0.50C na hatimaye kuchangia kupungua kwa athari za mabadiliko ya tabianchi, kuongezeka kwa fursa ya upatikanaji wa rasilimali fedha, teknolojia mbadala na kujengewa uwezo wa kitaalam katika kutekeleza Marekebisho ya Kigali na kuchangia kupungua kwa matumizi ya rasilimali za ndani za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali utazingatia Sheria za Nchi ikiwa ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, na kufanya marekebisho katika Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Kemikali Zinazoharibu Tabaka la Ozoni) za Mwaka 2007;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge hili katika Mkutano wa **Kumi na Saba** na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (**Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to The Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances**.

Mheshimiwa Spika; naomba kuwasilisha na kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana kwa kuwasilisha haya maazimio mawili.

Sasa Mwenyekiti wa Kamati husika; Viwanda, Mazingira, ooh! Kwa niaba yake Mheshimiwa Ntimizi, una muda usiozidi dakika 15, kwa yote mawili, siyo moja tu. Yako mawili.

Wewe unasoma moja tu!

MHE. MUSA R. NTIMIZI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA): Ndiyo.

MWENYEKITI: Haya. Ukinitunzia muda wangu, nitashukuru sana.

MHE. MUSA R. NTIMIZI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba nitoe Maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) na (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya *SADC* kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)*, ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge kuliridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Itifaki ya *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community) of 1992.* Lengo kuu la mkataba huu ni kukuza uchumi, kupunguza umasikini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Jumuiya ya *SADC* ina malengo mengine mahsusi ambapo moja kati ya malengo hayo ni kuwa na matumizi endelevu ya maliasili na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Itifaki ya *SADC* kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ni changamoto za mazingira zinazoendelea kuibuka ambazo zinavuka mipaka katika Ukanda wa *SADC.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto hizi na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 22 ambayo inatoa nafasi kwa nchi wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa mkataba huo, nchi wanachama zilipitisha Azimio la kuanzisha Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management and Sustainable Development)* mnamo tarehe 18 Agosti, 2014, Mjini *Gaborone, Botswana.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za kimazingira zinazotazamiwa kutatuliwa na Itifaki ya *SADC* kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ni pamoja na Kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; upotevu wa bioanuai; kupungua kwa rasilimali za maji; uchafuzi wa hewa; uharibifu wa ardhi na misitu; na kuenea kwa viumbe wageni wavamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge ambapo ilitekeleza shughuli hizo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa Mkataba huu ulioletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati ni pamoja na madhumuni na maudhui ya Itifaki, faida za kuridhia Itifaki hii na hasara kama nchi haitaridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhumuni la kuanzishwa kwa Itifaki hii ni kuhakikisha unawekwa mfumo rasmi wa pamoja wa usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa *SADC* ikizingatiwa kuwa, masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifahamishwa kuwa, baada ya kuridhia Itifaki hii, Nchi Wanachama wa *SADC* zitakuwa na fursa ya kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka. Katika Ukanda wa *SADC* rasilimali zinazovuka mipaka ya nchi moja kwenda nchi nyingine ni pamoja na: Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Mto Zambezi, Mto Ruvuma, Mto Save/Sabi, Mto Embeluzi, Mto Songwe, Mto Congo, Mto Limpopo, Mto Orange, Bwawa la Kariba, Jangwa la Kalahari na Msitu wa Congo. Kila nchi ina wajibu wa kusimamia na kuhifadhi rasilimali zake kwa mujibu wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijiridhisha kuwa utekelezaji wa Itifaki hii haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Sema kwa lengo la kutekeleza masharti ya Itifaki hii ipasavyo, tunahitaji kuandaa Kanuni na Miongozo chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ili kwenda sambamba na makubaliano ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilijiridhisha juu ya faida zitakazopatikana kutokana na kuridhia Itifaki hii. Faida hizo ni pamoja na Kuongeza uwezo wa nchi wa kukabiliana na changamoto za kimazingira zinazovuka mipaka ya nchi; kuimarisha usimamizi wa pamoja wa maliasili zinazovuka mipaka ya nchi; kuchangia ustawi wa hali ya uchumi na maisha ya jamii; na kuchangia kuimarika kwa amani na usalama kati ya nchi yetu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community) of 1992* pamoja na baadhi ya Itifaki zake; na

KWA KUWA, Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa *SADC* na inalenga kuweka nguvu za pamoja katika kusimamia na kuhifadhi mazingira na matumizi endelevu ya maliasili zinazovuka mipaka ya nchi moja kwenda nyingine; kuhamasisha matumizi sahihi na endelevu ya maliasili kwa faida ya kizazi cha sasa na baadaye; na kuimarisha usimamizi thabiti wa kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na

KWA KUWA, sote kunakubaliana kuwa masuala ya Mazingira ni Mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia wala ya kisiasa, inahitajika ushirikiano na jitihada za pamoja baina ya Nchi Wanachama katika kukabiliana na changamoto zilizopo na hatimaye kuweka usimamizi

utakaopelekea matumizi endelevu ya rasilimali zetu na kuleta maendeleo endelevu katika Ukanda wa *SADC;*

HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge lako Tukufu kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ili kuunganisha nguvu na wanachama wenzetu wa *SADC* katika kuleta mwamko wa uzingatiaji wa dhana ya usimamizi endelevu wa mazingira kwa wananchi wa ukanda wa *SADC* wakati wa kuendesha shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Namshukuru pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuwashukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Naibu Waziri Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Makatibu Wakuu, pamoja na wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba orodha yao iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Michael Chikokoto na Katibu wa Kamati Bi Zainabu Mkamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA SADC KUHUSU USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MAENDELEO ENDELEVU *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)* - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) na (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development)*, ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge kuliridhia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Itifaki ya SADC.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community)* wa 1992. Lengo kuu la Mkataba huu ni kukuza uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maisha bora kwa watu wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Jumuiya ya SADC ina Malengo mengine mahsusi ambapo moja kati ya malengo hayo ni kuwa na matumizi endelevu ya maliasili na uhifadhi wa mazingira.

2.0 CHIMBUKO LA ITIFAKI YA SADC

Mheshimiwa Spika, chimbuko la Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo endelevu ni changamoto za mazingira zinazoendelea kuibuka ambazo

zinavuka mipaka katika Ukanda wa SADC. Kwa kutambua changamoto hizo na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 22 ambayo inatoa nafasi kwa Nchi Wanachama kuanzisha Itifaki mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya ushirikiano yanayohitajika kwa wakati husika kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba huo, Nchi Wanachama zilipitisha Azimio la kuanzisha Itifaki ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management and Sustainable Development)* mnamo tarehe 18 Agosti, 2014, Mjini Gaborone, Botswana.

Mheshimiwa Spika, changamoto za kimazingira zinazotazamiwa kutatuliwa na Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ni pamoja na Kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi; Kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; Upotevu wa bioanuai; Kupungua kwa rasilimali za maji; Uchafuzi wa hewa; Uharibifu wa ardhi na misitu; na Kuenea kwa viumbe wageni vamizi.

3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu;-

i) Tarehe 6 Novemba, 2019 Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Itifaki ya SADC, maelezo hayo yaliwasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuridhia Itifaki hii;

ii) Tarehe 7 Novemba, 2019, Kamati ilipokea Uchambuzi wa Sekretarieti ya Kamati juu ya Dhana ya Itifaki pamoja na vipengele vya Kisheria katika Itifaki hii, Uchambuzi huu uliwasaidia wajumbe kupata uelewa na kuwaweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii; na

iii) Tarehe 9 Novemba, 2019, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliwapatia wajumbe Semina ya kujenga uelewa katika itifaki husika. Semina hii iliiwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake.

4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati ni pamoja na madhumuni na maudhui ya Itifaki, faida za kuridhia Itifaki hii na hasara kama nchi haitaridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, dhumuni la kuanzishwa kwa itifaki hii ni kuhakikisha unawekwa mfumo rasmi na wapamoja wa usimamizi endelevu wa mazingira katika ukanda wa SADC ukizingatia kuwa, masuala ya mazingira ni mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa, baada ya kuridhia Itifaki hii, Nchi Wanachama wa SADC zitakuwa na fursa ya kushirikiana katika usimamizi wa pamoja wa rasilimali zinazovuka mipaka. Katika Ukanda wa SADC rasilimali zinazovuka mipaka ya nchi moja kwenda nchi nyingine ni pamoja na: Bahari ya Hindi; ziwa Tanganyika; ziwa Nyasa; mto Zambezi; mto Ruvuma; mto Save/Sabi; mto Umbeluzi; mto Songwe; mto Congo; mto Limpopo; mto Orange; bwawa la Kariba; jangwa la Kalahari na msitu wa Congo. ***Kila nchi ina wajibu wa kusimamia na kuhifadhi rasilimali zake kwa mujibu wa Itifaki hii***.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa, utekelezaji wa Itifaki hii haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Sema kwa lengo la kutekeleza masharti ya Itifaki hii ipasavyo tunahitaji kuandaa Kanuni na

Miongozo chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ili kwenda sambamba na makubaliano ya Itifaki hii.

Aidha, Kamati ilijiridhisha juu ya faida zitakazopatikana kutokana na kuridhia Itifaki hii, faida hizo ni pamoja na:-

i) Kuongeza uwezo wa Nchi wa kukabiliana na changamoto za mazingira zinazovuka mipaka ya Nchi;

ii) Kuimarisha usimamizi wa pamoja wa maliasili zinazovuka mipaka ya nchi;

iii) Kuchangia ustawi wa hali ya uchumi na maisha ya jamii; na

iv) Kuchangia kuimarika kwa amani na usalama kati ya Nchi yetu na Nchi wanachama majirani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha pia kuhusu maudhui ya Itifaki ya SADC kwa kupitia vifungu vya mkataba huo. Baadhi ya vifungu muhimu katika Itifaki hii ni pamoja na **Ibara ya 13 kipengele cha 1-19** kimefafanua utekelezaji wa Itifaki hii ambapo imeweka wajibu wa nchi wanachama kutekeleza Itifaki ya SADC, kwenye mambo yanayohusu rasilimali zinazovuka mipaka. Nchi wanachama watashirikiana kuhakikisha malengo ya Itifaki hiyo yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 15 – Kipengele cha (1 – 11) imeweka Usimamizi wa Kisheria, Imeweka wajibu kwa nchi wanachama kuchukua hatua za makusudi za kuweka sheria mbalimbali za usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha malengo ya itifaki hiyo yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Ibara ya 19 kipengele cha 1 – 8, imeweka wajibu wa nchi wanachama kushirikiana katika kuanzisha miradi na program za pamoja katika kufanya utafiti katika masuala yahusuyo maliasili ikijumuisha bahari zilizopo katika eneo la nchi wanachama, bahari kuu, mabadiliko ya Tabianchi, mazingira

yavukayo mipaka na kutilia mkazo matatizo ya jumla ya kisayanzi katika Ukanda wa SADC.

Ibara ya 20, kipengele cha 1 – 6, imeweka wajibu kwa nchi wanachama kuzingatia masuala ya jinsia katika utekelezaji wa itifaki hii, ambapo program, sera, miradi pamoja na bajeti za utekelezaji wa Itifaki hii zinazingatia masuala ya jinsia.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, **kwa kuwa** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(The Treaty for the Establishment of the Southern African Development Community)* wa 1992 pamoja na baadhi ya Itifaki zake, na

Kwa kuwa, Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa SADC na inalenga kuweka nguvu za pamoja katika kusimamia na kuhifadhi mazingira na matumizi endelevu ya maliasili zinazovuka mipaka ya nchi moja kwenda nyingine; Kuhamasisha matumizi sahihi na endelevu ya maliasili kwa faida ya kizazi cha sasa na baadaye; na Kuimarisha usimamizi thabiti wa kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, na

Kwa kuwa, sote kunakubaliana kuwa masuala ya Mazingira ni Mtambuka na hayazingatii mipaka ya kijiografia wala ya kisiasa, inahitajika ushirikiano na jitihada za pamoja baina ya Nchi Wanachama katika kukabiliana na changamoto zilizopo na hatimaye kuweka usimamizi utakaopelekea matumizi endelevu ya rasilimali zetu na kuleta maendeleo Endelevu katika Ukanda wa *SADC.*

Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu

ili kuunganisha nguvu na wanachama wenzetu wa SADC katika kuleta mwamko wa uzingatiaji wa dhana ya usimamizi endelevu wa mazingira kwa wananchi wa ukanda wa SADC wakati wa kuendesha shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo kuimarisha uhifadhi wa mazingira.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Mussa Ramadhani Sima (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

1. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe

11. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb Mjumbe
12. Mhe. Zainab Mndolwa Amiri, Mb Mjumbe
13. Mhe. Machano Othman Said, Mb Mjumbe
14. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb Mjumbe
15. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb Mjumbe
16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb Mjumbe
17. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb Mjumbe
18. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb Mjumbe
19. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb Mjumbe
20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb Mjumbe
21. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb Mjumbe
22. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb Mjumbe
23. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani, Msahauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria Ndg. Seraphine Tamba pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA

13 Novemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Ntimizi. Tunakuja upande wa Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YAKUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Marekebisho ya Kigali ya kupunguza Uzalishaji wa Matumizi ya Kemikali ya Jamii ya *Hydrofluocarbons (HFCs)* chini ya Itifaki ya *Montreal* inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) na (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, Hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Marekebisho ya Kigali, Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya *Hydrofluocarbons (HFCs)* chini ya Itifaki ya *Montreal* inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni iliwasilishwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge lako Tukufu kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya *Montreal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Mkataba wa *Vienna* 1988, unaohusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa lengo la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na kumong'onyoka kwa Tabaka la Ozoni ambalo huzuia mionzi ya urujuani *(Ultraviolet-B radiation)* kutoka kwenye jua isifike duniani. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 1993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Itifaki ya Marekebisho ya Kigali ni tafiti za wanasayansi ambazo zinaendelea kufanyika na kuibua kemikali mbalimbali ambazo zinamong'onyoa tabaka la ozoni au kuwa na athari nyingine za kimazingira kama kusababisha ongekezo la joto-gesi duniani. Tafiti hizi zimekuwa zikifanyika chini ya Itifaki ya *Montreal* na mpaka sasa tafiti hizo zimeibua kemikali

mbalimbali ambazo zimepelekea kufanyika kwa marekebisho sita chini ya Itifaki ya *Montreal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya marekebisho sita yaliyofanyika chini ya Itifaki ya *Montreal,* Tanzania imesharidhia marekebisho matano na sasa ndiyo tupo katika mchakato wa kuridhia marekebisho ya sita ambayo ndiyo haya Marekebisho ya Kigali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo ya Kuridhia Itifaki hiyo. Maelezo hayo yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), yakifafanua nia ya Serikali kutaka kuridhia itifaki hii. Kamati ilipokea uchambuzi wa Sekretarieti ya Kamati juu ya dhana ya Itifaki pamoja na vipengele vya kisheria katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu uliwasadia Wajumbe wa Kamati kupata uelewa na kuwaweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii. Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) iliwapitisha Wajumbe Semina ya kujenga uelewa katika itifaki husika. Semina hii iliiwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati hii ni pamoja na madhumuni na maudhui ya Itifaki, faida za kuridhia Itifaki na hasara kama nchi haitaridhia Itifaki hii. Kamati ilijiridhisha pia kuwa utekelezaji wa Itifaki hii haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Marekebisho ya Kigali ni kuweka mfumo wa kisheria katika kuzisimamia nchi wanachama wa Itifaki ya *Montreal,* kushirikiana na kuchukua hatua za pamoja za kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya *HFCs.* Pia, Itifaki inadhamiria kuzisimamia nchi wanachama kutumia kipindi cha mpito, yaani kuanzia 2019 hadi 2047 kuhakikisha zinapunguza matumizi ya Kemikali ya *HFCs* kwa asilimia 80 na kutumia kipindi hicho kutafuta kemikali mbadala wa *HFCs* ambayo itakuwa ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Marekebisho ya Kigali imegawanyika katika ibara kuu tano. Ibara ya 1 inaelezea vifungu vinavyofanyiwa marekebisho; Ibara ya 2 inaeleza Uhusiano wa Itifaki ya Marekebisho na Mkataba ya Beijing 1999; Ibara ya 3 inaelezea Uhusiano wa Itifaki ya Marekebisho na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na Itifaki ya *Kyoto;* Ibara ya 4 inaelezea kuanza Utekelezaji wa Itifaki; na Ibara ya 5 inaelezea masharti ya nchi mwanachama kujitoa katika Itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, faida zinazotarajia kupatikana baada ya nchi kuridhia Itifaki hiyo ya Marekebisho, ni kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara zinazotarajiwa kupatikana kwa kutoridhia Itifaki hii zinazoonekana wazi kupitia kusoma Itifaki hii, ni nchi kuzikosa fursa na faida zote zilizoambatana na Itifaki hii. Pia, kama tunavyotambua teknolojia yetu bado ni duni na kemikali za jamii ya *HFCs* haizalishwi hapa nchini, tunategemea kuingiza kutoka nje. Hivyo basi, kama hatutaridhia tunaenda kukumbana na changamoto ya kushindwa kuinunua kutoka katika nchi zilizopo katika Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilichambua vifungu vya Itifaki na marekebisho ya baadhi ya vifungu muhimu pamoja na Ibara ya 2 aya ya 5 ambayo imetambulisha *Article* mpya ya *2(j)*. Ibara hii imeweka wajibu wa Nchi Wanachama kupunguza uzalishaji au matumizi ya kemikali ya jamii ya *Hydrofluorocarbons.* Ili kutekeleza hilo, ibara imeweka wajibu wa Nchi Wanachama kufanya vipimo na kutambua kiasi cha matumizi ya kemikali zenye madhara...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lipeleke kwenye maoni na ushauri wa Kamati, hayo yote tunayo.

MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YAKUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni Mwanachama wa Mkataba wa *Vienna* wenye lengo la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na shughuli za kibinadamu zinazosababishwa kumong'onyoka kwa Tabaka la Hewa ya Ozoni na Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya *Montreal.* Ni sehemu ya Utekelezaji wa Mkataba wa *Vienna;*

NA KWA KUWA, Itifaki ya *Montreal* imetambua athari zinazotokana na matumizi ya kemikali mbalimbali ikiwepo kemikali za jamii ya *Hyrofluorocarbons;*

NA KWA KUWA, lengo kuu la Itifaki ya Marekebisho ya Kigali ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia uwajibikaji wa Nchi Wanachama katika kupambana na kemikali zinazoendelea kumong'onyoa Tabaka la Ozoni;

NA KWA KUWA, sisi sote ni mashuhuda wa athari za kimazingira zinazotokana Mabadiliko ya Tabianchi yanayosababishwa na ongezeko la gesi-joto duniani, linalosababishwa na vyanzo mbalimbali ikiwemo uzalishaji na

matumizi ya kemikali za *HFCs* na hivyo kuathiri Tabaka la Ozoni na kupunguza uwezo wake wa kuzuia miale ya urujuani;

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bunge kuridhia Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia matakwa ya Ibara ya 4 aya ya pili. Ibara hii inaitaka nchi mwanachama kuanzisha na kusimamia mfumo wa kutoa leseni kwa waagizaji wa vifaa vinavyotumia kemikali ya jamii ya *HFCs.* Aidha, usimamizi huu utasaidia kutambua viwango vya *HFCs* inayoenda kuzalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Namshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ramadhani Sima, Makatibu Wakuu, pamoja na wataalam wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano wao walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama ilivyoonyeshwa hapo chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Michael Chikokoto; Makatibu Bi Zainabu Mkamba na Bi Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio. *(Makofi)*

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU MAREKEBISHO YA KIGALI YA KUPUNGUZA UZALISHAJI NA MATUMIZI YA KEMIKALI JAMII YA HYDROFLUOCARBONS (HFCS) CHINI YA ITIFAKI YA MONTREAL INAYOHUSU KEMIKALI ZINAZOMONG'ONYOA TABAKA LA OZONI *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances)* - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 **UTANGULIZI**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) na (4) ikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016, hoja ya Serikali kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu kemikali zinazomong'onyoa Tabaka La Ozoni *(Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances)* ililetwa mbele ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ajili ya kulipitia, kulichambua na hatimaye kulishauri Bunge lako tukufu kuliridhia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal.

Mheshimiwa Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi Mwanachama wa Mkataba wa Viena 1988, unaohusu Hifadhi ya Tabaka la Ozoni kwa lengo la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na kumong'onyoka kwa Tabaka la Ozoni ambalo huzuia mionzi

ya urujuani *(Ultraviolet-B radiation)* kutoka kwenye jua isifike duniani. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 1993.

2.0 CHIMBUKO LA ITIFAKI YA MAREKEBISHO

Mheshimiwa Spika, Chimbuko la Itifaki ya Marekebisho ya Kigali ni tafiti za wanasayansi ambazo zinaendelea kufanyika na kuibua kemikali mbalimbali ambazo zinamong'onyoa tabaka la ozoni au kuwa na athari zingine za kimazingira kama kusababisha ongekezo la joto-gesi duniani. Tafiti hizi zimekuwa zikifanyika chini ya Itifaki ya Montreal na mpaka sasa tafiti hizo zimeibua kemikali mbalimbali ambazo zimepelekea kufanyika kwa marekebisho sita (6) chini ya Itifaki ya Montreal.

Kati ya marekebisho sita (6) yaliyofanyika chini ya Itifaki ya Montreal Tanzania imekwisharidhia marekebisho matano (5) na sasa ndio tupo katika mchakato wa kuridhia marekebisho ya sita (6) ambayo ndio haya Marekebisho ya Kigali.

3.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Itifaki hii:-

i) Tarehe 6 Novemba, 2019 Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Itifaki hiyo, maelezo hayo yaliyowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuridhia itifaki hii;

ii) Tarehe 7 Novemba, 2019, Kamati ilipokea Uchambuzi wa Sekretarieti ya Kamati juu ya Dhana ya Itifaki pamoja na vipengele vya Kisheria katika Itifaki hii, Uchambuzi huu uliwasadia wajumbe kupata uelewa na kuwaweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii; na

iii) Tarehe 9 Novemba, 2019, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira iliwapitisha wajumbe Semina ya kujenga uelewa katika itifaki husika. Semina hii iliiwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake.

4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Mambo muhimu yaliyozingatiwa na Kamati ni pamoja na madhumuni na maudhui ya Itifaki, faida za kuridhia Itifaki hii na hasara kama nchi haitaridhia Itifaki hii. Kamati ilijiridhisha pia kuwa utekelezaji wa Itifaki hii haukinzani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria za nchi zinazohusiana na usimamizi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Marekebisho ya Kigali ni kuweka mfumo wa kisheria katika kuzisimamia nchi wanachama wa Itifaki ya Montreal kushirikiana na kuchukua hatua za pamoja za kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya HFCs. Pia, itifaki inadhamiria kuzisimamia nchi wanachama kutumia kipindi cha mpito yaani kuanzia 2019 hadi 2047 kuhakikisha zinapunguza matumizi ya Kemikali ya HFCs kwa asilimia Themanini (80) na kutumia kipindi hicho kutafuta kemikali mbadala wa HFCs ambayo itakuwa ni rafiki wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Itifaki ya Marekebisho ya Kigali imegawanyika katika ibara kuu Tano yani Ibara I – V. **Ibara ya I** inaelezea vifungu vilivyofanyiwa marekebisho; **Ibara ya II** inaeleza Uhusiano wa Itifaki ya Marekebisho na Mkataba ya Beijing 1999; **Ibara ya III** inaelezea Uhusiano wa Itifaki ya Marekebisho na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi pamoja na Itifaki ya Kyoto; **Ibara ya IV** inaelezea kuanza Utekelezaji wa Itifaki; na

Ibara ya V imeelezea masharti ya Nchi mwanachama Kujitoa katika Itifaki.

Aidha, faida zinazotarajia kupatikana baada ya Nchi kuridhia Itifaki hii ya Marekebisho ni pamoja na:-

(i) Kuchangia kupungua kwa athari za mabadiliko ya tabianchi kutokana na kupungua kwa uzalishaji na matumizi ya kemikali za HFCs ambazo huchangia ongezeko la joto duniani;

(ii) Kuongezeka kwa fursa ya upatikanaji wa rasilimali fedha, teknolojia mbadala na kujengewa uwezo wa kitaalam katika kutekeleza Marekebisho ya Kigali; na

(iii) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na Jumuiya ya kimataifa utokanao na utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali.

Mheshimiwa Spika, hasara za zinazotazamiwa kupatikana kwa kutoridhia Itifaki hii zinazoonekana wazi kupitia kusoma Itifaki hii ni Nchi kuzikosa fursa na faida zote zilizoambatana na Itifaki hii. Lakini pia, kama tunavyotambua teknolojia yetu bado ni duni na kemikali jamii ya HFCs haizalishwi hapa nchini tunategemea kuingiza kutoka nje, hivyo basi kama hatutaridhia tunaenda kukumbana na changamoto ya kushindwa kuinunua kutoka katika nchi zilizopo chini ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, kamati pia ilichambua vifungu vya Itifaki ya marekebisho na baadhi ya vifungu muhimu ni pamoja na **Ibara ya 2 aya ya 5** ambayo imetambulisha *Article* mpya yani ***Article 2J***. Ibara hii imeweka wajibu kwa Nchi wanachama kupunguza uzalishaji au matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons. Ili kutekeleza hilo ibara imeweka wajibu wa nchi wanachama kufanya vipimo na kutambua kiasi cha matumizi ya kemikali zenye madhara kwa Tabaka la Ozoni kwa lengo la kuhakikisha hewa ya matumizi hayazidi viwango vilivyoainisha katika ibara hii.

Utekelezaji wa Ibara hii utasaidia kutambua na kudhibiti ongezeko la kiwango cha uharibifu wa Tabaka la Ozoni unaosababishwa na kemikali zote chini ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 10(1) ya Itifaki ya Marekebisho ya Kigali inatoa fursa kwa nchi zinazoendelea ikiwepo Tanzania kupata misaada ya kitaalamu, kiteknolojia na kifedha kwa ajili ya kutekeleza makubaliano ya Itifaki ya Kigali. Hii ni moja ya faida ambayo tunaweza ipata kupitia kuridhia Itifaki hii kwani itatujengea uwezo kama nchi wa kushirikiana na wenzetu katika kupambana na ongezeko la kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilijiridhisha juu ya hatua iliyofikia katika utekelezaji wa Itifaki ya Marekebisho ya Kigali ambapo ilibaini kuwa ulianza rasmi tarehe 8 Januari, 2019, na hii ni kwa mujibu wa **Ibara ya IV**, ambapo Nchi Wanachama zilikubaliana utekelezaji uanze tarehe 1 Januari, 2019 endapo nchi wanachama Ishirini zitakuwa zimeridhia au ndani ya siku Tisini tokea mwanachama wa Ishirini kuridhia.

Aidha, Kwa mujibu wa takwimu za Jumuiya hadi kufikia Oktoba, 2019, jumla ya Nchi Wanachama 85 kati ya Nchi 197 zilikuwa zimesaini itifaki hii zikiwemo nchi mbili za Afrika Mashariki ambazo ni Rwanda na Uganda.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, **kwa kuwa,** Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Vienna wenye lengo la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na shughuli za kibinadamu zinazosababisha kumong'onyoka kwa Tabaka la Hewa ya Ozoni, na Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal ni sehemu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Viena, na

Kwa kuwa, Itifaki ya Montreal imetambua athari zinazotokana na matumizi ya kemikali mbalimbali ikiwepo kemikali jamii ya *Hyrofluorocarbons,* na

Kwa kuwa, lengo kuu la Itifaki ya marekebisho ya Kigali ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia uwajibikaji wa Nchi wanachama katika kupambana na kemikali zinazoendelea kumong'onyoa Tabaka la Ozoni, na

Kwa kuwa, sisi sote ni mashuhuda wa athari za kimazingira zinazotokana Mabadiliko ya Tabianchi yanayosababishwa na ongezeko la gesi-joto duniani linalosababishwa na vyanzo mbalimbali ikiwemo uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya HFCs na hivyo kuathiri Tabaka la Ozoni na kupunguza uwezo wake wa kuzuia miale ya jua kurudi ardhini.

Hivyo basi, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Kigali chini ya Itifaki ya Montreal ili kuungana na Jumuiya ya Kimataifa katika utekelezaji wake wenye lengo kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya HFCs na kupambana na uharibifu wa Tabaka la Ozoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bunge kuridhia Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia matakwa ya **Ibara ya 4B aya ya 2**, Ibara hii inaitaka nchi mwanachama kuanzisha na kusimamia mfumo wa kutoa leseni kwa waagizaji wa vifaa vinavyotumia kemikali jamii ya HFCs. Aidha, usimamizi huu utasaidia kutambua viwango vya HFCs inayoenda kuzalisha.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe.

George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Mussa Ramadhani Sima (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Azimio hili mbele ya Bunge lako tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

1. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Zainab Mndolwa Amiri, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
21. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Idara

ya Kamati Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA
13 Novemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kuwasilisha vizuri. Kambi ya Upinzani, nani? Tunaanza na nani? Mmejipangaje hapo? Yote mawili ni wewe mmoja? *SADC* au? Mnanilia muda wangu. Sasa mwende *straight* kwenye maoni yenu, hii *background* yote tunayo, ndiyo maana Serikali imekuja imewavuta kuwaelezea ni nini.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya Maendeleo Endelevu *(The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuathiri tafsiri na maana ya neno mazingira kama ilivyotolewa na wana taaluma mbalimbali, Kambi Rasmi ya Upinzani inachukulia mazingira kama kitovu cha maisha ya binadamu. Kama uhalisia ndio huo hatuna budi kuyatunza na kuyalinda mazingira yetu kwa kuwa mazingira hayo ndiyo maisha yetu. Kwa kuwa mazingira hayana mipaka kama ilivyo mipaka ya nchi na nchi ni dhahiri kwamba hata athari zinazotokana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira haziwezi kuwa na mipaka. Kama ilivyo vigumu

kuzuia hewa, mito, ardhi na uoto kubaki katika mipaka ya nchi fulani peke ndivyo ilivyo vigumu kuzuia athari zitokanazo na uharibifu na uchafuzi wa mazingira kama vile joto, ukame, mafuriko na kadhalika kusambaa na kuvuka mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo mapambani dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira na mapambano dhidi ya athari zotokanazo na uharibifu na uchafuzi huo yatakuwa na tija tu pale ambapo kuna nguvu na juhudi za pamoja za kimataifa katika kukabiliana na athari hizo. Ni katika muktadha huo ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona mantiki ya kuridhia itifaki hii kwa kuwa itaongeza nguvu ya usimamizi wa mazingira na hivyo kupunguza au kuthibiti kabisa athari za kimazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala ya Msingi Kabla ya Kuridhia Itifaki. Pamoja na ukweli kwamba itifaki hii ina mtazamo chanya kuhusu usimamizi wa mazingira kwa maendeleo endelevu kwa nchi washirika watakaoridhia itifaki hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuishauri Serikali na Bunge kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuridhia itifaki hiyo.

(i) Uwezo wa kitaifa wa kudhibiti uchafuzi wa hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya Tano ya itifaki hii inaeleza kwamba nchi wanachama watatakiwa kuchukua hatua ya kusimamia na kudhibiti madhara yatokanayo na uchafuzi wa hewa ambapo kimsingi yanavuka mipaka ya nchi zao kwenda nchi nyingine. Hatua hizo ni pamoja na kujenga uwezo wa kitaifa wa kuanzisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa ubora wa hewa *(Air Quality Monitoring Systems)*, kusimamia na kudhibiti uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na shughuli mbalimbali kama vile usafirishaji, uzalishaji wa umeme pamoja na maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kulieleza Bunge hili kuwa imejengwa uwezo wa Kitaifa kwa kiwango gani kwa kuweza kusimamia na

kudhibiti uzalishaji wa usambazaji wa hewa chafu zinazozalishwa viwandani na maeneo mengine ambako kwa asili yake huathiri ubora wa hewa katika anga la nchi yetu na nchi nyingine.

(ii) Uwezo wa Kitaifa Kudhibiti Taka Sumu na Usimamizi wa Kemikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya Sita na ya Saba ya itifaki hii inazitaka nchi wanachama kujenga uwezo wa kitaifa wa kudhibiti taka sumu na pia usimamizi bora wa kemikali zisilete madhara katika mazingira. Pamoja na malengo mazuri ya Ibara hizi yapo mashaka ya uwezo wetu kama Taifa ya kudhibiti taka sumu na kemikali ambazo huathiri mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matukio ya wananchi wetu kudhurika na matumizi ya kemikali kama vile Zebaki na Sanaidi hususani katika shughuli za machimbo katika migodi ya madini ya dhahabu ambapo kemikali hizo hutiririka kwenye maji ya mito na hivyo kuathiri afya za viumbe hai akiwemo binadamu. Jambo hili lilitokea katika maeneo yanayopakana na migodi ya dhahabu Nyamongo na mpaka leo Serikali haijatoa taarifa kuhusu athari hizo na imezidhibiti kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imeibua jambo hili ili liwe kipimo cha uwezo wa nchi yetu kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na matumizi ya kemikali zenye sumu katika shughuli za kiuchumi kabla ya kuingia kwenye mikataba mikuwa ya kimataifa kama itifaki hii huku tukijua uwezo wetu ni mdogo. Kwasababu hiyo tunaitaka Serikali ilieleze Bunge, Serikali imejenga uwezo wa Kitaifa kwa kiwango gani wa kudhibiti taka sumu na kemikali ambazo zina madhara makubwa katika mazingira yetu na afya za watu wetu kabla ya kuridhia itifaki hii.

(iii) Utayari na uwezo wa kufanya biashara na uwekezaji ndani ya nchi washirika wa itifaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18 ya itifaki inaeleza kwa ujumla kwamba nchi ya washirika wa itifaki watatakiwa kukuza biashara na uwekezaji endelevu miongoni mwao kwa kuzingatia athari za kimazingira zinazoweza kutokana na biashara na uwekezaji huo.

Hata hivyo kifungu kidogo cha nne cha Ibara hiyo kimeweka msisitizo kwa nchi washirika kukuza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kushughulikia masuala ya uwekezaji katika program za mazingira, hususani kutengeneza sera na kufanya mageuzi ya kitaasisi na kisheria kwa ajili ya kujenga mazingira rafiki ya ubia kati ya Sekta binafsi na Sekta ya Umma *(Publican Private Partnership)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha kifungu hicho kinazitaka nchi washirika kutoa mafunzo na msaada wa kitaalam kwa ajili ya kujenga uwezo katika mshirikiano ya sekta binafsi na sekta ya umma na mwisho kutoa taarifa muhimu na miongozo ya namna bora ya kutekeleza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyefahamu kwamba Serikali iliwahi kuzuia wananchi wasiuze mahindi nchini Kenya na nchi nyingine majirani kwa sababu nyepesi ya kulinda akiba ya chakula nchini. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Aidha, hakuna asiyefahamu tukio la Serikali hii la kuchoma moto vifaranga vya mfanyabiashara mmoja aliyeingiza vifaranga vya kuku nchini kutoka Kenya. Hayo yote yaliitia doa Serikali hii kwa ubinafsi mkubwa wa kutotaka kufungua milango ya biashara huru miongoni mwa majirani zake. Kwa matukio hayo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni...

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKI: Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya ngapi?

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(a) na Kanuni ya 63.

MWENYEKITI: Mh! sawa kabisa.

NAIBU WAZIRI KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Mwenyekiti, msomaji anayesoma taarifa ni kwamba anatoa taarifa ambazo si sahihi. Si kweli kwamba kama nchi tumefunga mipaka na kuzuia kuuza mazao ya chakula nje kwa nchi wanachama ama nchi zinazotuzunguka.

Tunavyoongea sasa hivi kwa kipindi cha miezi mitatu wafanyabiashara wa Tanzania wameuza mahindi jumla ya tani 54,000 katika nchi ya Kenya, wameuza mchele tani 26,000 katika nchi ya Kenya, wameuza maharage tani 24,000 katika nchi ya Kenya. Pamoja na hayo katika nchi za Rwanda, Uganda, *DRC*, Burundi, Oman na Zambia tumeshatoa jumla ya vibali 156 vya kuruhusu kuuza mazao ya kilimo. Kwa hiyo nilikuwa naomba kuhusu utaratibu kwamba hii taarifa si sahihi ni kupotosha na ukweli ni kwamba kama Serikali hatujafunga mipaka kuzuia mazao ya chakula kwenda nje. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa, hili ni suala la utaratibu.

Mheshimiwa Naibu wa Kilimo amesimama kwenye *point of order* kupitia Kanuni alizozitaja ambazo ni sahihi. Ninakutaka wewe kama mwenye matamshi hayo una *option* mbili ya kwanza ya kutaka kuthibitiasha hayo ambayo umeyaandika humo ambayo Serikali inasema si kweli, lakini *option* ya pili ambayo ni ya kiungwana tu unafuta kauli yako katika eneo hilo ili uendeleee kuwasilisha taarifa yako kuhusiana na hilo. Unachukua *option* ipi; usifundishane hapa wewe ndiwe, semea hapo hapo.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU

WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, *I withdraw*. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, endeelea tunakutunzia muda wako.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni aina na tatizo na dhamira ya itifaki katika eneo hili la tafiti za kisayansi sipokuwa ina mashaka na uwezo wa utayari wetu kama taifa kushiriki katika program hizo. Hii ni kwa sababu eneo hili halijapewa kipaumbele kabisa hasa katika Serikali hii ya awamu ya tano. Kwa mfano kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/ 2017, 2020/2021 Serikali ilijiwekea kiwango cha kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa *(GDP)* kwa ajili ya shughuli za sayansi, teknolojia na ugunduzi. Hata hivyo Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiwekea utaratibu huo, kama Serikali ingefuata maelekezo ya mpango basi ingekuwa inatenga shilingi trilioni 1.98 kwa ajili ya shughuli za tafiti kutokana na Pato Ghafi la Taifa kuwa dola za Kimarekani 52.09 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 119.807.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume na maelekezo ya mpango huo fedha iliyotengwa kwa Tume ya sayansi na teknolojia *COSTECH* kwa ajili ya tafiti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 7.574, sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani. Kwa mwenendo huo itakuwa ni aibu kwa nchi yetu kushiriki katika *program* za pamoja kwa bajeti ndogo namna hiyo.

(iv) Mfumo wa usimamizi na usimamizi wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 ya itifaki inaelekeza nchi wanachama kushirikiana katika kutoa na

kusambaza na kubadilishana taarifa kwa ajili ya utekelezaji bora wa itifaki. Taarifa hizo zinahusu masuala mbalimbali ya mazingira kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mashaka kama Serikali inaweza kutekeleza maelekezo hayo kwa ufanisi ikiwa imetengenezewa mazingira magumu ya upatikanaji na usambazaji wa habari hapa nchini. Jambo la kwanza kuba lililowahi kufanywa na Serikali hii ya awamu ya tano mara tu baada ya kuingia madarakani ilikuwa ni kutunga sheria kandamizi za kudhibiti upatikanaji na usambazaji wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako ingia la pili tumalize azimio lile lingine maana unayo mawili.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE, LA KURIDHIA ITIFAKI YA SADC YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA AJILI YA MAENDELEO ENDELEVU (THE SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT COMMUNITY PROTOCOL, ON ENVIRONMENTAL MANAGEMENT FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT) - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c)

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika,bila kuathiri tafsiri na maana ya neno mazingira kama ilivyotolewa na wanataaluma mbalimbali; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayachukulia

mazingira kama kitovu cha maisha ya binadamu. Ni vigumu kufikiri kama maisha yanawezekana nje ya mazingira tuliyo nayo. Hii ni kwa sababu kila hitaji la msingi katika maisha ya binadamu lina uhusiano wa moja kwa moja na mazingira tunamoishi.

2. Mheshimiwa Spika, kama uhalisia ndio huo, hatuna budi kuyatunza na kuyalinda mazingira yetu kwa kuwa mazingira hayo ndiyo maisha yetu. Hata hivyo, kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu anazofanya katika mazingira yake kwa ajili ya kujitafutia maisha; mazingira yamekuwa mhanga mkubwa wa uharibifu, na uchafuzi unaosababishwa na shughuli hizo.

3. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mazingira hayana mipaka kama ilivyo mipaka ya nchi na nchi, ni dhahiri kwamba hata athari zinazotokana na uharibifu au uchafuzi wa mazingira haziwezi kuwa na mipaka. Kama ilivyo vigumu kuzuia hewa, mito, ardhi na uoto kubaki katika mipaka ya nchi fulani pekee, ndivyo ilivyo vigumu kuzuia athari zitokanazo na uharibifu na uchafuzi wa mazingira kama vile joto, ukame mafuriko na kadhalika kusambaa na kuvuka mipaka ya nchi.

4. Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, mapambano dhidi ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira; na mapambano dhidi ya athari zitokanazo na uharibifu na uchafuzi huo yatakuwa na tija tu pale ambapo kuna nguvu na juhudi za pamoja za kimataifa katika kukabiliana na athari hizo.

5. Mheshimiwa Spika, ni katika muktadha huo, ambapo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona mantiki ya kuridhia itifaki hii kwa kuwa itaongeza nguvu ya usimamizi wa mazingira na hivyo kupunguza au kudhibiti kabisa athari za kimazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi yetu.

B. MASUALA YA MSINGI YA KUZINGATIA KABLA YA KURIDHIA ITIFAKI

6. Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba itifaki hii ina mtazamo chanya kuhusu usimamizi wa mazingira kwa

maendeleo endelevu kwa nchi washirika watakaoridhia itifaki hii; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kuishauri Serikali na Bunge kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuridhia itifaki hii:-

i. Uwezo wa Kitaifa wa Kudhibiti Uchafuzi wa Hewa

7. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 5 ya itifaki hii inaeleza kwamba; nchi wanachama watatakiwa kuchukua hatua ya kusimamia na kudhibiti madhara yatokanayo na uchafuzi wa hewa ambayo kimsingi yanavuka mipaka ya nchi zao kwenda nchi nyingine.

8. Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na kujenga uwezo wa kitaifa wa kuanzisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa ubora wa hewa (air quality monitoring systems); kusimamia na kudhibiti uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na shughuli mbalimbali kama vile usafirishaji, uzalishaji wa umeme, pamoja na maendeleo ya viwanda.

9. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili imejenga uwezo wa kitaifa kwa kiwango gani cha kuweza kusimamia na kudhibiti uzalishaji na usaambaji wa hewa chafuzi zinazozalishwa viwandani na maeneo mengine ambazo kwa asili yake huathiri ubora wa hewa katika anga la nchi yetu na nchi nyingine.

ii. Uwezo wa Kitaifa wa Kudhibiti Taka-Sumu na Usimamizi wa Kemikali

10. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 6 na ya 7 ya Itifaki hii zinazitaka nchi wanachama kujenga uwezo wa kitaifa wa kudhibiti taka-sumu na pia usimamizi bora wa kemikali zisilete madhara katika mazingira. Pamoja na malengo mazuri ya ibara hizi, yapo mashaka ya uwezo wetu kama taifa ya kudhibiti taka-sumu na kemikali ambazo huathiri mazingira yetu.

11. Mheshimiwa Spika, yapo matukio ya wananchi wetu kudhurika na matumizi ya kemikali kama vile Zebaki na Cyanide hususan katika shughuli za machimbo katika migodi

ya madini ya dhahabu ambapo kemikali hizo hutiririka kwenye maji ya mito na hivyo kuathiri afya za viumbe hai akiwemo binadamu. Jambo hili lilitokea katika maeneo yanayopakana na migodi ya dhahabu Nyamongo; na mpaka leo Serikali haijatoa taarifa kuhusu athari hizo na imezidhibiti kwa kiwango gani.

12. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeibua jambo hili ili liwe kipimo cha uwezo wa nchi yetu kudhibiti uchafuzi wa mazingira utokanao na matumizi ya kemikali zenye sumu katika shughuli za kiuchumi kabla ya kuingia kwenye mikataba mikubwa ya kimataifa kama itifaki hii huku tukijua uwezo wetu ni mdogo. Kwa sababu hiyo, tunaitaka Serikali ilieleze Bunge, Serikali imejenga uwezo wa kitaifa wa kiwango gani wa kudhibiti taka-sumu na kemikali ambazo zina madhara makubwa katika mazingira yetu na afya za watu wetu kabla ya kuridhia itifaki hii.

iii. Utayari na Uwezo wa Nchi Kufanya Biashara na Uwekezaji ndani ya Nchi Washirika wa Itifaki

13. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18 ya Itifaki inaeleza kwa ujumla kwamba; nchi washirika wa Itifaki watatakiwa kukuza biashara na uwekezaji endelevu miongoni mwao kwa kuzingatia athari za kimazingira zinazoweza kutokana na biashara na uwekezaji huo. Hata hivyo, kifungu kidogo cha nne (4) cha ibara hiyo, kimeweka msisitizo kwa nchi washirika kukuza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kushughulikia masuala ya uwekezaji katika programu za mazingira, hususan kutengeneza sera na kufanya mageuzi ya kitaasisi na kisheria kwa ajili ya kujenga mazingira rafiki ya ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma (PPP). Aidha, kifungu hicho kinazitaka nchi washirika kutoa mafunzo na msaada wa kitaalam kwa ajili ya kujenga uwezo katika mashirikiano ya sekta binafsi na sekta ya umma, na mwisho kutoa taarifa muhimu na miongozo ya namna bora ya kutekeleza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeona itoe maoni yake katika ibara hii kwa kuwa Tanzania imekuwa

na tabia tofauti hasa wakati huu wa Serikali ya Awamu ya Tano, ya kuweka vikwazo vingi vya ushirikiano wa kibiashara na majirani zake na pia imeiweka kando sekta binafsi katika kujenga uchumi wa Taifa.

15. Mheshimiwa Spika, hakuna asiyefahamu kwamba Serikali iliwahi kuzuia wananchi wasiuze mahindi nchini Kenya na nchi nyingine majirani kwa sababu nyepesi ya kulinda akiba ya chakula nchini. Aidha, hakuna asiyefahamu tukio la Serikali hii hii la kuchoma moto vifaranga vya mfanyabiashara mmoja aliyeingiza vifaranga vya kuku hapa nchini kutoka Kenya. Hayo yote yaliitia doa Serikali hii kwa ubinafsi mkubwa wa kutotaka kufungua milango ya biashara huru miongoni mwa majirani zake. Kwa matukio hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado ina mashaka kama Serikali hii iko tayari kufungua milango ya biashara huru na uwekezaji miongoni mwa nchi washirika wa Itifaki. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mashaka pia kama wafanyabiashara wa nchi yetu wanaweza kuwekeza katika nchi washirika wa Itifaki ukizingatia mazingira magumu ya kibiashara hapa nchini yatokanayo na ukata uliokithiri, mzunguko hafifu wa fedha, na upatikanaji duni wa mikopo na utekelezaji duni wa sera za fedha na mfumo wa kodi usiotabirika.

16. Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; wakati Itifaki hii inasisitiza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Serikali hii inaonekana kwenda kinyume kabisa na dhamira hiyo. Hii ni kwa sababu sekta binafsi hapa nchini imetengwa kabisa kushiriki katika ujenzi wa uchumi.

17. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata ujasiri wa kusema hivyo kwa sababu Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/2021) umeeleza bayana kwamba; miradi yote mikubwa ambayo kwa asili yake ni ya kibiashara itatekelezwa na sekta binafsi isipokuwa kama kuna sababu ya msingi ya kutofanya hivyo. Mpango unaeleza kwamba; naomba kunukuu ***"The working principle is that "commercially viable projects should be left***

to the private sector", unless there is strong justification for doing otherwise".[1]

18. Mheshimiwa Spika, tofauti na maelekezo hayo ya Mpango, Serikali hii ya Awamu ya Tano imekumbatia miradi yote mikubwa na kuitekeleza yenyewe na kuiweka kando sekta binafsi. Kwa mfano, utekelezaji wa miradi mikubwa kama vile Mradi wa wa Ujenzi wa Reli kwa kiwango cha Kimataifa (SGR), Mradi wa Umeme wa Stiegler's Gorge, Ununuzi wa Ndege na kadhalika ingetakiwa kutekelezwa na Sekta Binafsi kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, lakini Serikali imejichukulia tender zote hizo bila ushindani. Kwa mwenendo huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haioni utayari wa nchi yetu kutekeleza matakwa ya itifaki hii ikiwa imeshindwa kutekeleza masuala hayo hayo hapa nchini.

iv. Uwezo wa Nchi katika Eneo la Sayansi na Teknolojia

19. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 19 ya Itifaki hii inaeleza kuwa nchi washirika wa itifaki zitatakiwa kushirikiana katika kuanzisha programu za pamoja za utafiti katika maeneo mahsusi ambayo yana mwingiliano wa mipaka miongoni mwa nchi washirika wa Itifaki. Maeneo yanayopendekezwa na itifaki kufanyiwa tafiti za pamoja ni kama vile mali asili yakiwemo maeneo ya bahari ambayo yapo ndani ya eneo la nchi washirika, mabadiliko ya tabia nchi, masuala ya kimazingira ambayo yanavuka mipaka ya nchi ndani ya nchi washirika na changamoto nyingine za kisayansi ambazo ziko ndani ya eneo la nchi washirika wa Itifaki.

20. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina tatizo na dhamira ya Itifaki katika eneo hili la Tafiti za Kisayansi; isipokuwa ina mashaka na uwezo na utayari wetu kama Taifa kushiriki katika programu hizo. Hii ni kwa sababu eneo hili halijapewa kipaumbele kabisa hasa katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. Kwa mfano; kwa mujibu wa Mpango

[1] Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020.21) aya ya 5.3 (uk. 90)

[2] Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 (uk.17

wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, Serikali ilijiwekea kiwango cha kutenga asilimia moja (1%) ya pato ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya shughuli za Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi[2] . Hata hivyo, Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiwekea utaratibu huo. Kama Serikali ingefuata maelekezo ya Mpango, basi ingekuwa inatenga shilingi trilioni 1.98 kwa ajili ya shughuli za tafiti kutokana na pato ghafgi la Taifa kuwa Dola za Kimarekani 52.09 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 119.807.

21. Mheshimiwa Spika, kinyume na maelekezo ya mpango huo, fedha iliyotengwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH kwa ajili ya tafiti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 7.574 sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani, na kwa mwenendo huo, itakuwa ni aibu kwa nchi yetu kushiriki katika programu za pamoja kwa bajeti ndogo namna hiyo.

v. Mfumo wa Usimamizi na Usambazi wa Taarifa

22. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 21 ya Itifaki inazielekeza nchi wanachama kushirikiana katika kutoa na kusambaza na kubadilishana taarifa kwa ajili ya utekelezaji bora wa itifaki. Taarifa hizo zitahusu masuala mbalimbali ya mazingira kwa ujumla wake.

23. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

24. Mheshimiwa Spika, ikiwa matukio yote hayo ni kinyume na ibara ya 21 ya Itifaki hii, je, Serikali itakuwa tayari kufuta sheria hizo kandamizi, ili iendane na matakwa ya ibara ya 21 ya kutanua wigo wa upatikanaji na usambazaji wa habari miongoni mwa wadau hata kama habari hizo zinaelezea udhaifu wa Serikali katika kulinda na kutunza mazingira?

C. HITIMISHO

25. Mheshimiwa Spika, kimsingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haipingi Itifaki hii kutokana na umuhimu wake katika kulinda na kutunza mazingira ambayo ndiyo kitalu cha

maisha ya binadamu na viumbe hai vingine. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa maangalizo kadhaa ya kuzingatiwa na Serikali kabla Bunge halijaridhia Itifaki hii. Tumetoa maangalizo hayo, ili kuisaidia Serikali kujiweka vizuri kuhusu changamoto hizo ili isije ikaleta aibu wakati wa utekelezaji wa itifaki yenyewe.

26. Mheshimiwa Spika, Waingereza wana usemi kwamba, ***"Charity Begins At Home"*** ikiwa na maana kwamba Upendo Unaanzia Nyumbani. Tafsiri pana ya maneno hayo katika muktadha wa Itifaki hii ni kwamba, haiwezekani kuridhia itifaki inayohubiri habari za uhuru wa kupata, kubadilishana na kusambaza habari wakati huku nyumbani uhuru huo umefungwa tena kwa sheria; haiwezekani kuridhia itifaki inayoweka msisitizo katika kuchochea tafiti za kisayansi wakati huku nyumbani masuala ya tafiti sio kipaumbele cha Serikali. Hivyo ndivyo ilivyo na kwa masuala mengine yaliyoainishwa na itifaki hii.

27. Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaipa changamoto (challenge) Serikali hii ijipime kwanza kama inakidhi vigezo vya uwezo na viwango vya utekelezaji wa matakwa ya Itifaki hii na kulieleza Bunge juu ya uwezo na utayari wake kabla Bunge halijaridhia Itifaki hii.

28. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Latifah Chande (Mb)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA
13 Novemba, 2019

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo kabla hajahama katika hii *document* ambayo unafikiria kwamba iingie moja kwa moja nina sehemu ambayo nafikiria pengine ilikuwa inahitaji ...

MWENYEKITI: Umesimama kwa *point* gani, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1) katika *paragraph* yake ya 23 kuna maneno ambayo yamezungumzwa naona si ya ukweli. Kwa sababu katika *paragraph* hiyo inazungumzia kuna sheria zimetungwa ambazo katika mwendelezo wa *paragraph* hiyo inazungumzia kwamba sheria hizo zilienda sambamba na kuzuia *Television* ya Taifa kurusha moja kwa moja mijadala ya Bunge, kufungia magazeti mbalimbali kushambulia, kuteka na kuwauwa baadhi ya waandishi wa habari walioonekana kukosea Serikali. Kwa hiyo nilikuwa naona kwamba akiondoka wakati hilo eneo halijafanyiwa kazi itakuwa ina changamoto.

MWENYEKITI: Basi mimi naagiza *paragraph* hiyo isiwe sehemu ya wasilisho kuhusiana na azimio hili ambalo liko mbele ya Bunge. Kwahiyo tunaagiza watu wa *hansard* wataipitia vizuri eneo hilo isiwe sehemu ya wasilisho la Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haipo hiyo kitu anazungumza; hazipo.

MWENYEKITI: Sasa mimi nimeshatoa uamuzi kinachofuata mimi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Mbunge aje kwenye azimio la mwisho ambalo linahusu *Ozone layer* ili muda wako tumalize, maana kuna haya mawili. Karibu

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuweka *record clear* hili eneo analoliongelea hii *paragraph* haipo kwa sababu kuna maneno ambayo tayari yalishakuwa yamefutwa/yameondolewa. Sasa atuelekeze zaidi yeye *paragraph* gani anayoongelea kwa sababu ukiangalia *paragraph* 23 hayo maneno anayoyazungumza hayo aliyoyasoma *unless* kama yeye ana taarifa au ana *document* nyingine tofauti na tuliyonayo sisi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi ninazo hapa ambazo zimewasilishwa tusaidie ya kwako, Waheshimiwa hebu tusianze mabishano naomba sana; zima hicho kipaza sauti! Haya; Mheshimiwa Naibu Waziri *paragraph* namba ngapi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimesikia maelekezo yako lakini pia na wenyewe wamesema kwamba wamefuta kwa hiyo kama yalikuwa vitu vibaya amefuta.

MWENYEKITI: Basi nawashukuru sana Mheshimiwa endelea.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo

MWENYEKITI: Mwongozo hapa acha amalize huyu, kama nitakuwa na muda unaniruhusu nitakupa nafasi ya mwongozo.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nilikuwa naomba tu asiwe *interrupted* Mawaziri wana...

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha eneo lingine ambalo halijasomwa la hotuba yangu iliyopita. Naomba niingie kwenye azimio linalofuata ambalo linakuja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza Uzalishaji na Matumizi

ya Kemikali Jamii ya *Hydrofluorocarbons* chini ya Itifaki ya *Montreal* inahusu kemikali zinazomomonyoa tabaka la *ozone*, Kigali *amendment on phasing down hydro fluorocarbons to the Montreal protocol on ozone depleting substances)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la matumizi na uzalishaji wa kemikali jamii ya hapa duniani yameonesha kuwa na athari katika mazingira kutokana na kumomonyoka kwa tabaka la *ozone*. Uchafuzi unaotokana na kemikali hizo ni mkubwa mara kumi elfu ya uchafuzi unaotokana na hewa ukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho haya yanatokana na mkataba mama wa Vienna wa kuzuia au kulinda tabaka la Ozoni wa mwaka 1985 na baadae zikaja itifaki nyingine za marekebisho ya London (1990), kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya *Chlorofluocarbons*, Marekebisho ya *Copenhagen* (1992), kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali ya *Methylbromide*, *hydrofluorocarbons*, *Vienna* (1995) kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya *chlorofluocarbons* na marekebisho ya *Montreal* (1997); ambapo marekebisho yake yalifanyika kigali, rwanda oktoba, 2016. Marekebisho yote hayo yana lengo hilo hilo la kulinda tabaka la *ozone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vikuu vya uzalishaji wa kemikali hizi hatarishi ni vifaa vya matumizi ya majumbani vilivyo chakavu kama nilivyoeleza hapo awali ambavyo mosi, vimekosa maeneo mahususi ya kuviteketeza na pili vimekosa mifumo ya kudhibiti athari zake. Kwa sababu hiyo, marekebisho ya Itifaki hii yanalenga kupata takwimu za viwango vya ubora wa vifaa kama *freezers*, *refrigerators*, air-*conditioners*, *heat pumps*, *water-coolers*, *portable fire extinguishers*, *air conditioners* za magari na kadhalika kwa minajili ya kupunguza athari zake katika kuharibu tabaka la *Ozone*. (Tazama kiambatanisho D cha Mkataba huu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Ibara Zilizofanyiwa Marekebisho Katika Mkataba. Mkataba una jumla ya Ibara 20, lakini marekebisho ambayo

yanapendekezwa kuridhiwa yamefanywa kwenye ibara zifuatazo; 1, 2, 2J, 3, 4, 4B, 5, 6, 7, 10 na 17. Sambamba na marekebisho kwa Ibara hizo, pia viambatanisho A, C na F vimefanyiwa marejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika marekebisho yanayopendekezwa kwenye Ibara ya 2 aya ya 8 katika aya ndogo ya (a) kwamba;

"Any such agreement may be extended to include obligations respecting consumptions or production under article 2J provided that the total combined calculated level of consumption or production of the Parties does not exceed the levels required by article 2J".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa utekelezaji wa marekebisho hayo unaweza kuwa mgumu kwa mazingira ya nchi yetu hasa ukizingatia kwamba taasisi zetu za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingia bado hazina uwezo mkubwa wa kukabiliana na viwango. Uthibitisho wa jambo hili ni kupatikana kwa bidhaa nyingi bandia nchini ilhali taasisi hizo zipo. Aidha, hata kama taasisi hizi zikiwa na uwezo bado kuna mwanya wa rushwa kubwa ambapo taasisi za ndani zinaweza kukubaliana na makampuni makubwa ya uzalishaji kwa ahadi ya malipo ya fedha ili zifumbie macho suala la viwango vya bidhaa hizo vilivyowekwa kwenye marekebisho ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara mpya ya 2J inayowekwa baada ya Ibara ya 2(I) ambayo ni maalum na ndiyo inayobeba dhana nzima ya Marekebisho ya Kigali ya – *Hydrofluorocarbons* imegawanyika katika aya saba, kila moja ikiwa na viwango vya matumizi na uzalishaji wa hizo kemikali kwa makundi mbalimbali kulingana na Majedwali kwenye viambatanisho vya mkataba na kila kimoja kimepangiwa muda wake na asilimia kulingana na hewa ukaa inayohitajika kuzalishwa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina wasiwasi mkubwa kwa nchi yetu kuweza kutimiza masharti

hayo ya mkataba kutokana na ukweli kwamba sisi ni wapokeaji na tumeshajiweka katika mazingira hayo, na pia teknolojia ya kuweza kugundua vifaa husika na kiwango cha hewa ukaa kinachoruhusiwa kulingana na mwaka husika kama ilivyotolewa kwenye marekebisho ya mkataba bado hatujakuwa na uwezo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii mpya inahitaji umakini mkubwa kuitekeleza na pia taasisi zetu za udhibiti wa ubora wa bidhaa zinahitaji kuwa na teknolojia ya hali ya juu katika kuhakikisha kuwa utendaji kazi wake unakidhi viwango vya kimataifa. Hivyo basi, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhakikisha Serikali inaziwezesha taasisi zinazohusika na kuhakiki viwango vya ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje ili ziendane na matakwa ya Ibara hii mpya ya 2J.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye Ibara mpya ya 2J, vivyo hivyo kwenye Ibara ya 3 ni ukweli mahesabu yanaweza kuhusu hewa inayotolewa kutoka kwenye mitambo inayovujisha hewa hizo au pale bidhaa zitakapoharibiwa, lakini kupima viwango hivyo kulingana na mahitaji ya mkataba kwa mazingira ya nchi yetu Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa bado ipo changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(2) inafanyiwa marekebisho kwamba; *"upon entry into force of this paragraph, each Party shall ban the import of the controlled substances in Annex F 'from any State' not Party to this Protocol".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kifungu kingine cha marekebisho kinasema kwamba; '*upon entry into force of this paragraph, each Party shall ban the export of the controlled substances in Annex F 'to any State' not Party to this Protocol"*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo jema ili watu wote kuwa na uelewa wa pamoja, kwa Serikali kueleza Kundi hilo la kemikali kwenye *ANNEX F (controlled substances)* ambayo ni mpya haipo

kwenye Mkataba mama wa Montreal, hizo kemikali matumizi yake ni nini hasa au zinatumika kutengeneza nini kwa matumizi ya kila siku kwenye uzalishaji viwandani au majumbani au mahospitalini. Jambo hili litasaidia sana Wabunge kufanya kazi yao wakiwa na uelewa zaidi wa kile wanachokipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; hizi kemikali hatarishi zinazosababisha mmonyoko wa tabaka la *ozone (HFCs)* kwa kiwango kikubwa zinatokana na vifaa ambavyo ni chakavu. Kwani vifaa chakavu vina uwezo mkubwa wa kutoa hewa yenye kemikali hizo kwa wingi sana ukilinganisha na vifaa ambavyo si chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba kwa mustakabali mzuri wa nchi yetu kwa nyakati zijazo; ni lazima Serikali iwe na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba wananchi wake wana uwezo wa kununua bidhaa mpya ambazo hazijawahi kutumika mahali popote ili kuondokana na uzalishaji wa kemikali hizi hatarishi ambazo kwa mazingira ya nchi yetu, udhibiti wake ni mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la matumizi ya vifaa chakavu au mtumba ni matokeo ya nchi yetu kuwa na mfumo wa kodi ambao unakatisha tamaa watu kununua bidhaa mpya. Hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa; pamoja na kuziwezesha taasisi za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa ndani toka nje na zinazozalishwa ndani; pia mfumo wa kodi nao urekebishwe ili uwe rafiki kwa wafanyabiashara na wananchi kwa jumla na hivyo kuwapa motisha kununua bidhaa mpya badala ya zile zilizokwishatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa; ni jambo lisilokuwa na ubishi kwamba Itifaki hii inahusu masuala magumu ya kikemia ambayo Wabunge wengi hawana taaluma yake. Kuleta kwa ghafla mkataba au itifaki ya namna hii na kuwataka Wabunge waridhie jambo ambalo hawajapatiwa semina elimishi ya kuwajengea uelewa wa jambo hilo, si tu kunawakosesha Wabunge haki ya kushiriki

kikamilifu, lakini pia kunaiingiza nchi kwenye mambo ambayo kama Taifa hatujajiandaa nayo na hatuna uelewa wa pamoja wa mambo hayo jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali mwema wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA MAREKEBISHO YA KIGALI YA KUPUNGUZA UZALISHAJI NA MATUMIZI YA KEMIKALI JAMII YA HYDROFLUOROCARBONS (HFCs) CHINI YA ITIFAKI YA MONTREAL INAYOHUSU KEMIKALI ZINAZOMONG'ONYOA TABAKA LA OZONE (KIGALI AMENDMENT ON PHASING DOWN HYDROFLUOROCARBONS (HFCs) TO THE MONTREAL PROTOCOL ON OZONE DEPLETING SUBSTANCES) - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6)(c) ya Kanuni ya Bunge, Toleo la Mwaka 2016)"

A. UTANGULIZI:

1. Mheshimiwa Spika, ongezeko la matumizi na uzalishaji wa kemikali jamii ya HFCs hapa duniani yameonesha kuwa na athari katika mazingira kutokana na kumong'onyoka kwa tabaka la ozone. HFCs hizo zinatokana hasa na uvujaji wa kemikali kutoka katika vifaa husika ikiwemo majokofu, viyoyozi, vifaa vya kuzimia moto na mitambo ya viwandani.

2. Mheshimiwa Spika, uchafuzi unaotokana na kemikali hizo ni mkubwa mara kumi elfu ya uchafuzi unaotokana na hewa ukaa. Kwa mfano, inakadiriwa kuwa Kilogramu moja ya HFC ina athari takriban mara 10,000 ya Kilogramu moja ya hewa ukaa (CO_2) ambayo huchangia kuongezeka kwa joto la dunia. Ongezeko hilo la joto hatimaye husababisha mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa sasa yamekuwa na athari za wazi katika nchi yetu katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

3. Mheshimiwa Spika, marekebisho haya yanatokana na mkataba mama wa Vienna wa kuzuia au kulinda tabaka la Ozoni wa mwaka 1985 na baadae zikaja itifaki nyingine za marekebisho ya London (1990), kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Chlorofluocarbons (CFCs), Marekebisho ya Copenhagen (1992) kusitisha uzalishaji na matumizi ya kemikali ya Methylbromide, hydrofluorocarbons (HBFCs), Vienna (1995) kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Chlorofluocarbons (CFCs) na marekebisho ya Montreal (1997) ambayo marekebisho yake yalifanyika Kigali, Rwanda Oktoba, 2016. Marekebisho yote hayo yana lengo hilo hilo la kulinda tabaka la ozone.

4. Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya uzalishaji wa kemikali hizi hatarishi ni vifaa vya matumizi ya majumbani vilivyo chakavu kama nilivyoeleza hapo awali ambavyo mosi,vimekosa maeneo mahususi ya kuviteketeza na pili vimekosa mifumo ya kudhibiti athari zake. Kwa sababu hiyo, marekebisho ya Itifaki hii yanalenga kupata takwimu za viwango vya ubora wa vifaa kama freezers, refrigerators, air-conditioners, heat pumps, water-coolers, portable fire extinguishers, air conditioners za magari na kadhalika kwa minajili ya kupunguza athari zake katika kuharibu tabaka la Ozone. (Tazama kiambatanisho D cha Mkataba huu).

B. MAPITIO YA IBARA ZILIZOFANYIWA MAREKEBISHO KATIKA MKATABA

5. Mheshimiwa Spika, mkataba una jumla ya Ibara 20, lakini marekebisho ambayo yanapendekezwa kuridhiwa yamefanywa kwenye ibara zifuatazo; 1, 2, 2J, 3, 4, 4B, 5, 6, 7, 10 na 17 sambamba na marekebisho kwa Ibara hizo, pia viambatanisho A, C na F vimefanyiwa marejeo.

6. Mheshimiwa Spika, katika marekebisho yanayopendekezwa kwenye Ibara ya 2 aya ya 8 katika aya ndogo ya (a) kwamba;

"Any such agreement may be extended to include obligations respecting consumptions or production under

article 2J provided that the total combined calculated level of consumption or production of the Parties does not exceed the levels required by article 2J"

7. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa utekelezaji wa marekebisho hayo unaweza kuwa mgumu kwa mazingira ya nchi yetu hasa ukizingatia kwamba; taasisi zetu za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingia bado hazina uwezo mkubwa wa kukabiliana na viwango. Uthibitisho wa jambo hili ni kupatikana kwa bidhaa nyingi bandia nchini ilhali taasisi hizo zipo. Aidha, hata kama taasisi hizi zikiwa na uwezo bado kuna mwanya wa rushwa kubwa kubwa (grand corruption) ambapo taasisi za ndani zinaweza kukubaliana (compromising) na makampuni makubwa ya uzalishaji kwa ahadi ya malipo ya fedha ili zifumbie macho suala la viwango vya bidhaa hizo vilivyowekwa kwenye marekebisho ya mkataba.

8. Mheshimiwa Spika, Ibara mpya ya 2J inayowekwa baada ya Ibara ya 2(I) ambayo ni maalum na ndiyo inayobeba dhana nzima ya Marekebisho ya Kigali ya **- HYDROFLUOROCARBONS** imegawanyika katika aya 7, kila moja ikiwa na viwango vya matumizi na uzalishaji wa hizo kemikali kwa makundi mbalimbali kulingana na Majedwali kwenye viambatanisho vya mkataba na kila kimoja kimepangiwa muda wake na asilimia kulingana na hewa ukaa (CO_2 equivalents) inayohitajika kuzalishwa na kutumika.

9. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina wasiwasi mkubwa kwa nchi yetu kuweza kutimiza masharti hayo ya mkataba kutokana na ukweli kwamba sisi ni wapokeaji na tumeshajiweka katika mazingira hayo, na pia teknolojia ya kuweza kugundua vifaa husika na kiwango cha hewa ukaa kinachoruhusiwa kulingana na mwaka husika kama ilivyotolewa kwenye marekebisho ya mkataba bado hatujakuwa na uwezo huo.

10. Mheshimiwa Spika, Ibara hii mpya inahitaji umakini mkubwa kuitekeleza na pia taasisi zetu za udhibiti wa ubora wa bidhaa zinahitaji kuwa na teknolojia ya hali ya juu katika

kuhakikisha kuwa utendaji kazi wake unakidhi viwango vya kimataifa. Hivyo basi, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhakikisha Serikali inaziwezesha taasisi zinazohusika na kuhakiki viwango vya ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje ili ziendane na matakwa ya Ibara hii mpya ya 2J.

11. Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye Ibara mpya ya 2J, vivyo hivyo kwenye Ibara ya 3 ni ukweli mahesabu yanaweza kuhusu hewa inayotolewa kutoka kwenye mitambo inayovujisha hewa hizo au pale bidhaa zitakapoharibiwa, lakini kupima viwango hivyo kulingana na mahitaji ya mkataba kwa mazingira ya nchi yetu Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa bado ipo changamoto.

12. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuona kuwa uhalisia wa kile tunachokipitisha upo ili kiweze kusimamiwa na hivyo jambo hilo litakuwa na maana zaidi kuliko kupitisha kitu ambacho hakitekelezeki kwa hali halisi ya nchi yetu. Hapo tunakuwa tunajidanganya wenyewe na hiyo ni hatari sana katika kutengeneza Tanzania bora kwa vizazi vijavyo.

13. Mheshimiwa Spika, Ibara ya 4 kwenye aya ya 2 inafanyiwa marekebisho kwamba;

*"upon entry into force of this paragraph, each Party shall ban the **import** of the controlled substances in Annex F '**from any State'** not Party to this Protocol".*

Vile vile kifungu kingine cha marekebisho kinasema kwamba;

"*upon entry into force of this paragraph, each Party shall ban the **export** of the controlled substances in Annex F '**to any State'** not Party to this Protocol"*

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo jema ili watu wote kuwa na uelewa wa pamoja, kwa Serikali kueleza Kundi hilo la kemikali kwenye ANNEX F (controlled substances[1]) ambayo ni mpya haipo

[1] Marekebisho Makataba yaliyofanyika Kigali uk. 9

kwenye Mkataba mama wa Montreal, hizo kemikali matumizi yake ni nini hasa au zinatumika kutengeneza nini kwa matumizi ya kila siku kwenye uzalishaji viwandani au majumbani au mahospitalini. Jambo hili litasaidia sana Wabunge kufanya kazi yao wakiwa na uelewa zaidi wa kile wanachokipitisha.

C. HITIMISHO

15. Mheshimiwa Spika, hizi kemikali hatarishi zinazosababisha kumong'onyoka kwa tabaka la ozone (HFCs) kwa kiwango kikubwa zinatokana na vifaa ambavyo ni chakavu. Kwani vifaa chakavu vina uwezo mkubwa wa kutoa hewa yenye kemikali hizo kwa wingi sana ukilinganisha na vifaa ambavyo si chakavu.

16. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba kwa mustakabali mzuri wa nchi yetu kwa nyakati zijazo; ni lazima Serikali iwe na mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kwamba wananchi wake wana uwezo wa kununua bidhaa mpya ambazo hazijawahi kutumika mahali popote ili kuondokana na uzalishaji wa kemikali hizi hatarishi ambao kwa mazingira ya nchi yetu, udhibiti wake ni mgumu.

17. Mheshimiwa Spika, jambo hili la matumizi ya vifaa chakavu au mtumba ni matokeo ya nchi yetu kuwa na mfumo wa kodi ambao unakatisha tamaa watu kununua bidhaa mpya. Hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa; pamoja na kuziwezesha taasisi za kudhibiti ubora wa bidhaa zinazoingizwa ndani toka nje na zinazozalishwa ndani; pia mfumo wa kodi nao urekebishwe ili uwe rafiki kwa wafanyabiashara na wananchi kwa jumla na hivyo kuwapa motisha kununua bidhaa mpya badala ya zile zilizokwishatumika.

18. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa; ni jambo lisilokuwa na ubishi kwamba Itifaki hii inahusu masuala magumu ya kikemia ambayo Wabunge wengi hawana taaluma yake. Kuleta kwa ghafla mkataba au itifaki ya namna hii na kuwataka Wabunge waridhie jambo ambalo hawajapatiwa

semina elimishi ya kuwajengea uelewa wa jambo hilo, si tu kunawakosesha Wabunge haki ya kushiriki kikamilifu, lakini pia kunaiingiza nchi kwenye mambo ambayo kama taifa hatujajiandaa nayo na hatuna uelewa wa pamoja wa mambo hayo jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali mwema wa Taifa letu.

19. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

.....
Latifah Chande (Mb)
MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA
13 Novemba, 2019

MWENYEKITI: Tunashukuru sana.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu, Kanuni ya 64(1); kufuatialia maelezo aliyesema Mheshimiwa Bashe ndani ya Bunge hili, ukiangalia maelezo aliyezungumza Mheshimiwa Msemaji wetu amezungumzia ile Ibara ya 15 na akisema kwamba Serikali iliwahi kuzuia mazao yetu kwenda nje na hii ni kweli iliwahi kutokea, siyo sasa, iliwahi kutokea. Kwa hiyo, nadhani maneno yaliyoko kwenye hotuba yetu ni sahihi na hayapaswi kuondolewa kwa sababu ni kweli, kama nchi kuna wakati tulizuiwa kupeleka mazao nje hasa Kenya na ndiyo ameelezea. Kwa hiyo, nadhani maelezo hayo ni sahihi kabisa.

MWENYEKITI: Yameshaondolewa. Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Bashungwa, una dakika zisizozidi 15.

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(Protocol Ammending the Marrakesh Agreement establishing the World Trade Organization – WTO)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la Kuridhia Itifaki ya mwaka 2014 ya Marekebisho ya Mkataba wa Marakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(Protocol Ammending the Marrakesh Agreement establishing the World Trade Organization – WTO).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwa nafasi ya kipekee kabisa na kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa msukumo wa kipekee katika kuboresha na kuimarisha mazingira bora na wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini, msukumo huo ni chachu muhimu katika kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda ambayo ni ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Biashara la Dunia *(World Trade Organization – WTO)* ni Shirika la Kimataifa lililoanzishwa tarehe 1 Januari 1995, ili kusimamia taratibu za kibiashara duniani. Shirika hilo kwa sasa lina jumla ya Nchi Wanachama 164 na Tanzania ni moja ya nchi wanachama waanzilishi. Lengo kuu la Shirika hilo, ni kuhakikisha kuwa Biashara ya Kimataifa inafanyika kwa uhuru kwa kufuata Sheria, Mikataba na Kanuni zinazojadiliwa na kukubalika na Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zilizofanywa na *WTO* kuhakikisha biashara inafanyika kwa wepesi, bado kuna changamoto za wingi wa ada na tozo *(multiple fees and charges),* kanunini nyingi za biashara ambazo zinasimamiwa na mamlaka tofauti na vikwazo visivyo vya lazima vya kiushuru na visivyo vya kiushuru ambavyo huongeza gharama za kufanya biashara duniani. Hivyo, ili kushughulikia changamoto hizo na kupunguza gharama za

kufanya biashara duniani, Nchi Wanachama wa *WTO* zilikubaliana kuwa na utaratibu wa kisheria wa Kimataifa unaojitegemea ulio wazi na mwepesi utakaotumika kama mwongozo. Hii ilizilazimu nchi hizo kuanza majadiliano ya kuanzishwa kwa mkataba wa Uwezeshaji Biashara *(Trade Facilitation Agrement-TFA)* mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mkataba huo kukamilika Nchi Wanachama wa *WTO* zilianza maandalizi ya Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(WTO)* ambayo ilikamilika mwaka 2014. Kulingana na kifungu cha 3 cha Ibara ya 10 ya Mkataba wa *WTO*, Itifaki hiyo ya Marekebisho ya Mkataba wa WTO, ilipaswa kuidhiwa na theluthi mbili ya Nchi Wanachama ili mkataba huo wa uwezeshaji biashara uweze kuwa sehemu rasmi ya Mkataba wa *WTO.* Mkataba huo wa wezeshaji biashara ulianza kutumika rasmi tarehe 22 Februari 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Ititaki ya Marekebisho ya Mkataba wa *WTO* kuridhiwa na Nchi Wanachama 112 kati ya wanachama 164 wa *WTO*. Hadi kufikia tarehe Mosi Oktoba, 2019, nchi wanachama 146 zilikuwa tayari zimekwisharidhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa *WTO*. Hii inamaanisha ni Nchi Wanachama 18 pekee, ikiwemo Tanzania ndio hazijaridhia mkataba huo hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hiyo ina vipengele muhimu vifuatavyo ambavyo nchi yetu imevizingatia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ibara Na.1 kwanza inayohusu uchapishaji na upatikanaji wa Taarifa *(Publication and Availability of Information)*; kuna Ibara na. 10(4) dirisha la pamoja la forodha la Huduma *(Electronic Single Window System)*; kuna Ibara Na. 11 inayohusu Uhuru wa upitishaji mizigo/bidhaa *(Freedom of Transit)*; kuna Ibara Na. 13, 14 na 19; inayohusu Maeneo ya Upendeleo kwa Nchi Changa na Zinazoendelea *(Special and Differential Treatment – S 7 DT)*;

kuna Ibara ya 23 inayohusu Muundo wa Kitaasisi yani *Institutional Arrangements.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba maelezo ambayo yako kwenye hizi Ibara yaingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa WTO wa uwezeshaji biashara unashabihiana kwa kiasi kikubwa na masuala ya uwekaji wa mazingira wezeshi na endelevu ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na mpango wa *blueprint* ambao Serikali inaendelea na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio husika.

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia *(World Trade Organization – WTO)* kupitia Hati iliyosainiwa na Serikali mnamo tarehe 22 Julai, 1994 na kuwasilishwa Sekretarieti ya Shirika hilo tarehe 6 Septemba, 1994;

NA KWA KUWA Mawaziri wa Biashara wa Nchi Wanachama kupitia kikao chao kilichofanyika Mjini Bali – Indonesia walikamilisha na kupitisha Mkataba wa Uwezeshaji Biashara *(Trade Facilitation Agreement)* mwaka 2013;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama wa *WTO* waliandaa Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(Protocol Ammending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization- WTO)*;

NA KWA KUWA Itifaki hiyo ililenga kuufanya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara *(Trade Facilitation Agreement – TFA)* kuwa sehemu rasmi *(integral part)* ya Mkataba wa uanzishwaji wa Shirika la Biashara la Dunia;

NA KWA KUWA Mkataba huo wa Uwezeshaji Biashara umekwishakuwa sehemu ya Mkataba wa Uanzishaji wa *WTO* toka tarehe 22 Februari, 2017 baada za Itifaki hiyo kuridhiwa na idadi ya theluthi mbili ya Nchi Wanachama;

NA KWA KUWA hadi tarehe 1 Oktoba 2019, Nchi Wanachama 146 kati ya wanachama 164 wa *WTO* zilikuwa zimeridhia Itifaki hiyo; ambapo ni Nchi Wanachama 18 pekee bado hazijaridhia Itifaki hiyo, ikiwemo Tanzania na Burundi kwa upande wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA Tanzania kama mwanachama wa *WTO* inapaswa kuridhia Itifaki hiyo ili kukidhi matakwa ya Itifaki husika na pia kuwezesha utekelezaji wa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara Nchini;

NA KWA KUWA Nchi Wanachama wa WTO zinatambua kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hiyo ni moja ya nyenzo muhimu katika kujenga mazingira wezeshi na rafiki ya kurahisisha ufanyaji biashara;

NA KWA KUWA Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia, pamoja na mambo mengine, unalenga:-

(a) Kuweka mfumo wa kisheria *(legal framework)* wa kimataifa ulio wazi na mwepesi utakaotumika kama mwongozo kwa Nchi Wanachama kwenye kutatua changamoto za ufanyaji biashara;

(b) Kuweka utaratibu wa pamoja *(harmonized procedures)* katika kushughulikia masuala ya uwezeshaji biashara;

(c) Kushughulikia masuala na changamoto zinazohusiana na biashara ili kupunguza gharama na ugumu wa ufanyaji biashara duniani;

(d) Kuwa na mfumo na utaratibu wa pamoja wa uratibu wa masuala hayo utakaowezesha kuweka taratibu

za ufanyaji biashara kuwa rahisi kwa kuondoa mwingiliano na hatimaye kuongezeka kwa biashara na ufanisi katika utendaji; na

(e) Kuhakikisha biashara ya kimataifa inafanyika kwa kufuata sheria, mikataba na kanuni zinazojadiliwa na kukubalika na Nchi Wanachama.

NA KWA KUWA kuridhiwa kwa Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia kutatoa fursa kwa Tanzania kunufaika na Mkataba wa Uwezeshaji Biashara ambao utasaidia:

(a) Kupunguza gharama za ufanyaji biashara duniani na kuongeza biashara ya kimataifa;

(b) Kuleta manufaa zaidi nchini ikilinganishwa na gharama za utekelezaji wake;

(c) Kuongeza biashara na mapato kwa nchi kutokana na wepesi wa mazingira ya kufanya biashara;

(d) Kuongeza uzalishaji na ajira;

(e) Kupata misaada mbalimbali ya kifedha na kiutalaam;

(f) Kupata mafunzo mbalimbali ambayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwajengea uwezo watumishi kwenye kazi zao;

(g) Kufaidika na fursa nafuu za biashara zinazotolewa kwa nchi maskini na zinazoendelea kwa mfumo wa "bila ushuru bila ukomo" *(duty free quota free – DFQF)* au tozo ndogo za ushuru zinapofanya biashara na mataifa yenye uchumi mkubwa;

(h) Kupungua gharama za ufanyaji na kupelekea biashara, uzalishaji na ajira kuongezeka;

(i) Kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha na huduma za kiufundi;

(j) Kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji;

(k) Kupanua wigo wa fursa ya ushiriki katika kufanya biashara na uongezaji thamani;

(l) Kupunguza mianya ya rushwa;

(m) Kuchochea utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini *(BluePrint for Regulatory Reform to Improve Business Environment)*; na

(n) Kuimarisha nafasi ya Tanzania katika viwango vya kimataifa vya ufanyaji biashara *(Ease of Doing Business)* na hivyo kuifanya Tanzania kuvutia zaidi uwekezaji katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.

NA KWA KUWA uchambuzi wa kina uliofanywa umebaini kuwa Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia haukinzani na sheria, kanuni na taratibu zinazotawala masuala ya biashara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na faida ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia na manufaa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Saba na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia *(The Protocol Ammending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization - WTO)* ili kuufanya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara kuwa sehemu rasmi ya Mkataba wa *WTO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

AZIMIO LA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA LA KURIDHIA ITIFAKI YA MWAKA 2014 YA MAREKEBISHO YA MKATABA WA MARRAKESH ULIOANZISHA SHIRIKA LA BIASHARA LA DUNIA (PROTOCOL AMMENDING THE MARRAKESH AGREEMENT ESTABLISHING THE WORLD TRADE ORGANISATION - WTO) - KAMA LILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Shirika la Biashara la Dunia (World Trade Organization - WTO) ni Shirika la Kimataifa lililoanzishwa tarehe 1 Januari 1995, ili kusimamia taratibu za kibiashara duniani. Shirika hilo kwa sasa lina jumla ya nchi wanachama 164 na Tanzania ni moja ya nchi wanachama waanzilishi. Lengo kuu la Shirika hilo, ni kuhakikisha kuwa Biashara ya Kimataifa inafanyika kwa uhuru kwa kufuata Sheria, Mikataba, Kanuni zinazojadiliwa na kukubalika na nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na jitihada zilizofanywa na WTO kuhakikisha biashara inafanyika kwa wepesi, bado kuna changamoto za wingi wa ada na tozo (multiple fees and charges); kanuni nyingi za biashara ambazo zinasimamiwa na mamlaka tofauti; na vikwazo visivyo vya lazima vya kiushuru na visivyo vya kiushuru ambavyo huongeza gharama za kufanya biashara duniani. Hivyo, ili kushughulikia changamoto hizo na kupunguza gharama za kufanya biashara duniani, nchi wanachama wa WTO zilikubaliana kuwa na utaratibu wa kisheria wa kimataifa unaojitegemea, ulio wazi na mwepesi utakaotumika kama mwongozo. Hii ilizilazimu nchi hizo kuanza majadiliano ya kuanzishwa kwa Mkataba wa Uwezeshaji Hiashara (Trade Facilitation Agreement - TFA) mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, Baada ya Mkataba huo kukamilika, nchi wanachama wa WTO zilianza maandalizi ya Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa *Marrakesh* ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (Protocol Ammending The Marrakesh Agreement Establishing The World Trade Organization - WTO) ambayo ilikamilika mwaka 2014. Kulingana na Kifungu cha 3 cha Ibara ya 10 ya Mkataba wa WTO, Itifaki hiyo ya marekebisho ya Mkataba wa WTO, ilipaswa kuridhiwa na theluthi mbili (2/3) ya nchi wanachama ili Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (TFA) uweze kuwa sehemu rasmi ya Mkataba wa WTO. Mkataba huo wa Uwezeshaji Biashara ulianza kutumika rasmi tarehe 22 Februari 2017, baada ya Itafiki ya Marekebisho ya Mkataba wa WTO kuridhiwa na nchi wanachama 112 kati ya wanachama 164 wa WTO. Hadi kufikia tarehe 1 Oktoba 2019, nchi wanachama 146 zilikuwa tayari zimekwisharidhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa WTO. Hii inamaanisha ni nchi wanachama 18 pekee, ikiwemo Tanzania ndio hazijaridhia Mkataba huo hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, Itifaki hiyo ina vipengele muhimu vifuatavyo ambavyo nchi yetu imevizingatia:

Ibara Na. 1: Uchapishaji na Upatikanaji wa Taarifa (Publication and Availability of Information):

Mheshimiwa Spika, Eneo hilo linahusu nchi wanachama kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu zinazohusiana na utaratibu na kanuni za kufanya biashara zinachapishwa na kupatikana kwa wadau kwa urahisi. Hatua hiyo itachochea juhudi zinazoendelea za Serikali za kuhakikisha wadau hususan Sekta Binafsi wanapata taarifa muhimu kuhusu fursa, sheria, kanuni na sera za biashara kwa wakati kwa kutumia mifumo ya kisasa.
Serikali kupitia taasisi zake za TRA, TBS, BRELA na nyinginezo imekuwa ikichapisha na kusambaza taarifa mbalimbali za biashara kwa rijia ya machapisho na mtandao. Taarifa hizo husambazwa kwa njia mbalimbali zikiwemo vyombo vya habari, semina na warsha za wadau kwa kutaja machache.

Ibara Na. 10 (4): Dirisha Ia Pamoja la Forodha la Huduma (Electronic Single Window System):

Mheshimiwa Spika, Eneo hilo linahusu kila nchi mwanachama kurahisisha namna ya kushughulikia mahitaji ya wafanyabiashara, hususan kwenye kodi/forodha, kwa kuanzisha mfumo utakaoziunganisha taasisi zote muhimu pamoja na wadau wengine wanaohusika na uingizaji na utoaji wa mizigo bandarini ambao unajulikana kitaalam kama Dirisha la Pamoja la Forodha la Huduma. Licha ya kuwa Serikali imekwishaanza kulifanyia kazi eneo hilo, kupitia Mkataba huo, Serikali ina fursa ya kuimarisha eneo hilo kwa kuhakikisha huduma kama hiyo inasambaa nchini kote na kufanyika kwa viwango na ufanisi wa kimataifa.

Ibara Na. 11: Uhuru wa Upitishaji Mizigo/bidhaa (Freedom of Transit):

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo inatoa maelezo na utaratibu utakaotumika kupitisha mizigo kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine (transit goods). Ibara hiyo iliwekwa ili kuhakikisha kuwa nchi hazizuii au kuweka vikwazo visivyo vya lazima kwa mizigo inayopita. Lengo ni kuhakikisha kuwa biashara ya upitishaji mizigo inaendelea kufanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi husika. Kwa mantiki hiyo, bidhaa zitakuwa zinaruhusiwa kupita nchini kwa kufuata utaratibu wa kawaida wa ndani ya nchi ikiwa ni baada ya kuingia nchini, kukaguliwa, kulipa kodi na tozo stahiki na kuruhusiwa kusafirishwa kama mzigo unaopita (on transit).

Utaratibu unaotumika nchini wa upitishaji mizigo (transit goods) ambao pia ni utaratibu wa EAC kupitia mfumo wa Himaya Moja ya Forodha (EAC Single Customs Territory) unahusisha mteja kulipia kodi ya uingizaji mizigo kwenye mamlaka ambako mizigo itaishia (destination model). Kodi, ushuru, tozo na ada zinazohusu mizigo inayopita hapa nchini (transit goods) zinalipwa na mteja kwenye mamlaka za hapa nchini. Utaratibu huohuo ndio ulioelezewa katika Ibara ya 11(2). Aidha, Ibara 11(16) inahamasisha nchi wanachama kushirikiana katika kurahisisha kupitisha mizigo

hususan katika maeneo ya tozo, taratibu na mahitaji ya kisheria, na mifumo inayotumika. Kwa mantiki hiyo, mifumo ya kodi, tozo, ada na ushuru mbalimbali ambao unatumika kwa sasa nchini utaendelea kutumika na hivyo hakutakuwa na madhara yoyote katika mapato ya nchi yetu.

Ibara Na. 13, 14 na 19: Maeneo ya Upendeleo kwa Nchi Changa na Zinazoendelea (Special and Differential Treatment-S&DT):

Mheshimiwa Spika, Ibara hizo ni mahsusi na zitatoa haki na wajibu wa upendeleo kwa nchi changa na zinazoendelea. Ibara ya 13(2&3) inatoa uhuru kwa nchi hizo kutekeleza Mkataba huo kulingana na uwezo wao wa kimaendeleo, kifedha, kitaasisi na mahitaji ya kibiashara. Ibara ya 14(1)(a,b,c) & (2) inatoa haki na wajibu kwa nchi changa na zinazoendelea kugawa matakwa ya Mkataba katika maeneo ya Kundi A, B na C. maeneo ya Kundi A ni shughuli ambazo tayari Serikali imejiridhisha kuwa utekelezaji umekwishaanza na hivyo kutohitaji muda wala rasilimali za ziada kwa utekelezaji wake. Kundi B ni maeneo ambayo Serikali inatahitaji muda zaidi wa utekelezaji. Kundi C ni maeneo ambayo Serikali itahitaji muda na msaada wa kifedha na kiufundi kuyatekeleza. Pia Ibara hiyo inatoa uhuru kwa nchi hizo kutekeleza matakwa hayo kwa awamu. Vile vile, Ibara ya 19 inaruhusu nchi hizo kuhamisha maeneo inayotaka kuyatekeleza kutoka Kundi moja kwenda lingine. Kwa mujibu wa vifungu hivyo, nchi hizo ikiwemo Tanzania zina uhuru wa kujifanyia tathmini na kupendekeza maeneo ya utekelezaji ambayo itapenda kuyaweka kwenye kundi A, B na C. Fursa hiyo itasaidia nchi changa ikiwemo Tanzania kujipanga vizuri katika kutekeleza Mkataba huo hususan maeneo ya kundi B na C. Fursa hizo zitaongeza vyanzo vya kifedha na huduma za kiufundi kwa ajili ya kujenga uwezo zaidi kwenye maeneo ya uwezeshaji biashara.

Ibara ya 23: Muundo wa Kitaasisi (Institutional Arrangements):

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo inaweka utaratibu wa kitaasisi wa kutekeleza Mkataba katika ngazi ya WTO na kwa kila nchi

mwanachama. Ibara ya 23(1) inaanzisha Kamati ya Uwezeshaji Biashara (Committee on Trade Facilitation) ambayo itasimamiwa na Sekretarieti ya WTO. Kamati hiyo inaundwa na wajumbe kutoka kila nchi mwanachama na ina wajibu wa kurejea utekelezaji wa Mkataba katika miaka minne kutoka kuanzishwa kwa Mkataba na mara kwa mara baada ya kipindi hicho. Kamati hiyo hukutana mara kwa mara katika Makao Makuu ya Shirika la Biashara la Duniani ambapo Tanzania huwakilishwa na Ubalozi wetu uliopo Mjini Geneva.

Ibara ya 23(2) inatoa wajibu kwa kila nchi mwanachama kuanzisha na/au kuendeleza Kamati za Kitaifa za Uwezeshaji Biashara zilizopo. Lengo la Kamati hiyo ya Kitaifa ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa vipengele vya Mkataba katika kila nchi mwanachama wa WTO.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa WTO wa Uwezeshaji Biashara unashabihiana kwa kiasi kikubwa na masuala ya uwekaji wa mazingira wezeshi na endelevu ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na Mpango wa *Blueprint* ambao Serikali inaendelea na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kwa nafasi ya pekee kabisa kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutoa msukumo wa kipekee katika kuboresha na kuimarisha mazingira bora na wezeshi ya .ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Msukumo huo ni chachu muhimu katika kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda ambayo ni ajenda kuu ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa niwasilishe Azimio husika.

Inncocent L. Bashungwa (Mb)
WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA
11 Novemba, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mheshimiwa Murad una muda usiozidi dakika 10.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marakeshi ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na kuweza kufika siku hii ya leo, lakini pia naomba niishukuru Ofisi zote zilizoweza kutusaidia hadi kufikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba yote yaliyopo katika taarifa yangu hii yaweze kuingizwa kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utangulizi; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya Bunge ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na aya ya 7(1)(b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ina jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kupokea Azimio hili, Kamati ilichambua na kujadili maudhui ya Mkataba husika na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao Kamati imetoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna Kamati ilivyoshughulikia hoja hii baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu. Tarehe 6 Novemba, 2019, Kamati ilikutana na kupokea wasilisho la Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Dunia. Maelezo yaliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya ambaye yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 7 Novemba, 2019, Kamati ilipokea uchambuzi wa Sekretarieti ya Kamati juu ya Dhana ya Itifaki hii ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia ambayo inapendekeza kuongeza Mkataba wa uwezeshaji biashara *(TFA)* kuwa sehemu ya Mikataba ya *WTO*, pamoja na vipengele vya kisheria katika Itifaki hii. Tarehe 9 Novemba, 2019, Wizara ya Viwanda na Biashara iliwapatia wajumbe Semina ya kujenga uelewa kuhusu itifaki hii. Semina hiyo iliiwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake. Tunashukuru sana kwa semina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chimbuko la Itifaki; Mkataba wa Marekebisho wa Marrakesh unatekelezwa na Nchi Wanachama wa Shirika la Biashara la Dunia *(World Trade Organization)* ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia tangu mwaka 1955. Shirika hilo lilipoanzishwa uanachama wa Tanzania ulikuwa ni wa moja kwa moja kutokana na kuwa mwanachama kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Forodha na Biashara. Hivyo, Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (*Trade Facilitation Agreement - TFA*) ulianzia katika makubaliano ya awali ya *WTO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa *WTO* walianza rasmi majadiliano kuhusu Mkataba wa Uwezeshaji

Biashara (*WTO Trade Facilitation Agreement – TFA*) mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati; ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali ya muhimu kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilirejea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa na kujiridhisha kuwa hakuna kipengele cha Katiba wala sheria yoyote itakayokiukwa kwa kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilizingatia umuhimu wa kujiridhisha kuhusu hasara na madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia itifaki hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna madhara ya moja kwa moja yanayotokana na kuridhia itifaki hii. Madhara ambayo yalikuwa yakitazamiwa ni kuwa mkataba ungeweza kusababisha nchi maskini na zinazoendelea kushindwa kutekeleza viwanda vyao vichanga *(infant industries).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu una ibara mbalimbali, Kamati imepitia ibara zote na tunaomba ibara zote ziingie katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania kwa sasa inajielekeza katika kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda na ukuaji wa viwanda hivyo unategemea mazingira mazuri ya kufanyia biashara ambalo ni lengo kuu la mkataba huu.

Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu huo Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba huu kwa lengo la kuboresha zaidi mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuridhia Mkataba huu, naomba nitoe maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo naomba yaingie moja kwa moja kutokana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wenzako wote kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda sana kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Eng.* Manyanya, Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili Tukufu. Orodha yao yote naomba iingie katika *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake wote; Makatibu wa Kamati, Bi. Zainabu Mkamba na wenzake wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa wasilisho lako.Sasa tunakwenda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; Mheshimiwa Cecil Mwambe una muda usiozidi dakika tano.

MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KURIDHIA ITIFAKI YA MAREKEBISHO YA MKATABA WA MARRAKESH ULIOANZISHA SHIRIKA LA BIASHARA LA DUNIA - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

(Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization**)**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 53(6)(b) ikisomwa pamoja na aya ya 7(1)(b) ya nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ina jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kupokea Azimio hili, Kamati ilichambua na kujadili maudhui ya Mkataba husika na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao Kamati imetoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization).

2.1 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu:-

i) Tarehe 6 Novemba, 2019 Kamati ilikutana na kupokea wasilisho la Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Dunia, maelezo yaliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara Mhe. Eng. Stella Manyanya ambaye yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuridhia Mkataba huu;

ii) Tarehe 7 Novemba, 2019, Kamati ilipokea uchambuzi wa Sekretarieti ya Kamati juu ya Dhana ya Itifaki hii ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Dunia ambayo inapendekeza kuongeza Mkataba wa uwezeshaji biashara (TFA) kuwa sehemu ya Mikataba ya WTO, pamoja na vipengele vya Kisheria katika Itifaki hii, uchambuzi huu uliwasaidia wajumbe kupatauelewana kuwaweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii; na

iii) Tarehe 9 Novemba, 2019, Wizara ya Viwanda na Biashara iliwapatia wajumbe Semina ya kujenga uelewa kuhusu itifaki hii. Semina hiyo iliiwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake.

3.0 CHIMBUKO LA ITIFAKI

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu wa Marekebisho wa Marrakesh unatekelezwa na nchi

wanachama wa Shirika la Biashara la Dunia (World Trade Organization) ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa mwanachama wa Shirika la Biashara la Dunia tangu mwaka 1995. Shirika hilo lilipoanzishwa uanachama wa Tanzania ulikuwa ni wa moja kwa moja kutokana na kuwa mwanachama kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Forodha na Biashara (General Agreement on Tariffs and Trade - GATT) wa Mwaka 1947.

Hivyo, Mkataba wa uwezeshaji biashara (Trade Facilitation Agreement - TFA) ulianzia katika makubaliano ya awali ya WTO hususani kwenye Mkataba wa GATT wa mwaka 1947. Makubaliano hayo yalijumuishwa kwenye baadhi ya Ibara za Mkataba huo ambazo ni Ibara ya V (Freedom of transit), Ibara ya VIII (Fees and formalities connected with importation and exportation) na Ibara ya X (Publication and administration of trade regulation).

Mheshimiwa Spika, Nchi wanachama wa WTO walianza rasmi majadiliano kuhusu Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (WTO Trade Facilitation Agreement – TFA) mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2013 huko Bali, Indonesia. Matokeo ya majadiliano hayo ni kupitishwa kwa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (TFA). Baada ya Mkataba huo kupitishwa na Mawaziri wa nchi wanachama wa WTO, majadiliano ya uandaaji wa Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa WTO (Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the WTO) itakayojumuisha Mkataba huo kwenye Mikataba ya Shirika la Biashara Duniani yalianza rasmi.

4.1 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza

madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilirejea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa na kujiridhisha kuwa hakuna kipengele cha Katiba wala sheria yoyote itakayokiukwa kwa kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Mkataba wa Uwezeshaji Biashara ambao umepelekea kuwepo Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia umegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ina Ibara 12 za utekelezaji, ya pili ina Ibara 10 inajumuisha maeneo maalum ya upendeleo kwa ajili ya nchi masikini na zinazoendelea, na sehemu ya mwisho ambayo ina Ibara 2 inayohusu masuala ya Muundo wa Kitaasisi.

Vilevile, Kamati ilitafakari na kujiridhisha juu ya faida zinazoweza kupatikana kutokana na kuridhia Itifaki hii ikiwa ni pamoja na;-

i) Kuendelea kunufaika na fursa nafuu za biashara zinazotolewa kwa nchi masikini na zinazoendelea kwa mfumo wa bila ushuru bila ukomo (duty free quota free – DFQF) au tozo ndogo za ushuru zinapofanya biashara na Mataifa yenye uchumi mkubwa;

ii) Nchi kuendelea kupata Misaada ya kitaalamu na kifedha. kwa upande wa kitaalamu, Maafisa wa Serikali chini ya ufadhili wa WTO wataendelea kupata mafunzo

ambayo yatawasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwajengea uwezo zaidi kwenye kazi zao, kwa mfano mafunzo ya juu ya biashara (advanced Trade Policy Course), na misaada ya kifedha, kupitia program mbalimbali chini ya Shirika hili kama vile Enhanced Integrated Framework (EIF);

iii) Kuongezeka kwa uwazi na uwajibikaji, hivyo kupunguza mianya ya rushwa kwa nchi wanachama wanapofanya biashara; na

iv) Tanzania kuendelea kupata urahisi kwenye utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa kutumia chombo cha usuluhishi cha WTO (Dispute Settlement Mechanism).

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilizingatia umuhimu wa kujiridhisha kuhusu hasara au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia Itifaki hii. Napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba hakuna madhara ya moja kwa moja yatakayotokana na kuridhia Itifaki hii. Madhara ambayo yalikuwa yakitazamiwa ni kuwa mkataba ungeweza kusababisha nchi masikini na zinazoendelea kushindwa kuendeleza viwanda vyao vichanga (infant industries).

Hata hivyo, Ibara ya 13, 14 na 19 ya Mkataba wa uwezeshaji biashara – TFA unatoa upendeleo maalum kwa nchi changa na zinazoendelea (Special and Differential Treatment – S & DT). Mkataba huu unatambua changamoto za kimaendeleo katika nchi changa, hivyo unatoa upendeleo maalum kwa nchi hizo katika utekelezaji wa masharti ya Mkataba. Upendeleo huo ni pamoja na muda mrefu wa utekelezaji, misaada ya kifedha na kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati ilijiridhisha hatua zilizofikiwa katika Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kuanza rasmi tarehe 22 Februari baada ya Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa WTO kuridhiwa na nchi wanachama 112 kati ya wanachama 164. Idadi hiyo ni zaidi ya theluthi mbili ya nchi wanachama iliyotakiwa na Ibara ya 10(3) ya Mkataba huo uanze kutumika rasmi.

Nanukuu: Article 10(3) **"Amendments to provisions of this Agreement, or of the Multilateral Trade Agreements in Annexes 1A and 1C, other than those listed in paragraphs 2 and 6, of a nature that would alter the rights and obligations of the Members, shall tahe effect for the Members that have accepted them upon acceptance by two thirds of the Members and thereafter for each other Member upon acceptance by** it". **Mwisho wa Kunukuu.**

Mheshimiwa Spika, hadi kufika tarehe 2 Oktoba, 2019 nchi wanachama 146 zilikuwa zimekwisharidhia Mkataba huo, isipokuwa nchi wanachama 18 pekee ikiwemo Tanzania ndio bado hazijaridhia Itifaki hii. Aidha, nchi zote za SADC zimekwisharidhia Itifaki hii isipokuwa Tanzania.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Mkataba wa Uwezeshaji Biashara (WTO Trade Facilitation Agreement – TFA) umeweka utaratibu wa pamoja (harmonized procedures) katika kushughulikia masuala ya uwezeshaji biashara na kuweka mfumo wa kisheria (legal framework), muongozo na msukumo wa kimataifa kwa nchi wanachama wa WTO kwenye kutatua changamoto za ufanyaji biashara, na

Kwa kuwa, Tanzania kwa sasa inajielekeza katika

kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda na ukuaji wa viwanda hivyo unategemea mazingira mazuri ya kufanyia biashara ambalo ndio lengo kuu la mkataba huu.

Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu huo Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba huu kwa lengo la kuboresha zaidi mazingira ya ufanyaji wa biashara nchini.

Pamoja na kuridhia Mkataba huu, naomba nitoe maoni na mapendekezo ambayo Kamati imeona ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23 ya Mkataba huu inataka kuanzishwa kwa Kamati ya Uwezeshaji wa Biashara itakayosimamia utekelezaji wa masharti ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mkataba kila baada ya miaka minne (4). Aidha Ibara ya 23(2) ya Mkataba inazitaka nchi wanachama kuanzisha Kamati ya Uwezeshaji Biashara kwa ajili ya kuratibu biashara ndani ya nchi lakini pia kusimamia utekelezaji wa masharti ya Mkataba huu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza makubaliano ya Mkataba huu kwa ukaribu na kwa ufanisi kupitia Kamati hiyo ya uwezeshaji biashara nchini. Aidha, kwa kupitia Kamati hiyo Serikali iandae Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Mkataba huu ili kurahisisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa masharti ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Uwezeshaji Biashara unalenga kurahisisha ufanyaji wa biashara kwa kuweka utaratibu wa pamoja na mfumo wa sheria kwenye ufanyaji wa biashara. Hivyo Serikali itekeleze kwa ufanisi Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (Blueprint for

Regulatory Reform to Improve Business Environment) ili kuimarisha nafasi ya Tanzania katika viwango vya kimataifa vya urahisi wa ufanyaji biashara (Easy of Doing Business) na kupelekea kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa viwanda nchini.

6.1 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Itifaki hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

1. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb M/Mwenyekiti

3. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb Mjumbe
4. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb Mjumbe
5. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb Mjumbe
6. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb Mjumbe
7. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb Mjumbe
8. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb Mjumbe
9. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb Mjumbe
10. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb Mjumbe
11. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb Mjumbe
12. Mhe. Zainab Mndolwa Amiri, Mb Mjumbe
13. Mhe. Machano Othman Said, Mb Mjumbe
14. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb Mjumbe
15. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb Mjumbe
16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb Mjumbe
17. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb Mjumbe
18. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb Mjumbe
19. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb Mjumbe
20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb Mjumbe
21. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb Mjumbe
22. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb Mjumbe
23. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhan, Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria Bw. Mossy Lukuvi pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

Suleiman Ahmed Saddiq, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA
13 Novemba, 2019

MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha maoni kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara Dunian *(Protocol Amending The Marrakesh Agreement Establishing The World Trade Organization – WTO)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara Duniani. Marekebisho ya Mkataba huu yana lengo la kuweka urahisi katika ufanyaji wa biashara baina ya mataifa mbalimbali. Marekebisho hayo pia yalilenga kubadili Muundo wa *WTO* ili kuhakikisha kunakuwepo na mazingira rafiki ya kuwasaidia na kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara kwa urahisi katika nchi wanachama wa Shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya ibara mbalimbali za itifaki; mkataba huu wa marekebisho una jumla ya Ibara 24 ambazo zinaonesha jinsi gani kutakuwepo na unafuu katika ufanyaji wa biashara mbalimbali baina ya mataifa wanachama wa mkataba huu. Pia jinsi gani sheria za ndani za nchi mwanachama zinavyotakiwa kujielekeza katika mkataba huu ili kuondoa vikwazo vyote vya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani itaangalia baadhi ya Ibara ambazo tunaona zinatakiwa kutiliwa mkazo zaidi katika mazingira yetu ya ufanyaji wa biashara, kwani vikwazo hivyo (changamoto za ufanyaji wa biashara ya kimataifa) kwa njia moja ama nyingine vinatumiwa na mamlaka zetu za kodi na tozo mbalimbali kuhakikisha biashara nyingi hazishamiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 1 inahusu utangazaji na upatikanaji wa taarifa muhimu za kibiashara kwa nchi mwanachama, wafanyabiashara na mtu yeyote anayehitaji kufahamu kuhusiana utaratibu wa biashara yoyote inayoweza kufanyika kimataifa. Ibara hii ni muhimu sana kwa Tanzania na Watanzania kwani Watanzania wana

bidhaa nyingi sana zinazozalishwa ndani na bidhaa hizo zinahitajika sana nje ya nchi, lakini tatizo la taarifa za utaratibu na mahitaji ya kiushuru ili kuweza kufanikisha biashara hiyo bado kuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutokufahamu mahitaji ya kama mtu anataka kufanya biashara nje na pale anapokuwa na taarifa anakumbana na tozo na kodi ambazo zinamfanya ashindwe kufanya biashara kutokana na wingi na ukubwa wa kodi. Katika hili rejea wafanyabiashara wa dagaa waliokuwa wanasafirisha nje katika Wilaya ya Kilwa walioshindwa kufanya hivyo kutokana na kodi na tozo kuwa kubwa kuliko bei ambayo ipo kwenye soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii itaondoa udanganyifu pia kwa wafanyabiashara kwani taarifa za kila bidhaa baina ya nchi mwanachama zitakuwa zinapatikana kwa uwazi zaidi na hivyo mamlaka za kikodi zitakuwa zinafahamu kila kitu ili kuhakikisha haki inatendeka katika ulipaji stahiki wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 2 ya mkataba inatoa fursa kwa nchi mwanachama kutoa ushauri kulingana na mfumo wa sheria na taratibu za kibiashara pamoja na kikodi za nchi mwanachama kabla ya biashara kuanza na kama kutakuwa na uwezekano wa marekebisho basi unaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inashauri kuwa kunawezekana kuwepo na marekebisho madogo kwa nchi mwanachama kuhusiana na ushuru mbalimbali ili kurahisisha ufanyaji wa biashara. Hiki kitu ni muhimu sana katika kuwavutia wafanyabiashara toka nje na kwenda nje, na huu ni mtihani kwa taasisi na mamlaka zetu za kodi na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 7 ya mkataba inahusu urahisishaji na usahihishaji wa utoaji wa mizigo inayoingia au kutoka kwenye nchi mwanachama kwa kuwa na utaratibu maalum katika uandaaji wa nyaraka za mizigo sambamba na malipo kwa njia ya kielekroniki. Hii yote ni

katika kuhakikisha biashara zinafanyika kwa haraka na katika mazingira ambayo ni wezeshi. Kwa utaratibu huu ni dhahiri mizigo ya aina yoyote ile hata kama zile *perishable goods* itaweza kufika pale inapohitajika kufika kwa muda uliokusudiwa bila ya kutokuwepo na uharibifu wowote ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 inatoa usaidizi katika kujengewa uwezo na uelewa kwa mataifa wanachama toka nchi zinazoendelea kwa lengo la kurahisisha ufanyaji wa biashara katika nyanja zote. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona jambo hili ni jema sana na hivyo fursa kama hii sio ya kuiachia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona litakuwa ni jambo jema kama sheria zetu zinazosimamia biashara ya nje pale ambapo vifungu vya ibara katika mkataba huu vimewekwa vizuri zaidi kwa wafanyabiashara basi vifungu vya sheria zetu virekebishwe/ viuhishwe ili kuakisi maudhui iliyotumika katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni sababu yoyote ile ya msingi kwa Tanzania kutokuridhia Mkataba huu wa Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara Duniani, kwani manufaa ya uridhiwaji wake ni makubwa sana kwa Tanzania na Watanzania wenyewe, hasa wale ambao wanahitaji kufanya biashara za nje kutokana na ukweli kwamba tuna bidhaa nyingi za kuuza nje ya nchi kuliko zile tunazoweza kununua kununua nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Cecil Mwambe, wewe ni mtu mwema sana, umezingatia muda. Lakini kabla sijaitoa hoja hii muijadili, nitumie tu mamlaka niliyonayo niongeze muda usiozidi dakika 30 ili tushughulike na maazimio haya matatu.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge maazimio ni hayo matatu, mtachangia kwa kadri utakavyoona, muda usiozidi dakika tatu, maana ni kukubali kuridhia au kutokukubali kuridhia, basi, mengine haya ni mbwembwe. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndiyo hivyo, sasa nina orodha nimeletewa hapa tuanze; Mheshimiwa Mbene.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

MWENYEKITI: ...eneo hili kwa sababu wewe umekuwa kule kwa muda mrefu; tusaidie.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naridhia hizi itifaki zote ambazo tunataka kuzipitisha hapa, lakini nataka nijikite kwenye hiyo ya *Montreal*, Itifaki ya *Montreal*. Hii ni itifaki muhimu sana na ninaamini kama ingekuwa dunia haikupitisha hii saa hizi tungekuwa tunazungumzia hali mbaya sana kwa afya zetu kuhusiana na jinsi ambavyo tabaka ya *ozone* ambayo ingeshakuwa imeharibika kwa kiasi kikubwa sana. Itifaki hii sasa hivi inaendelea kulenga kuboresha kanda zetu au nchi mbalimbali jinsi ambavyo inajiwekea sasa mikakati zaidi ya kuhakikisha kuwa inaendelea kuzingatia utekelezwaji wa itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Tanzania ni muhimu sana kwa sababu tumeona kabisa jinsi ambavyo matatizo ya tabianchi yanatuathiri, na athari zinazotokana na mmomonyoko au ubomokaji wa *ozone layer* ni mbaya kuliko hata zile tunazozizungumzia za masuala ya *carbon dioxide.* Kwa hali hiyo nafikiri *protocol* hii ni muhimu sana kuizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu ni moja tu kwa Serikali; itambuliwe kuwa huko nyuma utafiti uligundua kuwa hii *ozone* au hili tabaka linaathirika sana na kemikali zinazotumika katika kutengeneza viyoyozi, kutengeneza majokofu na kutengeneza haya makopo ya dawa za

kupulizia. Na hivi karibuni tumeona kuwa majokofu na viyoyozi vingi chakavu vinaingia nchini, sijui ni nani anayekagua kuhakikisha kuwa havibebi zile kemikali ambazo huko nyuma ndiyo zilitambulika kuwa zinaathiri hili tabaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuwa kutokana na hii, hii gharama ya kuondoa, ya kusafisha hizi kemikali zilizoko katika matumizi ya wananchi ni kubwa sana. Huko nyuma kulikuwa kuna fungu lilikuwa linatolewa ambalo lilikuwa linapitishwa Umoja wa Taifa, nakumbuka kwa Tanzania Umoja wa Taifa walikuwa wanasimamia fungu hilo, kwa hiyo walikuwa wanafanya kazi na viwanda kuhakikisha kuwa wanaondoa hizi kemikali. Sasa sijui kwa sasa hivi kama lile fungu bado linaendelea kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo tu.

MWENYEKITI: Nashukuru sana Mheshimiwa Mbene; Mheshimiwa Salum Rehani, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Othman Machano.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali turidhie hizi itifaki zote tatu na ninapongeza Serikali kwa kuja nazo ili iweze kurahisisha katika utekelezaji wa majukumu yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika eneo lile la kwanza la *Montreal*, ni vizuri sana, nashukuru kwamba turidhie hiyo itifaki, lakini muhimu ni Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha kwamba tunaendelea kuzuia na tunaendelea kuzingatia sheria zilizowekwa kwa manufaa yetu sisi Watanzania. Tusije tukawa *dumping ground,* yaani eneo la kutupa taka ambazo baadaye itakuwa ni sumu kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hilo pia kuna Mjumbe mmoja alichangia kwamba sheria za kodi ndiyo zinafanya sisi tununue vitu chakavu; hiyo sio sahihi. Sahihi ni kwamba tumeweka kodi kubwa kwenye bidhaa ambazo ni

used, yaani bidhaa chakavu ina kodi *20% extra* ili tusinunue bidhaa chakavu, kwa hiyo hiyo *record* ikae vizuri; Serikali imefanya vizuri sana, bidhaa zilizotumika zina kodi ya 20% ili kulinda mazingira yetu, kwa hiyo hiyo *record* ikae vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa upande wa *WTO,* naomba pia itifaki hii Wabunge wote turidhie ili iweze kufanya kazi. Lakini muhimu kuliko yote, tutakaporidhia hizi itifaki za kimataifa ni vizuri sisi kama ndani ya nchi pia tuhakikishe kwamba tunatenda yale ambayo tumekubaliana huko kimataifa. Kwa mfano kwenye hii ya ufanyaji biashara, *ease of doing business,* ni vizuri yale yote ambayo tumekubali tutafanya kimataifa huku ndani ndiyo tuwe na dirisha na tuwe tunafanya vizuri zaidi ili huko nje tuwe wa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwenye *hizo bring business* naomba Serikali ije na hiyo Sheria ya *Blueprint* itekelezwe kwa asilimia 100, bidhaa zetu ziwe na gharama ndogo ya uzalishaji kutokana na *regulatory bodies* nyingi. Na pia kuingia kwenye mfumo mzima wa kufanya kazi kwa kupitia *internet* na urahisi wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa Itifaki ile ya *SADC,* naunga mkono sana kwa sababu changamoto hizi zote ambazo zinahusiana na masuala ya mazingira hakuna namna tunaweza kujitenga kama kisiwa. Kwa hiyo, tufanye kazi kwa pamoja. Sheria zote za nchi za *SADC* zikiwa zinafanana na itifaki tukikubaliana nayo naamini kabisa tutaweza kusaidia nchi yetu kufanya kazi kwa pamoja kwa sababu tunashirikiana katika mambo mengi. Kwa hiyo, itifaki hizi zote naomba Wabunge wote tuunge mkono ili ziweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ombi langu pia; zile itifaki zingine ambazo tuliwekewa kwenye orodha ya ratiba kwamba zitakuja, basi ziletwe, kwa mfano *International Solar Alliance* na itifaki nyingine. Basi na hizo zenyewe zije zote turidhie ile tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja itifaki zote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni; Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Othman Machano, yuko wapi Mheshimiwa Machano?

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima, na pia niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa kuwasilisha maazimio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia hili Azimio la *WTO.* Kwanza naunga mkono uamuzi wa Serikali wa kulileta hapa Bungeni, lakini pia naomba Waheshimiwa Wabunge tulipitishe azimio hili kama maazimio mengine ambayo tumeyapitisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio hili lina umuhimu mkubwa kwa Tanzania katika uendelezaji wa biashara, lakini pia kuzalisha bidhaa bora. Ni vyema kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya mashauri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili, pamoja na kwamba Bunge linaridhia azimio hili, lakini pia kwa upande wa Zanzibar nao waelewe na wafahamu faida ambazo zitapatikana kwa kuridhia azimio hili kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipowasilisha alieleza faida za azimio hili kwa kuzitaja baadhi ya ibara ambazo zitaleta na kuimarisha mshikamano na mtengamano wa kibiashara kwa Tanzania. Kwa mfano Ibara ya 10 inatoa fursa kwa kuweka forodha ya pamoja na mambo mengine ambayo yatasaidia katika uendelezaji wa biashara, lakini pia kulinda na kuimarisha wataalam wetu katika shughuli za uzalishaji na kuweka viwango bora vya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kwamba tulichelewa

kidogo kwa sababu kati ya nchi nyingi tu sisi tulikuwa miongoni mwa nchi 18 ambazo zilichelewa kuridhia azimio hili, lakini leo ni furaha kwamba tumekubaliana na tumeridhia azimio hili. Hivyo kama ulivyozungumza, hatutakiwi kuzungumza sana isipokuwa kuunga mkono azimio hili, na mimi naliunga mkono kwa asilimia mia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Machano kwa mchango wako; Mheshimiwa Zungu, atafuatiwa na Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Gimbi Masaba ajiandae.

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kabla ya yote kwanza nichukue nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuleta maazimio haya yote, na naunga mkono maazimio yote haya matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Azimio la *Montreal*; kuna mashirika ya ndege sio chini ya 25 mpaka 30 yanatumia anga la Tanzania, na kila abiria anatakiwa alipe kodi ya *carbon emission (carbon emission tax).* Nataka kuuliza Serikali, wamejipanga vipi katika kudai pesa hizi ziweze kurudi nchini na kuboresha mazingira ya Mlima Kilimanjaro, tukapanda miti zaidi ya bilioni moja, kwa sababu ndege hizi zinaharibu mazingira yetu hapa nchini. Kwa hiyo, naomba Serikali walione hilo; kama tunalipa kodi na ndege zinatumia anga zetu ni bora tukatafuta namna ya kudai pesa hizi ili zirudi hapa nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu *depreciation* ya *ozone; depreciation* ya *ozone* inatokana na mambo mengi, pamoja na friji. Nchi nyingi zilizoendelea sasa hivi wamepiga marufuku kutumia friji aina ya *Freon;* hizi friji zimepigwa marufuku nchini mwao lakini zinaletwa nchini mwetu, na zikija kwetu zinaharibu mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelimisha wananchi wetu waelewe; hivi sindano ambayo imetumika Ulaya utakubalije Tanzania itumike kama sindano mtumba? Na sasa hivi magari mengi yataacha kutumia petroli na *fossil fuels,*

wataanza kutumia umeme na gesi, magari haya yana hatari ya kuja katika Bara la Afrika na kuharibu mazingira yetu. Kwa hiyo, naomba kama wenzetu Ulaya wamekubali sasa kutumia *HFC 134a, tetphoroicine*, na sisi tukubali kuacha kutumia *freon gas* kulinda mazingira ya Taifa letu na Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana; Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nakubaliana na niishukuru Serikali kwa kuleta haya maazimio, maazimio yote matatu mimi nayaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanazungumza viingereza virefu sana hapa, lakini ukweli ni kwamba dunia hapo inapokwenda sasa ni hatari zaidi. Na nchi yetu, ukiangalia katika zile nchi 10 za Afrika ambazo ziko, wanasema *most likely to be destroyed by climate change,* Tanzania ni nchi ya 10. Na kila nchi imepewa sababu zake za kutoweka; sisi tumepewa sababu za kutoweka kwa mambo ya mafuriko na ukame, *floods and drought.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa kama hivyo ndivyo ilivyo, sisi tumeshaambiwa kwamba *climate change* ni jambo la kidunia, na *ozone layer 0.003%* imeshaharibika na uwezo wa kuirudisha ni mgumu sana kwa sababu nchi za Ulaya ambazo zinatumia viwanda vingi vinavyosababisha mambo ya *greenhouse gases* zinakuwepo; *carbon dioxide, nitrus, methane chlorophene* zinakuepo. Sasa kama sisi hatuna uwezo wa kuzuia hizo maana yake wametupa sababu za nchi yetu kutoweka na nchi yetu kutoweka ni mafuriko na ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi hatuna uwezo wa kuzuia hizo, maana yake wametupa sababu za sisi nchi yetu kutoweka na mafuriko na ukame. Kama ndivyo ilivyo, basi, sisi hatuna namna yoyote ya mpango wowote makusudi zaidi ya kupanda miti, kwa sababu miti ni *carbon sinker*, inachukua

carbon dioxide. Kwa hiyo, lazima tufanye kila namna, kwa kila eneo, kwa kila mkoa, kwa kila sehemu kupanda miti ili kuepuka janga ambalo wametupa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Getere. Mheshimiwa Gimbi Masaba atafuatiwa na Mheshimiwa Omar.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru, nami naomba kuchangia. Napenda tu niseme kwamba Itifaki hii kimsingi imekuja wakati ambao asilimia 80 za maambukizi ya magonjwa yanatokana na kemikali zinazotokana na madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza kuridhia Itifaki ya *SADC,* ni sawa, lakini natoa masikitiko yangu kwamba, pamoja na kwamba tunaridhia Itifaki hii lakini kumekuwa na utaratibu wa kutozingatia umuhimu wa mazingira ya Taifa letu. Ukiangalia bajeti ya mazingira iliyopita ni 0.0. Sasa nilikuwa najiuliza, tunavyozungumza kuridhia Itifaki hii, wakati huo huo Serikali haioni umuhimu wa kuboresha mazingira yetu kupitia bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunakwenda kuridhia vitu kama hivi, bado kwenye taarifa ya Makamu wa Rais imezungumzia asilimia 61 ya ukataji wa miti nchi yetu iko hatarini. Kwa hiyo, pamoja na kwamba Serikali imeleta Azimio hili na huku ukizingatia karibu dawa zote zinatumia kemikali, hata ukiangalia kwenye kilimo chetu, dawa tunazotumia kwenye mahindi zote zinatumia kemikali; ukienda kwenye mboga mboga zote zinatumia kemikali; nataka niiulize Serikali, imejipangaje kuhakikisha kwamba inakuja na utaratibu ambao utawezesha kkutupatia dawa ambazo hazina kemikali? Kwa sababu dawa karibu zote zina kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia, kuhusu suala la *ozone layer*, bado

narudi kule kule kwenye bajeti. Kwenye Bajeti Kuu ya fedha za Maendeleo kulikuwa na sifuri, lakini bado fedha za nje tulipata kiasi cha shilingi milioni 500. Sasa najiuliza, Wazungu wanaona umuhimu wa mazingira wa Taifa letu, lakini sisi hata huu mradi wa *Ozone Layer* hatuoni umuhimu wa kuzuia hili joto ambalo ni hatari kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza suala la mazingira ni lazima turudi kwenye Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 kuhakikisha kwamba inatumika vizuri ipasavyo kuliko ambavyo tunavyozungumza kinagaubaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Omar Juma, wa mwisho hao.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Mimi kidogo mchango wangu utakuwa ni tofauti na wachangiaji waliopita. Kwanza kabisa, naomba kuunga mkono kabisa kabisa, mia kwa mia Itifaki hizi mbili za mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa sababu ni jambo ambalo linatu-*affect* vizazi vya sasa na vizazi vinavyokuja. Nataka nianze kwa kusema, hii *ozone layer* hai-*belong to any state,* wala siyo ya mtu binafsi. Mwenyezi Mungu alipoumba dunia akaweka *ozone layer. The question now rise, why should there be no depletion of ozone layer*? *Ozone layer* ina mambo mawili makubwa; moja, ni *production of oxgen*. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu wa *chemistry,* kwa hiyo, nataka niwalete kwenye *chemistry*. Nafikiri wale wale waliokuwa hawanifahamu, degree yangu ya kwanza ya *Bachelors* ni *Physics* C*hemistry,* lakini ya pili nime-*specialize* kwenye *Chemistry*. Sasa *Ozone layer* ni *producer of oxygen.* O*xygen* ni hii hewa safi ambayo tunaivuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, *ozone layer* Mwenyezi Mungu kaiweka makusudi siyo kwa bahati mbaya ili iwe ni *blanket* au *insulating sheets* ya jua, mionzi inayotokana na jua. Mtakumbuka kwamba jua liko *around 93 million miles from earth surface.* Kwa hiyo, kama ingekuwa ile mionzi ya jua inatupiga *direct,* nafikiri hapa kungekuwa hakuna mtu tena, wala kiumbe kisingeweza kuishi katika dunia hii, lakini kwa sababu ya *ozone layer* ndiyo tunapata *protection.* Mungu atunusuru, siku za the day of *eruption* eeh, wanaita siku ya kufufuliwa. Inasema...

MBUNGE FULANI: *Rise eruption.*

MHE. JUMA HAMAD OMAR: *Yes, rise eruption.* Wanasema hili jua litakuwa karibu sana na sisi; nasi tutakaa sana kabla ya kuhukumiwa. Kwa sababu tutakaa sana, jasho lile litakalotutoka litafika mpaka kwenye mabega, wale wenye dhambi kali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uwepo wa *ozone layer* haukufanywa kibahati mbaya na Mwenyezi Mungu. *I agree* na maazimio haya na hasa lile Itifaki ya *Motreal* na marekebisho yaliyofanywa nchini Rwanda, nakubaliana nao mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nadhani sisi mwanzoni tulifikiri tatizo la *ozone layer* kutobokatoboka, kuwa na matundu ni kwa sababu ya kemikali za aina zinazoitwa *CFS (Chlorofluorocarbons),* lakini baadaye tukagundua kwamba unaweza uka-*get rid of chemical* inayoitwa *chloralfluorocarbons* hasa kwenye utengenezaji wa friji, jokofu, *air conditions* na kadhalika kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge. Tukaja na kemikali mbadala inaitwa *hydrochlorolfluorocarbons.* Hata hivyo, *as we say* na kwa mujibu wa *protocol* hii ya *Montreal* kuna *a lot of chemicals* ambazo zinasababisha mmomonyoko wa *ozone layer.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo siyo la Tanzania. Nataka nisikubaliane na Kambi ya Upinzani kidogo na wale ambao walikuwa wanafikiri kwamba kuleta friji mbovu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda!

MBUNGE FULANI: Mwongezee!

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe elimu.

MWENYEKITI: Kwa sababu ya *field* yako hiyo, natumia mamlaka yangu hayo, ongea kidogo dakika tatu zaidi. *(Makofi)*

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu *problem* iko katika nchi zilizoendelea. Suala la haya mafriji, majokofu, kutengenezwa kwa kutumia hiyo kemikali mbadala, *hydrofluoro*carbon siyo tatizo. Tatizo ni kwamba nchi zilizoendelea, zenye viwanda zina *a lot of emission* ya hizi kemikali ambazo huwa ni *distractive. We don't want to talk of hydrofluorocarbons;* na hiyo sasa imeambiwa kwamba nayo ina madhara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kama sikosei kuna kama kemikali za aina sita ambazo zote ni *destructive* ya *ozone layer.* Ukiacha *CFS*, unakuja *hydrofluorocarbon* ambayo sasa hivi inatumika katika utengenezaji wa mafriji, lakini kuna *hydrofluorobromocarbons,* kuna *hydrobromochlorocarbons a number of them;* kuna hizi *chemicals* zinazoitwa *halons* ambazo *is nothing but carbontetrachloride.* Kuna *a lot of chemicals* sasa hivi na hizi hatuzalishi sisi, wanazalisha nchi zilizoendelea, zenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kusema kwamba friji bovu au kifaa chakavu kitaleta *emission* hiyo, siyo kweli. Hata ukinunua friji zima jipya, basi kule kuna *hydrofluorocarbons.* Kwa hiyo, friji inavyofanya kazi, liwe jipya, liwe kongwe lina *emission* ya *hydrofloralcarbons.* Tatizo nasema tena ni nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *solution* ni nini? Kwanza tuzibane nchi kubwa kwamba ipo *side penalt clause* katika ile Itifaki lakini *is not punitive*, wala haitekelezwi. Leo Taifa kama Marekeni, China, Japan, Italy ambazo zina viwanda tukizibana tukawaambia lazima watoe *5% of their budget* kusaidia nchi changa kwa suala la kuharibiana mazingira, hilo litakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, au tukazibana tuwe na *effort* ya pamoja, tufanye *reseach* ili tupate kamikali mbadala. Hiyo inawezekana. Suala la *AIDS*, *HIV*, tuna *research* ya pamoja na mpaka sasa hivi hatujapata dawa, lakini *at least* kuna jitihada *joint efforts* ambazo zinaonekana zitazaa matunda huko baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mataifa haya makubwa waambiwe wapunguze viwanda ambayo huwa vina-*emit* hizo *hydrofuorocarbons otherwise* suala la *ozone layer* litaendelea. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, *again,* naomba kuunga mkono azimio hilo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omar nakushukuru sana kwa mchango wako na ushauri huo, lakini ndiyo haya kwenye *platform* za Kimataifa, nchi zinazoendelea, hoja yetu ndiyo hiyo kwamba hawa walipe. Kwa hiyo, umesema vizuri sana, lakini hujatimiza ahadi yako ile ya kuandika kitabu kwa masuala haya. Mimi nakushauri, andika, una uzoefu mkubwa sana.

Mheshimiwa Rehani.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi hii niweze kuzungumza kidogo. Na mimi naunga mkono Itifaki hii ya Kigali, lakini

napenda kuishauri nchi katika eneo hili kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Tanzania tumetangaza kwamba sera yetu ni Uchumi wa Viwanda. Ila moja kati ya vitu ambavyo vinaleta athari ya hizo *emission* katika *ozone layer* ni aina ya viwanda ambavyo vinatoa *carbonmonoxide* kwa kiwango kikubwa. Sasa sijui katika ile *blueprint* yetu na huo mkakati wa uchumi wa viwanda tumejiandaaje kukabili kiwango kikubwa cha *emission* ambazo zitakuja kuzalishwa hapa ndani ya nchi, pengine nasi kama Tanzania tukatakiwa tutoe fidia kwa uharibifu wa mazingira ya *ozone layer.* Sasa hilo natoa angalizo la mwanzo kabisa kwa nchi, tunapokwenda huko tuwe na tahadhari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, bado ndani ya nchi vile vile hakujawa na mikakati thabiti. Hapo nyuma tuliandaa mpango mkakati unaitwa *REDD (Reduce, Emission, Degradation of Deforestation)* kwa ajili ya kunusuru *emission* zote ambazo zinaweza kutokea, iwe kupitia kwenye madawa na kemikali mbalimbali za viwandani, lakini vilevile kwa *carbon monoxide* ambayo haivunjiki kutokana na miti tuliyonayo kidogo haiwezi kunyonya au kuvuta hewa yote ya *carbon monoxide.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine vilevile, ndani ya nchi bado mkakati wa kuwadhibiti watu wenye magari mabovu yanayotoa moshi mwingi njiani na sehemu nyingine haujawekwa na tukaweza kuona kwamba kuna una udhibiti kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi ninaloliona, hata viwanda viwanda vyetu vile vya Wazo, hata ile Songwe vile vya saruji vinatoa moshi mkubwa. Ile ni *pure carbon monoxide* ambayo kuvunjika kwake kunataka kuweko na *emission* nyinginezo ambazo zinaweza kusaidia kuvunja. Sisi tumeviacha vile viwanda, hatuvishauri katika mazingira haya tuliyokuwanayo. Kwa hiyo, tunachangia na sisi katika uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wito wangu nafikiri Wizara inahusika, ikae na wahusika, tuweke mpango thabiti sasa ambao utaweza kudhibiti huo uharibifu wa mazingira kwa hilo eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Haya tunaendelea. Mtoa hoja, tunaanza na Mheshimiwa Prof. Naibu Waziri Sima, dakika tatu tu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mbarawa, nawashukuru Kamati na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ijikite hasa katika kujibu hoja za wenzetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Wamesema yawezekana taasisi ambazo tunazo ni taasisi ambazo hazina viwango, hazina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze tu kwamba, tunaporidhia mkataba kama huu, maana yake Serikali inapata teknolojia, lakini tunapata fedha kwa ajili ya kufanya *capacity building.* Kwa hiyo, eneo hili tunakuwa tumelimaliza kulingana na utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwanya wa rushwa, wamesema kuna *grand corruption,* siyo kweli. Sisi tuna *focal point,* maana yake hizi nchi wanachama ziko *focal point,* hakuna bidhaa inaingia kabla Mkurugenzi wa Mazingira hajaridhia. Akisharidhia, maana yake ile bidhaa haina tatizo. Kwa hiyo, hakuna *compromise* ya kampuni yoyote itakayoingiza bidhaa yake bila sisi kama Serikali na Ofisi ya Makamu wa Rais kukubali kwamba iingie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamepewa semina. Kam mmemsikiliza Mwenyekiti hapa, ameeleza vizuri kwamba Kamati imeshapata semina na

wamekuwa na uelewa mkubwa; na kwa semina hiyo uelewa huo maana yake wametuwakilisha sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili halijaanza leo, nchi imeridhia Mkataba huu wa Vienna tangu mwaka 1993 na kuanzia hapo marekebisho yameendelea. Huu ni mkataba wa sita; tumefanya wa kwanza, wa pili, mpaka wa tano na huu ni wa sita. Kwa hiyo, kama nchi tuna uelewa mkubwa sana kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Nirejee kwa Mheshimiwa Janeth Mbene; ni kweli fungu lipo kama alivyoeleza, linaendelea kwa utaratibu ule ule. Pia namshukuru Mheshimiwa Jitu Soni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zungu ameeleza hoja yake ya msingi sana ambayo nataka kueleza Bunge lako kwamba tunaendelea na utekelezaji kuhakikisha nchi inapata fidia kulingana na uharibifu wa mazingira wa viwanda vya wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Juma Hamad, kwa kweli ametoa elimu ya kutosha sana, Mungu ambariki. Nadhani sasa watu wote wamepata uelewa wa juu ni nini kifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa dakika zako.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mbarawa hitimisha hoja yako kwa muda usiozidi...

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote tena napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii nami kuja kuhitimisha hoja zetu hizi mbili za Maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa michango

mizuri na maekelezo mazuri ambayo wanatupatia hasa kwenye Maazimio haya mawili. Naomba niwahakikishie tu kwamba maoni yao, mawazo yao na fikra zao zote tumezichukua na tutakwenda kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, wameonesha kwa dhati umuhimu mkubwa wa kupambana na *emission* hizi ili kuhakikisha kwamba na sisi Taifa letu na ulimwengu kwa ujumla unakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wote wamechangia vizuri Maazimio yote mawili; kwanza, Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya *SADC* ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu. Kama tunavyojua kwamba *emission* hazina mipaka kwa vile ni juhudi za pamoja, zinahitajika kwa nchi zote za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia na kutoa msisitizo mkubwa kuhusu Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Kigali ya Kupunguza hizi *Emissions* za *HFCs* ambazo zina athari kubwa kama alivyosema Mheshimiwa Juma Hamad.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu, nakubaliana na Bunge kwamba, kwa pamoja hatunabudi kupitisha maazimio haya kwa sababu zina faidi kubwa ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezieleza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana. hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa. Aah, Samahani! Nataka niwahoji; samahani Mheshimiwa Waziri Bashungwa, nataka tumalizane kabisa hapa lisilale zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio haya mawili nitawahoji.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Azimio la kuridhia Marekebisho ya Kigali nchini ya Itifaki ya Montreal kuhusu Kupunguza Uzalishaji na Matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal Inayohusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni (yaani Kigali Amendment On Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCs) to The Montreal Protocol on Ozone Depleting Substances liliridhiwa na Bunge)

(Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya SADC ya Usimamizi wa Mazingira kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu. (The Southern African Development Community Protocol on Environmental Management for Sustainable Development liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashungwa.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kuendesha kikao chetu kwa umahiri mkubwa *always.* Nakushukuru sana. Pia, naishukuru Kamati yangu ya Viwanda, Biashara na Mazingira inayoongozwa na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Suleiman Saddiq pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na maoni na maelekezo wanayozidi kuipa Wizara yangu. Tunashukuru sana Wajumbe wa Kamati pamoja na Mwenyekiti.

Mhehimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote waliochangia na wale ambao hawajapata kuchangia lakini wanakubaliana nami kwamba

hoja hii imeungwa mkono na Wabunge wote. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Wabunge wa Chama Tawala na Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Tunawashukuru kwa kutambua kwamba Serikali imefanya jambo jema sana kuleta *Protocol* hii. Kwa hiyo, tunawashukuru kwa *support* na kuunga mkono hoja ya Azimio la Bunge la Marekebisho ya Mkataba wa *WHO.*

Mhehimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kufanya hivi ni kudhihirisha kwamba suala la kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini ni la kwetu sote, siyo la Chama Tawala wala Upinzani. Mfano, huu ningependa uendelee kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu pale tunaposema vibaya kuhusu nchi yetu, dunia ambayo haiko hapa, wakati mwingine tunaweza tukafanya hivyo kwa ushabiki wa kisiasa lakini hatujui kwamba tunaharibu sifa ya nchi na wakati mwingine kwa ushabiki tu wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kuweka mazingira wezeshi hapa nchini ni suala letu wote, lisiwe la kisiasa, lisiwe la ushabiki wa kisiasa au kiitikadi kwa sababu wote tuna vijana wetu na akina mama ambao wanatafuta ajira na tutatengeneza ajira kwa kupitia ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *protocol* hii ni moja ya jitihada za Serikali, mnafahamu tuna utekelezaji wa *blueprint* na Marekebisho ya Mkataba huu wa *WHO* unaongeza nguvu katika mkakati wa Serikali wa kutekeleza *blueprint* ili miaka inayokuja ile *ranking* ya hiyo ISO *business* basi nchi yetu iendelee ku-*improve* katika hizo *ranking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, nasi tunaahidi baada ya Bunge kuridhia Marekebisho ya Mkataba huu, *Business Facilitation Act,* ambayo tunaiandaa ije Bungeni, basi ni fursa hata Kamati ya utekelezaji wa *protocol* hii tutazingatia katika *Bill* itakayokuja Bungeni maudhui ya sheria hiyo yatazingatia uhitaji wa Kamati itakayosimamia utekelezaji wa huu Mkataba.

Mhehimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, tayari hii Kamati imeshaundwa, lakini tunataka *Business Facilitation Bill* iwe ni fursa ya kuchukua maudhui ambayo tumeyajadili katika mkataba huu yawe pia katika *Business Facilitation Act* na baada ya hapo Kamati hii itatangazwa kwa Umma.

Mhehimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa Machano, hata maandalizi ya Azimio hili tumeshirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na nikuahidi Mheshimiwa Machano pamoja na Bunge hili tutaendelea kushirikiana katika kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania.

Mhehimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh Ulioanzisha Shirika la Biashara ya Dunia (The Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization Uliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Wote wameafiki. Kwa hiyo, Bunge limeridhia Azimio la Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa *Marrakesh* ulioanzisha Shirika la Biashara ya Dunia *(The Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization).*

Hiyo ndiyo kazi yetu ya leo, tumefanya vizuri. Nawashukuru sana kuanzia asubuhi wakati wa maswali,

tumekuja kwenye shughuli ya Maazimio haya muhimu sana; nami niungane nanyi katika hayo mazuri mliyoyasema kuishauri Serikali. Ni eneo muhimu sana katika yote matatu.

Nina tangazo moja kwa Wajumbe wa Kamati ya Kanuni za Bunge. Mnaarifiwa mara tu baada ya shughuli hizi kuahirishwa, kwenda kwenye kikao cha Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sina tangazo lingine, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 14, siku ya Alhamisi saa 3.00 asubuhi.

(Saa 7.25 Mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 14 Novemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)